Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Sita - Tarehe 3 Februari, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Elimu Kibaha kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mfuko wa Fedha za Barabara kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 (*The Annual Report and Accounts of the Roads Funds Board for the Financial year 2005/2006*).

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa na *TCRA Consumer Consultative Council (TCRA – CCC)* kwa miaka inayoishia 30 Juni, 2005/2006/2007. (*The Annual Report and Audited Accounts of the TCRS Consumer Consultative Council (TCRA – CCC) for the years ended 30th June, 2005/2006/2007.*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 68

## Mafunzo ya Msingi kwa Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa baadhi ya Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Kata za Namtumbo kutopata mafunzo ya kujua wajibu wao pamoja na kutokulipwa:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwapa mafunzo ya msingi Wajumbe hao ili wawe na upeo juu ya wajibu wao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 20 Aprili, 2007 katika kikao cha tisa cha mkutano wa Saba wa Bunge lako Tukufu, ofisi yangu ilijibu swali Namba 116 kuhusu Mabaraza ya Ardhi ya Kata na Vijiji kama lilivyoulizwa na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum. Nililifahamisha Bunge lako kwamba Serikali inafahamu kuwa Mabaraza ya Ardhi ya Kata na Vijiji yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa mafunzo kwa Wajumbe wa Mabaraza haya.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoyakabili Mabaraza ya Ardhi ya Kata na Vijiji zinapaswa kushughulikiwa na Halmashauri ambazo ndizo zinaunda na kumiliki Mabaraza hayo. Kwa mara nyingine tena napenda kuziagiza Halmashauri zote nchini kuhakikisha uanzishwaji wa Mabaraza hayo kwa kila Kata na Kijiji unafanyika na kuandaa mipango maalum ya kuwaelimisha na kuwawezesha Watendaji wa Mabaraza hayo katika kutekeleza majukumu yao. Hii ni pamoja na utoaji wa elimu kwa umma juu ya utumiaji wa Mabaraza hayo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Namtumbo mpaka sasa ina jumla ya Kata 12 na Vijiji 61. Katika Kata 8 tayari mafunzo kwa Wajumbe yameshatolewa.

Kata hizo ni Namabengo, Msindo, Mkongo na Rwinga. Kata nyingine ni Namtumbo, Luchili, Mgombasi na Luegu.

Kata zilizobaki ni Kitanda, Lusewa, Magazini na Ligera zinategemea kupatiwa mafunzo hayo kabla ya mwaka huu wa Fedha 2008/2009 kumalizika.

Aidha, katika mipango yake Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo imepanga kuanza na mafunzo kwa Mabaraza ya Kata na kisha kumalizia na Mabaraza ya Ardhi ya vijiji.

Katika kufikia azma hii, Waheshimiwa Wabunge kama Wajumbe kwenye Baraza la Madiwani watoe msukumo kwa Halmashauri ili ziyawezeshe Mabaraza hayo kufanya kazi ipasavyo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niipongeze Serikali na Halmashauri yangu kwa kuanza kuwapa mafunzo baadhi ya Mabaraza ya Kata katika Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, kwanza Mabaraza ya Kata yanafanya kazi yake kisheria na moja ya kazi zao za Wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kata ni kutembelea maeneo yanayolalamikiwa ili kuona hali halisi na kutoa maamuzi stahili.

Kwa maeneo ya Namtumbo sehemu kubwa inayolalamikiwa ni maeneo ya shambani na wanatembea kwa mwendo mrefu porini na wanahatarisha maisha yao kwa kukutana na nyoka wakali lakini hawapati posho.

Je, Sheria hii ya mabaraza haya inasema nini na nani anapasa kuwalipa posho hawa Wajumbe wa Baraza la Kata?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikubali kwamba ni kweli kwamba hawa Wajumbe wa Mabaraza haya wanapata mazingira ambayo ni magumu na wakati mwingine kutembea kwa miguu kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na hata kukutana na nyoka kama anavyosema ni kweli kwa sababu hali halisi ya Bajeti yetu inaonekana kwamba haiwezi kusaidia sana majukumu mengi kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, lakini nilipokuwa najibu swali hili nimesema kwamba Mamlaka ambayo inahusika katika kuendesha mabaraza haya kwa maana ya posho zile za wale Wajumbe, nauli zao na vitu vyote hivyo ni Halmashauri za Wilaya zinazohusika. Ninatambua kwamba ufinyu wa Bajeti unazifanya Halmashauri hizi zishindwe kuhudumia vizuri lakini hili ni suala la kipaumbele tu. Mheshimiwa Mbunge anachotakiwa kufanya hapa ni kuhimiza na kuona kwamba kiasi cha pesa za kutosha kinatengwa kwa ajili ya nauli pamoja na posho kwa ajili ya Wajumbe wa Baraza hili.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini ifahamike kwamba kwa sasa hivi migogoro ya ardhi vijijini ni mikubwa kwa sababu idadi ya watu imeongezeka na ardhi haiongezeki.

Kwa kuwa, migogoro hiyo ni mingi na taratibu za usuluhishi wa Mabaraza haya kuanzia Baraza la Kijiji na Kata unapotaka kukata rufaa unakwenda kwenye Baraza la Wilaya ambako ni mbali na wanavijiji wengi hawana uwezo.

Je, Serikali isingeona ni busara kukata rufaa kutoka kwenye Baraza la Kata kwenda kwenye Mahakama ya Mwanzo badala ya Baraza la Wilaya ambako ni mbali na wakati mwingine Wilaya nyingi bado hazijaunda mabaraza hayo? Je, Serikali inasemaje?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi ninachokielewa hapa ni kwamba Mheshimiwa Simbachawene anaonyesha tu kwamba kuna tatizo kubwa hapa na kwamba namna ambayo inaweza ikasaidia katika kukabiliana na hali ni kwamba uhamishe sasa masuala ambayo yanahusu huo mlolongo wa ardhi yahamie katika Mahakama za Mwanzo, kitu ambacho sasa kule kwenye Mahakama za Mwanzo nako kule kumeshonana na kuna mambo mengi sana ambayo yanatokea kule.

Mimi naamini kwamba hili ni jambo ambalo tunaweza tukajadiliana siwezi mimi sasa hapa nikafanya rolling nikasema basi hamishieni pelekeni kwenye Mahakama za Mwanzo. Ni jambo ambalo linasaidia katika kufikiri namna nzuri ya kutatua hili tatizo kwa sababu kweli kama wanavyosema Wabunge kuna tatizo hilo la kwamba tuna ufinyu wa Bajeti na kwa hiyo kupeleka mpaka kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya inakuwa ni taabu na ni mbali.

Mimi nafikiri ni jambo ambalo tunaweza tukajadiliana wote kwa pamoja lakini nasita kusema kwamba tulipeleke kwenye Mahakama za Mwanzo kwa sababu kule nako kuna kesi nyingi sana ambazo zimejazana kule.

Na. 69

**Kutengeneza Barabara ya Majengo – Senga**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara ya Majengo – Senga iliyopo katika Wilaya ya Sumbawanga ambayo inaweza kuiongezea Serikali mapato kutokana na usafirishajiwa mazao ya Mahindi, Vitunguu Saumu na Ngano?

(b)Je, Serikali haioni kama haiwatendei haki wananchi wa Senga walioko katika Wilaya ya Sumbawanga kwa kutowatengenezea barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Rishard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Barabara anayoizungumzia Mheshimiwa Mbunge inaitwa Mpanda – *SIDO* – Senga – Wipanga. Barabara hii ina urefu wa Km. 13.1 na inahudumiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Aidha, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba sehemu inapopita Barabara hii ni muhimu kwa kuongeza kipato kwa Serikali kwa maana ya Manispaa ya Sumbawanga kwa sababu ya aina ya mazao yanayolimwa katika eneo hilo.

Hata hivyo, Barabara hii inapita kwenye eneo lenye milima na matengenezo yake yanahiaji kiasi kikubwa cha fedha. Serikali kwa kutambua umuhimu wa Barabara hii huifanyia matengenzo ya mara kwa mara ili iweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali kupitia Mfuko wa Barabara na *Program* ya Barabara za Serikali za Mitaa (*Local Government Transport Program (SGTP)* ilitenga kiasi cha shilingi 33,139,945/= na kuifanyia matengenzo ya sehemu korofi (*Spot Maintenance*) Barabara hii.

Katika Mwaka wa Fedha 2008/2009, mchakato wa kumpata Mkandarasi umekamilika baada ya *MAP Civil and Building Construction Compa*ny wa Sumbawanga kushinda zabuni. Mradi huo utatekelezwa kwa gharama ya shilingi milioni 48,751,700/-. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na matengenzo ya muda maalum (*Periodic Maintenance*) kutoka *Mpanda Road (SIDO* hadi *Mafulala Road*, (kilomita 2.0).

Pia matengngnezo katika maeneo korofi (*Spot Improvement*) kutoka *SIDO* hadi *Wipanga Road*, (kilomita 4.0). Kilomita 7.1 hazipo katika mwaka huu wa fedha, yaani 2008/2009. Mkandarasi anategemea kuanza utekelezaji wa mradi huo tarehe 16 Februari, 2009 na mradi utakamilika ndani ya kipindi cha miezi minne (wiki 16) kwa mujibu wa Mkataba huo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatenda haki kwa wananchi wake wote, hii ikiwa ni pamoja na wananchi wa Manispaa ya Sumbwanga na maeneo mengine ya Mkoa. Barabara nyingi za Halmashauri nchini ziko kwenye hali mbaya na zinahitaji kufanyiwa matengenezo makubwa yanayogharimu fedha nyingi.

Kutokana na ufinyu wa Bajeti inayoikabili Serikali kwa ujumla wa matengenezo makubwa ya Barabara hizi yanafanywa kwa awamu, kulingana na uwezo wa Serikali kwa wakati husika.

Mwisho, napenda kumpongeza Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, kwa jinsi anavyofuatilia masuala muhimu ya Mkoa wa Rukwa hususan  Maendeleo ya Miundombinu ya Barabara.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo hayajaridhisha sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri zetu katika matengenezo ya Barabara zinapewa fedha kidogo mno, na kwa kuwa ukizingatia Halmashauri zetu ndizo ambazo zinafungua vijiji vingi katika maeneo yetu na maeneo ya huko vijijini kwetu. Na kwa kuwa, ukiangalia Barabara nyingi za vijijini hazina matengenezo kabisa ya kiwango kizuri kutokana pesa kidogo. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuzipangia Halmashauri zetu pesa za kutengeneza Barabara kwa kiwango kizuri?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Kutokana na hali ya Barabara zinavyotengenezwa hakuna mifereji kabisa na ukizingatia kipindi hiki cha masika hata Barabara zikitengenezwa maji yanakwenda kukata barabara kutokana na kwamba hakuna mifereji.

Je, Serikali inaweka fedha za kutengeza mifereji kwa kiasi gani na kwa kiasi gani wanaona umuhimu wa kutengeza mifereji ?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anna R. Lupembe Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwamba anasema majibu ni mazuri lakini amesema kwamba hayaridhishi, lakini majibu ndiyo hayo sina majibu mengine. Haya majibu ninayotoa hapa siyo ya kwangu ni ya Serikali, lakini nimshukuru.

Mimi nasema kwamba kimoja ambacho nakiona hapa ni kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Anna R. Lupembe, mimi mwenyewe nilitakiwa kuondoka hapa kwenda Sumbawanga na nimekwenda mpaka Sumbawanga nimetembelea Mkoa wote wa Rukwa. *(Makofi)*

Nataka nithibitishe kwamba maneno anayoyaeleza hapa Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba barabara za Sumbawanga pamoja na umuhimu wake katika uchumi. Sumbawanga inashiriki sana katika kulisha nchi kwa maana ya kilimo cha mahindi, mambo ya utalii na kadhalika. Kwa hiyo, siwezi kupinga hapa kwa sababu nimeona kwa macho yangu kwamba hali iliyopo kule si nzuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu amekwenda kule na yeye ameona hivyo hivyo, ameona na anajua kwamba hali si nzuri kule.

Sasa kiasi kinachozungumzwa hapa ni kiasi cha pesa ambacho kinaonekana kwamba kinatengwa kidogo.

Mheshimiwa Spika, hela zinazotumika hapa kwa ajili ya barabara ni wewe unayetuuliza hapa kwamba kifungu hicho kimepitishwa na sisi tunasema ndiyo! Kwa hiyo, mpaka iletwe tena na wewe utuulize kwamba kifungu hicho kimepitishwa, tuseme ndiyo ! ndivyo inavyokuwa. Kwa hiyo, kama kuna upungufu ni kuja hapa tuseme Bajeti hiyo imepitishwa …... (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili ni jambo letu sisi wote na tutalifanyia kazi.

Lakini ame – *pause* swali namba mbili, hili swali linazungumzia habari ya mifereji. Ile *package* inayotolewa pale unapopeleka mafungu pale kwa ajili ya barabara ndani yake unaweka pia na zile njia za kutolea maji. Njia za kutolea maji ndiyo roho ya barabara kwa sababu usipotoa maji haya na kwa sababu barabara zetu nyingi ni udongo na za kuwekwa Moramu zitakufa hata kama ni ya lami kama hukuweka mkondo wa kutolea maji itakufa ile barabara.

Tunachosema kwa vile Bajeti ni kidogo kwenye upande huu wa njia za kutolea maji tunawashauri Halmashauri wawahamasishe wananchi wafanye kazi hiyo ili barabara itakayotengenezwa pale kama ni kilomita 10 walau sita ziweze kutengenezwa vinginevyo tukienda kama anavyosema maana yake ni kwamba tutakwenda kuweka mkondo wa kutolea maji na barabara itakayopitika ni kidogo kwa sababu pesa ile itakwenda katika lile eneo.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge aende akahamasishe wananchi wake sisi tunasema kwamba kabajeti tunaweka hizo katika Bajeti yetu.

Na. 70

**Kufeli kwa Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, asilimia 53 ya wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waliofanya mitihani ya mwaka 2007/2008 wamefeli mitihani yao:-

(a) Je, ni sababu gani iliyopelekea wanachuo hao wafeli kwa kiwango kikubwa hivyo?

(b) Je, ni wanachuo wangapi ambao wamefeli kwa kiwango cha kutopata nafasi ya kurudia mitihani?

(c) Je, Serikali inashauri nini katika hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA MUGOSI KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Mariam Reubeni Kasembe (Viti Maalum) lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

(a) Vyuo vimeanzisha mfumo wa ufundishaji (*modular system*) katika mfumo huo, somo moja kwa mfano, Kemia hugawanywa na kufundishwa kama kozi kadhaa zinazojitegemea. Kozi hizo hutahiniwa kila moja peke yake na mwanafunzi anatakiwa afaulu angalau kwa kiwango cha alama C kila moja ya kozi hizo tofauti na walivyokuwa wakisoma na kufanya mitihani kwa somo moja tu.

Kimsingi wanafunzi wanatakiwa wasome kwa bidii sana ili wawe mahili katika kila kozi inayofundishwa na hivyo kufaulu kwa viwango vinavyotakiwa. Mfumo huu hivi sasa unatumika hapa nchini na duniani kote. Mfumo huu hivi sasa unatumika hapa nchini na katika vyuo vingi hapa duniani.

(b) Mheshimiwa Spika, Wanafunzi waliofeli kwa kiwango cha kutopata fursa ya kurudia mtihani ni 0.9% (kiasi hiki kimeshuka kutoka 2.5% kwa mwaka 2006/2007). Zifuatazo ni taarifa rasmi za matokeo zilizotolewa Januari, 2009.

·Waliofaulu moja kwa moja 53.6%.

·Walitakiwa kufanya mitihani ya marudio katika kozi kadhaa walizofeli 36.1%.

·Waliozuiliwa matokeo ya mitihani kutokana na kudaiwa ada mbalimbali 0.4%.

·Waliahirisha baadhi ya mitihani au masono yote 4.5%.

·Walioacha masomo (*absosconded studies*) 0.9%.

·Wanaorudia somo katika mwaka wa masomo unafuata 1.7%.

·Wanafunzi waliofeli moja kwa moja ambao hawataruhusiwa kurudia mtihani ni 0.9%.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa ushauri wa kuwataka wanafunzi wasome kwa bidii na wazingatie taaluma zao na Vyuo Vikuu viweke msisitizo kwa wanafunzi kuzingatia masomo.

Aidha, wanafunzi wawatumie kikamilifu washauri wa masomo (*Academic Advisors*) na wakati huo huo washauri wa masomo nao wanahimizwa kutenga muda wa kuwasaidia wanafunzi kitaaluma.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa, wananchi wengi wamekuwa wakizungumzia migomo inayofanywa vyuoni kama ni chanzo kimojawapo cha wanafunzi kukosa masomo hivyo kutofanya vizuri kwenye mitihani yao. Je, Serikali inasema nini kuhusu hilo?

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuangalia matatizo yanayowakuta wanafunzi katika vyuo hivi vikuu ili kuondoa kero zao kwa haraka ili watoto wetu waweze kupata kusoma kwa muda wote ule ambao unatakiwa na hatimaye kufanya vizuri katika mitihani yao mwisho?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA MUGOSI KABAKA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, kama ifuatavyo:

Inawezekana kama wanavyohisi wengi kwamba migomo inaweza ikaathiri kwa kiasi fulani lakini kwa mfano mgomo uliosababisha vyuo kufungwa muda mfupi uliopita hautaathiri masomo wala hautaathiri *semister* ya hawa wanafunzi.

Lakini ni kweli kwamba tunawaomba wanafunzi na wananchi mtusaidie, wanafunzi waache kutumia migomo kama suluhisho la kero ambazo wanafikiri kwamba zinawapata katika vyuo. Kuna njia nyingi za kutatua matatizo yao ukianzia pale katika vyuo lakini pia hapa kwetu Wizarani tunawasikiliza wanafunzi katika matatizo ambayo yanawapata.

Wizara yangu imeanza kushughulikia matatizo yanayohusu Bodi ya Mikopo ikiwa ni pamoja na kuunda Kamati ambayo inaangalia kwa undani taratibu nzima ya kazi inayofanywa na Bodi ya Mikopo ili kuweza kurekebisha baadhi ya vigezo ambavyo tunafikiri ndiyo vinaleta matatizo katika utoaji wa mikopo na mambo mengine ambayo tunafanya ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaendelea na masomo bila kukatishwa na migomo ambayo siyo ya lazima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu wiki iliyopita wakati akijibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, alionyesha kwamba ukiachilia wale wanafunzi ambao hawakujisajili upya chuoni kama walivyotakiwa, wanafunzi wengine wote licha ya upungufu wao ambao unaendana pamoja na kuomba rufaa kwa Mheshimiwa Waziri watakuwa na *access* ya chuo pamoja na *library*. *(Makofi)*

Lakini taarifa ambazo zipo sasa hivi ni kwamba wanafunzi ambao wamekata rufaa kwa kutokuwa na uwezo wa kujilipia shule wananyimwa kuingia *Library* wakati mitihani inakaribia na *test* zinaendelea.

Sasa nataka Mheshimiwa Naibu Waziri anisaidie. Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na watu wanaowanyima fursa wanafunzi hawa ambao ni watoto wa maskini?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushsukuru sana kwa kunipa fursa ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima J. Mdee.

Mheshimiwa Spika, ingekuwa rahisi zaidi kama swali hili lingeletwa lenyewe kwa utaratibu wa kawaida kwa sababu swali la msingi hapa ni mitihani ya wanafunzi. Lakini hata hivyo, nilikuwa napenda kujibu swali lake kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwamba karibu wanafunzo wote waliotegemewa kurudi chuo kikuu ambao waliomba wamerudi kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Wanafunzi wale ambao waliomba rufaa kama Sheria inavyohitaji mwisho wa kuomba rufaa zao ilikuwa ni tarehe 30 Januari, 2009 na rufaa hizo sasa zinafanyiwa kazi na katika kipindi kifupi uamuzi utatolewa.

Baada ya maamuzi hayo ni matumaini yangu kwamba wanafunzi walio wengi walioomba rufaa hizo watarudi chuoni kama kawaida. *(Makofi)*

Na. 71

**Nafasi za Masomo Nje ya Nchi Kuzingatia Pande za Muungano**

**MHE. MOHAMMED A. CHOMBON** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika jibu la msingi la Namba 445 katika Mkutano wa Kumi na Mbili Kikao cha Hamsini, Serikali ilijibu kuwa haitoi nafasi ya kwenda kusoma nje kwa kuzingatia sehemu mbili za Muungano ila ni kwa vigezo na sifa zinazohitajika:-

Je, Serikali haioni kuwa ni bora kubadilisha utaratibu huo ili kutoa nafasi kwa mpango utakaokubalika na pande zote mbili kutoa wanafunzi wenye sifa zinazotakiwa kama Wizara nyingine za Muungano zinavyotoa nafasi za ajira?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA MUGOSI KABAKA )** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mohammed Chombon, Mbunge wa Magomeni, naomba nitoe maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimkumbushe Mheshimiwa kuwa katika jibu langu namba 445 aya ya mwisho nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa uteuzi wa waombaji wa nafasi za masomo ya Elimu ya Juu Nje ya Nchi, hufanywa na Kamati Teule ya Elimu ya Juu ya Muungano (*Sub Advisory Committee on Higher Education and Training*) ambapo huzingatia zaidi sifa za Kitaaluma, umri na uraia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kujali mwombaji anatokea sehemu gani ya Muungano.

Kamati hii ina Wajumbe kutoka Tanzania Bara na Tanzania Visiwani (Zanzibar).

Mheshimiwa Spika, naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kuwa ni ukweli usiopingika kwamba kuna waombaji wengi wenye asili ya Zanzibar wanaoishi Tanzania Bara na huomba na kupata nafasi na udhamini wa masomo ya nje ya nchi zinazotangazwa na Wizara yangu.

Kwa upande mwingine wapo waombji wenye asili ya Tanzania Bara ambao wanaishi Zanzibar nao huomba na kupata nafasi hizo.

Pia wapo waombaji wa Zanzibar wanaoishi kule wanaoomba na kufanikiwa kupata hizi nafasi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haa mafupi naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mohammed Chombon Mbunge wa Magomeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuimarika kwa Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar na mwingiliano mkubwa uliopo kwa watu wenye asili ya Zanzibar na Tanzania Bara, Wizara yangu haioni kuwa ni busara kubadilisha utaratibu wa sasa wa kuchagua waombaji kwa kuzingatia sifa zao za kitaaluma.

Badala yake, Wizara yangu itaendelea kuimarisha utaratibu huu kwa kuchagua waombaji wenye sifa nzuri za kitaaluma ili wnafunzi wetu wawe Mabalozi wazuri kwa nchi wanazokwenda kusoma na wanaporudi wawe ni watu wenye taaluma inayokubalika kimataifa.

Aidha, hawa wanafunzi walichaguliwa na Kamati Teule ya Muungano siyo mwisho, kwani hushindanishwa na wanafunzi wengine wa nchi nyingine kabla ya kupatiwa nafasi katika vyuo vya nje.

Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa tukichagua wanafunzi ambao hawatimizi vigezo vilivyowekewa, Tanzania itkuwa inapoteza nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwaomba Wabunge kokote wanakotoka kuwahimiza vijana wtu wasome kwa bidii ili wawe na sifa nzuri za kujiunga na vyuo vya Elimu ya Juu hapa nchini na nje ya nchi.

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Baada ya majibu ya Mheshimiwa

Naibu Waziri nilikuwa nataka kumwuliza anaweza kunipatia orodha ya wanafunzi waliotoka kwenye Vyuo au kwenye *High Schools* za Zanzibar waliopata nafasi kwenda katika Vyuo vya nchi za nje?

**SPIKA:** Nadhani huo ni wajibu wake atakupatia tu. Kwa hiyo, tunaendelea ni zamu sasa ya Wizara ya Fedha na Uchumi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, wa Viti Maalum Mwanza.

Na. 72

**Ushuru wa VAT kwenye Vitabu**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ushuru wa *VAT* huwekwa katika manunuzi ya vitabu vitumikavyo katika shule zetu hapa nchini:-

Je, Serikali haioni kuwa, hali hiyo ndiyo chanzo kikubwa cha wanafunzi kushindwa kununua vitabu na hivyo kuchangia kushuka kwa elimu hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* Sura 148 inasimamia ukadiriaji na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi ya ongezeko la thamani.

Kwa mujibu wa Sheria hii, bidhaa na huduma zinazouzwa nchini na kustahili kutozwa kodi ya *VAT* hutozwa kiwango cha asilimia ishirini (20%) isipokuwa bidhaa na huduma zilizoorodheshwa kwenye Jedwali la kwanza ambalo bidhaa na huduma zinazotozwa *VAT* kwa kiwango cha asilimia sufuri (0%) na la pili ambazo bidhaa na huduma zilizosamehewa *VAT* kwa mujibu wa Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu na mchango wa Elimu kwa maendeleo ya Taifa, Sheria ya *VAT* chini ya kifungu cha 10, kipengele namba 4 na 6 kwenye Jedwali la pili, vinatoa msamaha wa kutozwa *VAT* kwenye huduma zote za elimu kwa Taasisi iliyosajiliwa na Serikali pamoja na manunuzi ya vitabu, majarida, ramani au vielelezo vyote vinavyotumika katika shule zetu hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika jibu la Naibu Waziri ametoa maelezo katika makundi mawili kwamba wapo wanaotozwa asilimia 20 ya *VAT* na wapo ambao hawatozwi.

Lakini naomba labda nipate maelezo tunapotembelea kwenye viwanda vya uzalishaji wa vitabu hivi lalamiko lao kubwa ni *VAT*, na kama ni Taasisi itauza kwa asilimia sufuri na kiwanda kimetoza *VAT* wanatarajia nini?

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo kwa nini kama ni suala nzima linagusa elimu lisiwe na asilimia sufuri moja kwa moja kutoka kiwandani mpaka kwenye Taasisi ili watoto wetu waweze kununua vitabu kwa wingi iwezekanavyo kulingana na upungufu wa vitabu katika shule zetu za sekondari?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kama Serikali ikiamua kufanya kama Mheshimiwa Mbunge anavyoshauri basi hatutatoza kodi na hilo kwa kweli haliwezekani.

Lakini la pili, ni kwamba katika mahitaji ya shule si tu vitabu vinavyohitajika. Kwa hiyo, ni lazima Serikali iwe na vyanzo vingine vya mapato vya kutoza kodi ili yale mengine ambayo yanahitajika kwenye shule zetu yawezekane kupangiwa fedha za matumizi.

Kwa hiyo, kinachofanyika ni kusamehe kodi pale ambapo manunuzi yana uhusiano moja kwa moja na wanafunzi yanapofanyika na ni Taasisi zile ambazo zinauza vile vifaa ambavyo vitatumika mashuleni ambavyo kama nilivyosema ni pamoja na vitabu, ni pamoja na majarida, ni pamoja na kompyuta na vifaa vya jiografia na kadhalika.

Na. 73

**Fidia kwa Halmashauri ya Shinyanga Vijijini**

**MHE. AHMED A. SALUM** aliuliza:-

Kwa kuwa, tarehe 31/6/2005 Serikali ilifuta madeni ya fedha za Serikali na mali na kuahidi kulipa fidia kwa Halmashauri husika; na kwa kuwa, msamaha huo uliathiri pato la Halmashauri ya Shinyanga Vijijini ambayo ilikuwa ikiidai SHIREKU jumla ya shilingi 111,475,951.25 kutokana na ushuru wa pamba na kulikosesha Halmashauri fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali:-

(a) Je, kwa nini Serikali imechelewa kujibu?

(b) Je, ni lini fidia hiyo italipwa kwa Halmashauri ya Shinyanga Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia kikao chache cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika Dodoma tarehe 12 Agosti, 2005, ilikubali kuanza kutekeleza programu ya Mageuzi na Uendeshaji wa Kisasa wa Ushirika nchini.

Kwa vile mageuzi yanayokusudiwa yanategemea kuwepo kwa vyama vya ushirika ambavyo vitajitegemea kibiashara na ambavyo vinaweza kuhimili nguvu za ushindani, kikao cha Baraza la Mawaziri kilimshauri Mheshimiwa Rais akubali Serikali kufuta, kuchukua au kulipa baadhi ya madeni ya Vyama vya Ushirika katika kipindi cha kuanzia mwaka 1992, mpaka mwaka wa 2004.

Lengo la uamuzi huo lilikuwa ni kuviwezesha Vyama husika kufanya maboresho katika muundo na utendaji kwa dhamira ya kujiimarisha kibiashara. Mheshimiwa Rais alikubali ushauri huo na kuagiza kwamba programu hiyo itekelezwe ipasavyo ili kurejesha Ushirika katika msingi sahihi.

Serikali ilileta Bungeni hoja ya kufuta madeni ya jumla ya shilingi bilioni 16.2 yaliyokuwa yanadaiwa na Serikali na Taasisi zake kwenye baadhi ya Vyama vya Ushirika. Katika madeni hayo Chama Kikuu cha Ushirika cha Shinyanga *(SHIRECU)* kilikuwa kinadaiwa jumla ya shilingi bilioni2,665,944,260/= likiwemo deni la shilingi milioni 111,475,951.25 la Halmashauri ya Shinyanga Vijijini, lililotokana na ushuru wa pamba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri za Wilaya, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, zinapata ruzuku toka Serikali Kuu, Serikali haioni sababu na mantiki ya kufidia deni hilo.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba na kumshauri Mheshimiwa Mbunge kuungana na watendaji wa Wilaya yake ili waweze kujenga hoja ya kupatiwa fedha za kutosha za ruzuku katika Bajeti ijayo, 2009/2010, kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa fedha hizi ni muhimu mno na Serikali inajua kabisa kuwa Halmashauri hazina mapato mazuri kama Halmashauri yetu ya Shinyanga; na kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema tukajipange upya kwa namna ya kuomba tena.

Je, tukiomba kwa mara ya pili ni lini hasa Serikali itupe uhakika kwamba itatulipa hizo fedha vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza tuelewane kwamba dhamira ya Serikali hapa ilikuwa kuimarisha Vyama vya Ushirika,

na katika dhamira hiyo Serikali ilifuta madeni na ilichukua madeni Serikali Kuu ya shilingi bilioni 2,665,944,260 ambazo zilikuwa za *SHIRECU* ambacho ni Chama cha Ushirika kilichopo Shinyanga Vijijini ambapo Halmashauri ya Shinyanga Vijijini ina jukumu la kutunza.

Kwa hiyo, mimi ningefikiri kwamba shilingi milioni 111,475,951 ambazo Halmashauri ilikuwa inaidai *SHIRECU* kama ushuru wa pamba. Halmashauri yenyewe ingechukulia kama namna ya kuunga mkono Serikali Kuu katika azma yake ya kuimarisha Chama cha Ushirika yaani *SHIRECU.*

Lakini la pili, ni kwamba hata hivyo mwaka huu 2008/2009 hizi fedha hazipo kwenye Bajeti, na mwaka 2009/2010 kama nilivyomshauri watakapoweka kwenye makisio ya Bajeti ya Halmashauri hiyo kwanza itategemeana na vipaumbele vya Halmashauri na katika *ceiling* ambazo watakuwa wamepewa, na kama fedha hizo zitakuwa miongoni mwa maombi kwenye Bajeti ya Wilaya na kama sasa itakubalika, basi fedha hizo zitakuja Wilayani, lakini siyo kama hili deni ama ulipaji wa deni lenyewe.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hayatoshelezi kabisa kwa sababu wananchi au Wilaya hizi ambazo zinaidai *SHIRECU*, Serikali ilijitolea ikayabeba hayo madeni na ikaahidi kwamba itazilipa Wilaya hizo; na kwa kuwa fedha anazosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba zinalipwa kwenye Halmashauri kama ruzuku, Serikali inalipa fidia ya vyanzo vya mapato ya kodi zilizofutwa.

Lakini suala la fedha za *honour sources* ambazo zinakusanywa na Halmashauri ni jambo lingine. Sasa Naibu Waziri haoni kwamba Halmashauri zinazodai fedha hizo kusema kwamba hizo zinaingizwa katika ruzuku ya Serikali ni kuzihujumu Halmashauri hizo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba tuelewane kwamba Halmashauri ni sehemu ya TAMISEMI, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. TAMISEMI ni sehemu ya Serikali Kuu. Serikali Kuu ndiyo inayoziwezesha Halmashauri zetu zote kwa njia ya ruzuku. Mimi ninashangaa kwamba Halmashauri itang'ang'ania ilipwe na Serikali Kuu deni wakati watakuja kutuomba tena fedha. Maana yake tunachoweza kufanya ingawaje hatufanyi hivyo ni kusema sawa tutawalipa ili mradi hizo fedha zimekwishapangiwa matumizi. Halafu tutakapokuja kwenye bajeti kuu tutaziondoa kwenye kasma yako hiyo haileti mantiki yoyote.

Lakini la pili, ni kwamba Serikali Kuu haipeleki fedha kwenye Halmashauri kwa sababu yoyote ile ambazo bado hazijapangiwa matumizi. Kwa sababu pamoja na wao kuridhika kwamba kutokana na vipaumbele vyao watatumia fedha watakazopata za ruzuku, lakini ni lazima Serikali Kuu na sisi tujihakikishie na turidhike kwamba matumizi yanayokusudiwa na Halmashauri hizi ni sahihi na yapo kwenye vipaumbele vyao ambavyo na vyenyewe ni sehemu ya vipaumbele vya Serikali Kuu.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya Wizara ya Maliasili na Utalii, swali linaulizwa na Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Viti Maalum.

Na. 74

**Faida Zitokanazo na Mti wa Mbuyu**

**MHE. MARGARET A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa mbuyu ni mti ambao una matumizi mengi muhimu kwa binadamu, na nchi kama Ghana huuza bidhaa za mbuyu nchi za nje:-

(a) Je, Serikali inafahamu faida hizo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza Mbuyu kitaalamu ili mazao yake yauzwe nje ya nchi na kuongeza pato la Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margreth Agnes Mkanga, ingawa amesema Na. 74 ni 73 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:- Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mti wa mbuyu kitaalamu unaitwa Adansonia digitata na ziko aina saba za jamii ya mti huu, kati ya hizo sita zinapatikana kwa wingi nchini Madagascar. Mbuyu unapatikana pia katika nchi zote zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara hasa maeneo makavu ya nyanda za chini yenye mvua zisizozidi milimita 300 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua faida zitokanazo na mbuyu ikiwa ni pamoja na kivuli, kuzuia mmomonyoko wa udongo, kuongeza unyevunyevu na mbolea kwenye udongo, kuhifadhi *bioanuai* kwa wanyama hasa ndege na nyuki ambao hutumia matundu ya mbuyu kwa kutengeneza viota vya kuishi. Kwa binadamu, mbuyu hutumika kama chakula chenye vitamini B aina ya *Carotene*, vitamini A ambayo husaidia macho kuona na vitamini C ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa fizi na meno, mifupa, ngozi na misuli.

Mbegu ya mbuyu hutoa mafuta ambayo hutumika kwa kupikia, kujipaka na hulainisha ngozi na kuzifanya kucha kumeremeta na kuwa mgumu. Tafiti zinaonyesha kuwa mbuyu hutumika kama dawa ya kutibu magonjwa kama ya Kansa, surua, ndui, ngozi, meno, fizi, kuhara na magonjwa ya moyo.

Unga wa majani na matunda ya mbuyu hutumika kama kiungo na kuongeza ladha ya chakula. Mbuyu pia hutoa nyuzinyuzi ambao hutumiwa viwandani kutengeneza

kamba. Mti wa mbuyu pia hutumika kutengeneza karatasi na boti za kuvulia samaki. Hapa nchini, matunda ya ubuyu yanatumika kutengeneza juisi katika maeneo ya Singida, Shinyanga na Dodoma. Pia katika maeneo haya matunda ya ubuyu ni zao la kibiashara na huuzwa sokoni.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahimiza utunzaji wa mti huu kutokana na umuhimu wake kiuhifadhi na kimazingira. Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania wanafanya majaribio ya kuotesha mbegu za mti huu Wilayani Mwanga (Kilimanjaro) ili kuona kama zinaweza kuzalishwa katika mashamba ya kilimo.

Kutoshamiri kwa biashara ya zao la mbuyu ni changamoto kwa Wizara yangu na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Na ni jukumu letu sasa kulitangaza zao hili ili litumike kama zao la biashara hapa nchini. (*Makofi*)

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa vile mbuyu kumbe tumeelimika leo kwamba una matumizi mengi sana na faidia kubwa. Je, Serikali sasa ina mpango gani mahususi wa kuendeleza zao hili kwa kilimo katika maeneo ambayo yametajwa kwamba tayari mbuyu unastawi kuliko kuanza na utafiti kabla ya kupata faida kubwa kwa maeneo ambayo mbuyu huu sasa hivi upo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema ni kweli mbuyu una faida nyingi lakini matumzi yake hapa nchini hayajawa makubwa sana. Kwenye nchi za wenzetu hasa nchi za Magharibi kama Senegal na Ghana zao hili limekuwa ni zao kubwa la kibiashara na huingiza fedha nyingi za kigeni. *(Makofi)*

Sasa mimi nafikiri cha muhimu cha kuanzia ni kuhamasisha matumizi ya zao hili. Tumesema ukitumia mbuyu au matunda ya ubuyu yanaimarisha meno na vitu vingine kama nilivyoeleza. Tukihamasisha Watanzania watumie mazao ya misitu badala ya kutumia madawa ya viwandani ambayo mengi yana madhara kwa afya zao, naamini kwamba itakuwa ni mwanzo mzuri. Wizara ya Kilimo na Ushirika tutafanya nayo kazi kwa pamoja kuona ni namna gani tuta-*responce* kwenye *demand* kubwa itakayokuwa imejitokeza kutokana na wananchi kuelewa umuhimu wa mtu huu. (*Makofi*)

**MHE. HAROUD S. MASOUD:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Bunge hili hili Mheshimiwa Waziri Dr. Hussein alipokuwa yuko Wizara ya Afya miongoni mwa maradhi ambayo yalikuwa yanatibiwa na mti wa mbuyu yalikuwa ni kuongeza nguvu za kiume. Je, mbona Naibu Waziri hajatuambia sisi kwa sababu tangu siku ile mibuyu iko katika harakati za kukatwa, kuchimbwa ili watu wapate nguvu za kiume? (*Makofi*)

**SPIKA:** Unahitaji kujibu sijui maana yake? Haya Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la mzee wangu, jirani yangu Mheshimiwa Haroub Masoud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, faida za mbuyu kama nilivyosema hizi nilizoziainisha ni chache. Ziko faida nyingi za kitiba. Kwa wenzetu wa upande wa Wizara ya Afya au wanaoshughulika na mambo ya kimatibabu hakika wanaweza wakaainisha matumizi mengine haya niliyoyataja. Kwa hiyo, kutaja haya niliyosema haimaanishi kwamba mbuyu faida zake zinaishia hapo. Una faida nyingi zaidi ya hapo. Kwa hiyo, inawezekana pia hata tatizo la nguvu za kiume mbuyu kuweza kuwa unasaidia. Kwa hiyo, sijakanusha kwamba hausaidii. Nilichoeleza ni baadhi ya faida zake.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ametupa faida nyingi sana za zao la mbuyu na zao la mbuyu kwa bahati nzuri lipo maeneo mengi hapa Tanzania ikiwepo Dodoma. Lakini wananchi wa Dodoma ni maskini sana, Singida, Tabora na Mikoa mingine mingi. Pia zao hili miti yake ipo porini haina kazi yoyote. Majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri yamekuwa mepesi sana kwamba watatoa tu ushauri jinsi ya kutumia au watahamasisha wananchi?

Je, Serikali sasa iko tayari kuja na mpango kabambe wa kuwezesha matumizi ya zao hili pamoja ikiwa ni pamoja na kulitangaza ili kuweza kuinua kipato cha Watanzania na kuondoa umaskini kwa Watanzania? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nilichosema ni kwamba matumizi ya mti huu hapa nchini si makubwa sana. Nikasema pia kwamba tutafanya kazi na wenzetu wa Wizara ya Kilimo na pia Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuweza kulitumia zao hili kibiashara. Sisi Wizara yetu Maliasili na Utalii hasa tunahusika katika utunzaji na uhifadhi wa mti huu. Lakini kuutumia mti huu katika maazingira ya kibiashara zaidi tutafanyakazi na wenzetu wa Wizara nilizotaja ambazo hakika nafikiri tukifanyakazi hiyo kwa pamoja kama ulivyoshauri tutaweza kufanikiwa. Kwa hiyo, nikubaliane na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwamba tutashirikiana na Wizara hizo ili tuweze kuendeleza matumizi ya mti huu. (*Makofi*)

Na. 75

**Kuboresha Maeneo ya Utalii Nchini**

**MHE. PROF. RAPHAEL R. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mikakati kabambe ya kuboresha maeneo mbalimbali ya kiutalii nchini:-

(a)Je, ni maeneo yapi yameainishwa kwa utalii katika mwambao wa Nyasa hususan katika Wilaya ya Ludewa?

(b)Je, ni mikakati gani imeandaliwa katika kuanza na kuboresha utalii katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu iliandaa Mpango Kabambe wa Uendelezaji Utalii (*Integrated Tourism Master Plan*) mwaka 1996 na kuupitia upya mwaka 2002. Mpango huu wa miaka 10 umegawa nchi katika kanda za uendelezaji .

Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, (*Southern Highlands Zone*) ilianishwa kama eneo muhimu la kuendelezwa ili kufungua na kuendeleza Utaii katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza mpango huu, Wizara yangu iliainisha vivutio vya Utalii Mkoani Iringa mwaka 2000 na kufanya semina ya uhamasishaji wa wadau mwaka 2001. Kufuatia matukio hayo, uongozi wa Mkoa na Halmashauri zake kwa kushirikiana na wadau wamejizatiti na kuhakikisha Sekta ya Utalii inakua kwa kasi kubwa.

Kwa kuzingatia mwamko huu, Wizara yangu imerudia zoezi la uainishaji vivutio vya utalii katika Wilaya zote ikiwemo Wilaya ya Ludewa Desemba, 2008. Vivutio vilivyoainishwa katika Wilaya ya Ludewa ni pamoja na:-

Mandhari nzuri ya kuvutia ya safu za Milima ya *Livingstone*, fukwe safi kwenye Ziwa Nyasa, maji mangavu ya Ziwa Nyasa yanayoruhusu kuona viumbe ndani ya maji, Mto wa Mchuchuma, Misitu ya Hifadhi ya Sakaranyumo eneo la Milo, Msitu wa Mshora, Msitu wa Madenge kwenye Milima ya *Livingstone,* yenye wanyama adimu kama mbega mweuzi na mweupe, ndege wa aina mbalimbali eneo la Manda ambako kuna fukwe nzuri na safi, makaburi ya Wajerumani na maeneo mengine mbalimbali ya kihistoria. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 Wizara yangu kwa ushirikiano na Shirika la Utalii Duniani (*World Tourism Organisation)* ilianisha miradi ya *Manda Community Tourism Development* na kuuombea ufadhili chini ya utaratibu wa *Step Initiative* (*Sustainable Tourism for Eliminating Poverty*) lakini bado hajapatikana mfadhili.

Wizara inaendelea kufuatilia suala hili. Taarifa ya vivutio na fursa zilizoko Mkoani Iringa ikiwemo Wilaya ya Ludewa zilizobainishwa Desemba, 2008 zitawekwa kwenye *CD* ili ziweze kutumika kutangaza na kuvutia watalii na wawekezaji.

Napenda kuchukua furasa hii kuhimiza Halmashauri za Wilaya kuiweka sekta ya utalii katika vipaumbele vya mipango yao na Wizara iko tayari kuendelea kutoa ushirikiano.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kuwa kuna maeneo kama alivyosema mengi ya kihistoria yenye kumbukumbu za vita kuu ya kwanza na ya pili, majimaji na mapambano na shughuli mbalimbali za Wajerumani na Waingereza ikiwa pamoja na mapango makubwa yaliyo chini ya ardhi yaliyowekwa na Wajerumani kujikinga na Waingereza.

Je, Wizara itatusaidia vipi Wilaya inataka iandike itoe vidokezo au *documentantion* ya maeneo haya kwa kujiandaa kwa ajili ya utalii. Wizara itatatusaidia vipi kuhakikisha hili linafanyika?

Lakini la pili, kwa kuwa wenzetu wa *Wildlife Conservation Society* wamekuwa wakiainisha rasilimali za kitalii kwenye milima Livingstone na hizo fukwe za Ziwa Nyasa na ripoti inakaribia kukamilika. Waziri anaweza akaja sasa Ludewa ili na yeye ajionee maeneo hayo aliyoyataja kwa macho yake ili tufanye maandalizi mazuri ya utalii katika Wilaya ya Ludewa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijajibu maswali yake nipende kumshukuru sana Prof. Raphael Mwalyosi na ni nikiri kwamba ni miongoni mwa Wabunge ambao tunafanya nao kazi kwa karibu sana. Pamoja kwamba ameuliza swali, lakini naamini ameuliza swali kwa ajili tu ya kufanya Watanzania waelewe kwamba kwa sasa tunafanya naye kazi kwa pamoja katika kutengeneza hiyo *documentation* na nimhakikishie kwamba sisi Wizara kupitia *TTB* tutashirikiana naye kukamilisha uandaaji wa hiyo *CD* pamoja na *documentation* zingine pamoja na utangazaji wa eneo hilo kama ambavyo Mheshimiwa Mbuge ameomba.

Kwa hili swali la pili, anaomba niende Ludewa niseme nimekubali tutapanga nitashirikina na wataalam wangu wa Utalii ili tuweze kuambatana nao kwenda kuona namna gani tunaweza tukashirikiana kuvitangaza vivutio vya Utalii vya Mkoa wa Iringa.

Na. 76

**Kujenga Kiwanda cha Nyama – Arusha**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kujenga Viwanda vya Nyama kwenye Mikoa inayofuga kama vile Arusha, Manyara, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Morogoro na kadhalika:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kiwanda cha Nyama Mkoani Arusha?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na sera za sasa za uchumi wa soko, Serikali imejiondoa katika shughuli za uzalishaji, usindikaji na masoko na kukabidhi majukumu hayo kwa sekta binafsi. Katika kutimiza azma hii, baadhi ya wawekezaji kutoka sekta

binafsi wamejenga machinjio na viwanda vitatu (3) vya kisasa vya kusindika nyama vya Sumbawanga *Agricultural and Animal Feeds* (Sumbawanga, Rukwa). *Tanzania Pride Mea*t (Mvomero, Morogoro) na *Mkuza Chicks* (Kibaha, Pwani).

Aidha, Serikali imeuza asilimia 51 ya hisa za machinjio ya kisasa ya Dodoma kwa Kampuni ya *National Investment Company Limited (NICOL)* na asilimia 49 zimechukuliwa na Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO).* Vile vile, Wizara imebinafsisha Kiwanda cha Kusindika Nyama cha Shinyanga kwa Kampuni ya *Triple "S" Beef Limited.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasi hii ndogo ya uwekezaji katika viwanda vya nyama, Serikali ilitangaza katika vyombo vya habari zabuni ya kutafuta watu wenye nia ya kuwekeza kwenye viwanda vya kusindika nyama (*Expression of Interest*) kujitokeza kwa lengo la kuingia ubia na *NARCO* katika kujenga, kuendesha na kusimamia viwanda/machinjio katika Mikoa ya Kagera, Mwanza, Musoma, Arusha, Mbeya na Pwani.

Mheshimiwa Spika, tathmini/uchunguzi uliofanywa na Wizara kwa kushirikiana na *NARCO* umebaini kuwa wawekezaji wachache waliojitokeza hawakuwa na sifa zinazostahili kuwekeza. Ili kutimiza azma hiyo Serikali ilitangaza upya zabuni kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa machinjio/viwanda vya nyama katika maeneo yote yaliyoainishwa kwa uwekezaji katika mikoa mbalimbali nchini ukiwemo Mkoa wa Arusha. Aidha, Wizara inaangalia uwezekano wa kulikabidhi suala hili moja kwa moja *NARCO* ili wakipata fedha waweze kujenga viwanda husika.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize masuala mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa ni muda mrefu sasa mifugo kutoka Mara, Shinyanga, Kigwe Arusha, Manyara na Kilimanjaro wanakwenda Kenya na kukuza uchumi wa Kenya. Je, Naibu Waziri haoni kwamba ni hasara kwetu kutopata uchumi wa nchi yetu?

Swali la pili, kwa kuwa ni kwa muda mrefu sasa kilio changu hapa Bungeni ni kudai kiwanda katika Mkoa wa Arusha. Je, Serikali haioni kwamba kilio cha Mbunge ni kilio cha wananchi na ni muda mrefu tukidai kwamba wananchi wanahitaji Kiwanda hicho. Je, lini sasa Serikali itachukua hatua na kutujengea kiwanda ili wananchi wawe na maisha bora na mifugo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nimetembelea katika sehemu hizo anazosema, nimetembelea jimbo lake, nafahamu kule Mkoa wa Mara ninakotoka. Vile vile nimetembelea Mkoa wa Arusha ng'ombe wengi sana kutoka Tanzania wanapelekwa Kenya kwa kiwanda cha *AGRIPA* kwa ajili ya mauzo huko na hao katika kiwanda hicho kwa ajili ya Nyama. Sisi kwa sababu hatuna kiwanda na masoko hayapo basi wananchi inabidi wapeleke ng'ombe Kenya.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema sisi tumetangaza na tunatafuta mtu au wawekezaji ili waweze kujenga viwanda katika Mkoa wa Arusha na sehemu nyingine, lakini hatujapata mtu. Sasa hivi tunatangaza lakini kitu ambacho tumeona kama tutashindwa kabisa tunahitaji kuweka katika Bajeti yetu tunakuomba fedha ambazo tutajenga viwanda katika katika mikoa hii. Kwa sababu hasara tunayoipata lazima tukiri ni kubwa hamna sababu yoyote ng'ombe toka Shinyanga, Arusha, Mara na sehemu zingine na kupelekwa kufaidisha nchi ya jirani.

Kwa hiyo, ningeliomba Mheshimiwa Mbunge uvute subira ili tuweze kuona kama tutakwenda kutafuta wawekezaji na kama hawatapatikana nafikiri hili jukumu tulichukue na kulipeleka Serikalini ili tupate fedha. Nimeshaongea na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na tukaona kwamba hilo ni *posibility* ya kuweza kuomba hela ili Serikali kwa kweli ijenge Viwanda hivi kama tulivyofanya hiki cha Dodoma. Tulipojenga hiki kiwanda cha Dodoma, kwa sasa hivi tumeshakikabidhi kwa *NILCO* pamoja na *NARCO* wameingia ubia *NILCO (51)* na *NARCO 49* na kinafanya kazi. Sasa nafikiri hii njia na huenda tukaitumia zaidi.

**MHE. JOYCE M. MASSUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Swali hili linafanana sana na la mkoa wetu wa Shinyanga pamoja na Mkoa wa Arusha.

Kwa kuwa tulisikia kuwa tumepata mwekezaji katika Kiwanda chetu cha Shinyanga na mpaka sasa hakuna chochote kinachoendelea. Je, Serikali inatueleza nini wananchi wa Shinyanga kuhusu kiwanda hiki cha Shinyanga kuhusu suala letu la nyama? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama wiki moja iliyopita tumepokea habari ambayo si ya kuridhisha kabisa kutoka kwa watu waliopewa hiki Kiwanda cha *Triple S.* ambacho kipo Shinyanga. Wametuandikia kwamba kwa sababu ya hali mbaya ya uchumi hawataweza kujenga kiwanda hicho na wanaomba tuwatafutie mbia ama sivyo tukichukue.

Kwa hiyo, Wizara yangu itachukua jukumu hilo tena ili tuwanyang'anye tukitangaze upya. Kwa hiyo, kwa kweli bado kabisa kazi ya hiki kiwanda kuanza kufanya kazi, lakini namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutachukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba kiwanda hiki kinaanza kazi haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Na. 77

**Umeme wa Vijiji vya Daluni, Gombero na Kwale**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kulikuwa na utata na mgongano kati ya kauli za Serikali Bungeni kwamba, umeme katika Vijiji vya Daluni, Gombero na Kwale ungewekwa chini ya

Mradi wa Umeme Vijijini Lakini Kiongozi Mwandamizi wa *TANESCO* kwenye mkutano wa Kamati ya Maendeleo ya Mkoa *(RCC)* wa Tanga alitoa kauli ya kukanusha kauli za Serikali Bungeni, hali iliyoleta mashaka makubwa kwa Viongozi na wananchi wa Mkinga; na kwa kuwa, hali hiyo ya hofu imeongezeka kutokana na kutojibiwa kwa barua Kumb. Na. MB/MK/Misc. 178/08 ya tarehe 25/7/2008 kutoka kwa Mbunge wa Mkinga kwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji wa *TANESCO:-*

(a) Je, Serikali inatoa uhakikisho gani wa utekelezaji wa mradi huo na sasa kuhusu tarehe halisi ya kuanza utekelezaji wake?

(b) Je, Serikali inaweza kufikiria kukipatia umeme Kijiji cha Vuga, Kata ya Kigongoni ambapo umeme unatarajiwa kupitia kutoka Mwele kwenda Daluni?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa upelekaji umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *REA* na ule wa usambazaji umeme katika mikoa sita ya Tanzania unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani chini ya programu ya *MCC.* Ni mipango miwili tofauti yenye lengo la kuhakikisha upatikanaji wa umeme nchini. Wakati Wizara yangu inawasilisha Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2008/2009 hapa Bungeni tarehe 9 Julai, 2008 ilieleza kuwa vijiji vya Daluni, Gombero na Kwale vitapatiwa umeme chini ya ufadhili wa Mfuko wa Umeme Vijijini *(REA/REF).*

Kiongozi Mwandamizi wa *TANESCO* anayenukuliwa kwenye swali la msingi alikuwa ni Mratibu wa Mpango wa Mradi wa *MCC.* Alialikwa kuhudhuria kikao hicho cha Kamati ya Maendeleo ya Mkoa wa Tanga *(RCC)* alipokuwa katika ziara ya kikazi Mkoani Tanga. Pamoja na mambo mengine alielezea miradi ya umeme inayotarajiwa kutekelezwa katika Mkoa wa Tanga chini ya mpango wa *MCC* ambapo vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge havikuwemo.

Ukweli ni kwamba vijiji vya Daluni, Gombero na Kwale viko chini ya ufadhili wa Mfuko wa Umeme Vijijini *(REA/REF)* kama ilivyoelezwa hapa Bungeni na si chini ya ufadhili wa MCC. Hivyo, Kiongozi Mwandamizi wa *TANESCO* alikuwa sahihi kwa kuwa alikuwa anazungumzia miradi ya umeme iliyo chini ya *MCC* ambapo vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge kweli havimo.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo juu, Wilaya ya Mkinga ipo katika mpango wa kupatiwa umeme kwa ufadhili wa Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* ikishirikiana na *TANESCO.*

Kiasi cha shilingi 88,800,000 zimekwishatolewa kwa *TANESCO* na Mfuko wa Umeme Vijijini *(REA)* kwa ajili ya mradi huu. Fedha hizi zitatumika katika kazi za ujenzi wa kituo cha kupoza umeme na njia ya umeme ya msongo wa *KV 0.4* kwa ajili ya kuyapatia umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga. Aidha, kazi za ujenzi wa kituo cha kupoza umeme na upimaji na kuagiza vifaa zinaendelea. Kwa sasa kipaumbele kimewekwa katika kufikisha umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufikisha umeme maeneo mengine aliyotaja Mheshimiwa Mbunge, yaani Gombero, Daluni na Kwale.

(b)Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mpango wa kupeleka umeme vijijini ni endelevu na unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha, mara kwa mara huwa tunafafanua utaratibu wa kuchagua miradi hii na vigezo vinavyotumika.

Pamoja na vigezo mbalimbali vya kiuchumi na kijamii, kigezo kingine ni cha mradi kuwa endelevu na wenye tija. Yaani *Sustainability and Efficiency*, na vile vile ili miradi hii, iweze kuwa na kuunganishwa *Connectivity* na hiyo miradi mingine itakayopangwa au inayopangiwa utekelezaji.

Baada ya kukamilika kwa tathmini hizi ambazo ni jumuishi C*omprehensive* miradi ya maeneo husika yanatengewa fedha, na halafu Serikali, kupitia *TANESCO* na Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* itaweka kwenye Bajeti yake ya siku za usoni fedha kwa ajili ya kupelekea umeme maeneo yaliyobaki ikiwemo kijiji cha Vuga.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa fursa hii kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru kwa majibu marefu na fasaha kwa ya Mheshimiwa Waziri. Lakini ningependa kuuliza kwamba mpango unakuwaje katika Bajeti ya mwaka nilidhani kwamba mpango huo uko tayari kwa kutekeleza katika mwaka huu wa fedha uliotajwa.

Miradi hii iliyozungumzwa iliwekwa katika Bajeti ya mwaka jana na mwaka huu wa fedha niliamini kwamba miradi itakuwa katika utekelezaji wa mwaka huu. Swali langu la msingi sikuuliza juu ya Makao Makuu, nilijua kwamba tayari mpango huu ulikuwa tayari.

Je, ni lini hasa kama nilivyouliza katika swali la msingi mradi wa umeme kwenye vijiji vya Daluni, Gombero na Kwale itatekelezwa? Ahsante Mheshimiwa Spika.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, swali lilikuwa linaulizia kama mradi huu uko *REA* au *MCC.* Sasa nimemjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba swali liko kwenye kutekelezwa na *REA* kwa maana ya Wakala wa Nishati Vijijini.

Lakini hata hivyo labda nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba *TANESCO* imeshawasilisha Wakala wa Nishati Vijijini maombi ya jumla ya shilingi bilioni 3.76 kwa ajili ya kufikisha umeme vijiji vya Gomero, Daluni, Kwale pamoja na vijiji vilivyo jirani na maeneo hayo.

Kwa maana kwamba wakati tunaeleza mpango huu unatakiwa kufanya mwaka huu mpango umewekwa hapo lakini vile vile unategemea upatikanaji wa fedha kupitia Mfuko wa *REA*. Kwa hiyo, kazi za awali za kuufanyia tathmini mradi huu kazi zote hizo zimekamilika na kazi zinazotarajiwa kufanywa ni pamoja na ujenzi wa kilomita 69 ya njia za umeme ya msongo wa *KV 33* na *KV 11*. Ujenzi wa kilomita 21 za njia ya umeme wa msongo wa *KV 0.4* na kufunga vipoza umeme vipatavyo 11.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi za awali za tathmini pamoja na kubaini gharama na maombi ya fedha kwenda *REA* kutoka *TANESCO* yamekwishafanyika na hivyo natarajia kwamba kulingana na upatikanaji wa fedha, mradi huu utatekelezwa.

Na. 78

**Kuweka Nguzo za Umeme Kati ya Nachingwea na Liwale**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa, utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa gesi ya *Mnazi Bay* kwa Mikoa ya Mtwara na Lindi utekelezaji wake umeanza; na kwa kuwa, kufikisha umeme huo Liwale umbali wa kilomita 136 kutoka Nachingwea na kazi hiyo haijaanza:-

(a) Je, lini kazi hiyo ya kusambaza nguzo kati ya Nachingwea na Liwale itaanza ili umeme huo utakapofika Nachingwea ufike na Liwale pia?

(b) Je, ni Kampuni gani itakayosambaza nguzo hizo kati ya Nachingwea na Liwale na Serikali itakuwa na michango gani katika mchakato mzima?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umeme wa gesi ya *Mnazi Bay* kwa Mikoa ya Mtwara na Lindi umepangwa kuunganisha miji ya Ndanda, Nyangao, Newala, Mtwara na Nachingwea. Katika Bajeti ya mwaka huu 2008/2009 Serikali imetenga shilingi bilioni 8.7 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Mikataba kwa ajili ya uendelezaji wa mradi huu iliwekwa saini tarehe 12 Desemba, 2008. Hatua iliyofikiwa mpaka sasa ni uitishaji wa Tenda kwa ajili ya kumpata Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Mwendeshaji wa Miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme mtarajiwa anayejulikana kwa jina la Umoja *Light Company* alifanya tathmini ya kiufundi na kibiashara iliyobainisha kwamba ujenzi na uendeshaji wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Lindi hadi Liwale, kwa kupitia Nachingwea ulikuwa hauna maslahi ya kibiashara kwake. Kutokana na matokeo hayo ya tathmini ya kitaalam ya Mwendeshaji Mtarajiwa, Serikali inalazimika kuangalia uwezekano wa njia mbadala ya kuwapatia wananchi wa Liwale huduma ya umeme inayoaminika.

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya ahadi hii, Serikali itaendelea kutafuta fedha za kuwezesha ujenzi wa mradi huu na baada ya kupata fedha, taratibu stahili ikiwemo mchakato wa kumpata mzabuni utafanyika. Endapo fedha hizo zitapatikana kazi ya ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa *KV 33* kutoka Nachingwea hadi Liwale, yenye umbali wa kilomita 136, ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *KV 0.4* pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza na kusambaza umeme, inakadiriwa kazi hiyo kufanyika na kukamilika katika kipindi cha miezi 15 tangu wakati itakapoanza. Makadirio ya awali yanaonyesha kwamba kiasi cha shilingi bilioni sita zitahitajika kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kazi ya kusambaza nguzo haijaanza kutokana na sababu zilizoelezwa hapo juu.

(b) Mheshimiwa Spika, bado haijajulikana ni Kampuni gani itapewa kazi ya kusambaza nguzo kati ya Nachingwea na Liwale, kwa kuwa uamuzi wa kufanya mradi huo haujapangwa.

Serikali kupitia *TANESCO* tutafanya tathmini ya ziada na pia kwa kuzingatia njia mbadala kwa kuwatumia *REA* na *TANESCO* tutahakikisha tunafanikisha utekelezaji wa azma hii.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri. Kutokana na umuhimu wa Wilaya ya Liwale na kwa kuwa ipo pembezoni na pia mchango wake kutokana na maliasili, misitu na wanyamapori kwa kuzingatia kwamba ndipo inapofanyika kwa kiasi kikubwa uwindaji wa kitalii, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha ili zoezi hilo lianze kufanyika mapema na tathimini ifanyika haraka iwezekanavyo?

La pili, hivi sasa Liwale inatumia ma-*generator* aina ya *Rose royce*, ma-*generator* hayo ni s*ervicealb*e tatizo kubwa ni upatikanaji wa vipuri, na kwamba *TANESCO* sasa hivi inasinzia kupeleka vipuri katika maeneo kama Liwale eti tu kwa kufikiria kwamba Liwale huenda ikawa chini ya *ARTMUS* au mwekezaji mwingine kwa ajili ya umeme.

Je, sasa hivi nikitoa orodha ya vipuri ambavyo vinahitajika kwa ajili ya ma-*generator* ya Liwale aina ya *Rose Royce* ili tusaidiwe upatikanaji wake haraka sana. Waziri yupo tayari kupokea?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameniuliza kama tumefanya tathmini ya umuhimu wa upatikanaji wa umeme Liwale. Ni kweli tathmini hiyo tumeifanya na ndio maana nikasema kwamba ile kazi ya kutoa umeme kutoka Nachingwea kwenda Liwale imeandaliwa lakini kwa kuzingatia vigezo vilevile ambavyo nilikuwa natumia wakati najibu swali la kwanza tumeangalia kwamba tuangalie mpango mbadala wa kuhakikisha kwamba umeme unapatikana pale.

Kama nilivyosema katika vigezo hivyo nimekubali kwamba kweli kuna uwindaji mkubwa na masuala ya kwamba ya maeneo kidogo ya pembezoni lakini naomba nimhakikishie kwamba tathimini tuliyofanya imezingatia vigezo vyote hivyo na tunaendelea kufanya kazi hii nitaendelea kuwasiliana naye kulingana na mafanikio tutakayopata.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, hili la vifaa vya *Rose Royce*. Labda niseme tu na nimwambie Mheshimiwa Mbunge namshukuru sana kwa sababu hili suala Mheshimiwa Mbunge alishakuja ofisini kwangu amelizungumzia ameniahidi kwamba ataniletea orodha ya vifaa hivyo kulingana na tathmini iliyofanywa na hao wataalamu huko na mimi ninakubali kabisa kwamba nitaipokea na kwa dharura kabisa nitaiwakilisha *TANESCO* kwa ajili ya utekelezaji.

Lakini nataka niweke angalizo tu kwamba katika uagizaji huu wa vifaa na namna ambavyo uagizaji wa vifaa unavyofanywa hii *process* kidogo inachelewa na hata hivi sasa vifaa vya Kigoma na Sumbawanga viko bandarini kwa muda wa miezi kama mmoja na nusu au miwili na bado tunashinikizana. Kwa hiyo, naomba niipokee hiyo orodha na nakuahidi kwamba tunavyofanyia dharura uingizaji wa vifaa vingine na hilo nalo tutalipitisha kwenye dharura hiyo hiyo.

Na. 79

**Uhakika wa Mbolea ya Ruzuku**
**Inayotolewa Mikoani**

**MHE. MARTH J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mahitaji na matumizi ya mbolea kwa maeneo mbalimbali ni suala la kitaalam na hasa wataalam wa Kilimo; na kwa kuwa, suala la uagizaji wa mbolea ya ruzuku mara nyingi hufanywa na Wanasiasa na Wabunge, ambao wengine siyo wataalam wa kilimo:-

Je, hiyo ruzuku ya mbolea inayotengwa kwa maeneo mbalimbali ya nchi yetu huhakikiwa na nani juu ya aina na gharama ya mbolea inayohitajika?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kupitia vituo vyake vya utafiti hufanya utafiti juu ya viwango vya virutubisho vilivyopo katika udongo katika maeneo mbalimbali nchini.

Taarifa inayopatikana kutokana na utafiti huo ndio inayotumika kuamua aina ya mbolea inayofaa kutumika katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa hiyo, kazi ya kutambua na kuamua aina ya mbolea inayofaa kutumika katika maeneo mbalimbali nchini hufanywa na wataalam wa kilimo na siyo wanasiasa.

Ili kutambua viwango vya mahitaji ya mbolea katika maeneo mbalimbali nchini, kabla ya msimu wa kilimo kuanza, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika hukusanya taarifa za makadirio ya mahitaji ya mbolea katika mikoa mbalimbali nchini kuipitia Sekretarieti za Mikoa. Baada ya kupokea taarifa na takwimu hizo za makadirio ya mahitaji, Wizara huitisha kikao cha wafanyabiashara wa mbolea na kuwapatia taarifa na takwimu hizo ili wazitumie katika mipango yao ya uagizaji na usambazaji wa mbolea.

Aidha, taarifa na takwimu hizo za mahitaji ya mbolea nchini ndizo zinazotumika kukadiria kiwango cha mbolea ya ruzuku kinachoingizwa katika mpango wa Serikali wa kugharamia ruzuku ya mbolea kulingana na uwezo wa Serikali wa kugharamia ruzuku ya mbolea katika msimu husika. Kwa hiyo, kutokana na maelezo hayo, Serikali ndiyo yenye jukumu la kuainisha aina ya mbolea inayohitajika katika maeneo mbalimbali nchini, kukusanya taarifa na takwimu za viwango vya mahitaji ya mbolea na kupanga viwango vya mbolea itakayoingizwa katika utaratibu wa ruzuku kulingana na uwezo wake wa kifedha katika msimu husika.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali mawili madogo ya Nyongeza. Pamoja na uhimizaji wa matumizi ya mbolea hizi za Viwandani, ambazo ni ghali na upatikanaji wake ni wa shida. Kwa nini Serikali isihimize na pengine kutoa ruzuku kwa ajili ya mbolea za asili kama mboji na samadi ambayo ni rahisi kutumia na wakulima wadogo wadogo kwa mfano wakulima wa Mkoa wa Manyara.

Swali pili, kwa kuwa katika dunia hii ya utandawazi, thamani katika biashara ya mazao ya chakula, thamani ya mazao inaenda pamoja na ongezeko la thamani, na kwa thamani hapa nina maana ya kwamba matumizi madogo au isiyo kuwa na matumizi ya mbolea zenye kemikali. Je, Serikali ina mpango upi wa muda mrefu wa kuhimiza pengine *organic farming* ambayo inaendelea kupata nguvu katika soko la dunia?.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Serikali kwa ujumla tutahimiza matumizi ya aina zingine za mbolea kama mbolea zingine za mboji au mbolea ya samadi.

Lakini kwa mfumo wa mbolea ya mboji na samadi, ni vigumu sana kuweza kuitolea ruzuku kwa sababu ruzuku ile inaenda katika bei.

Lakini kama mtu ana zizi la mifugo na anachukua mbolea kwenye zizi lake kupeleka shambani siwezi kujua ni namna gani unaweza ukampa ruzuku mtu wa namna ile. Isipokuwa kupitia mpango wa *ASDP* mipango ya kuwasaidia wakulima kupata vitu kama mikokoteni, inawezekana ili kuwasaidia kuweza kubeba ile mbolea na kuifikisha shambani kwake kwa urahisi zaidi kuliko kutotumia chombo hicho muhimu. Kwa namna hiyo Serikali inaweza ikashiriki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la matumizi kwa ajili ya *organic* kwa ajili ya kupunguza matumizi ya *organic*. Ni kweli duniani hapa kuna soko linaloendelea kukua, ambalo linahitaji mazao ambayo hayatumii kemikali, na tumeanza kuwatia moyo wakulima na viko vyama vya wakulima tayari ambavyo vinatilia mkazo kilimo cha *organic* kwa ajili ya kulipata soko hili.

Lakini hiki ni kitu ambacho kinaenda pole pole sana na kwamba huwezi kwa muda mfupi sana ukaacha kutumia mbolea ya viwandani na ukaanza kutumia mbolea zile zisizokuwa na kemikali kwa sababu hazipatikani kwa wingi sana hapa nchini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ili tumalize haya maswali tunakwenda swali linalofuata linaloulizwa sasa na Mheshimiwa Castor Ligallama, Mbunge wa Kilombero kwa Wizara hiyo hiyo ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Na. 80

## Kilimo cha Kakao Kilombero

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakulima wengi wa Kilombero katika Kata za Mbingu, Mchombe, Mofu, Chita na Mlimba wamehamasika sana na kilimo cha Kakao (*Cocoa*) ambayo hustawi sana katika maeneo hayo:-

(a) Je, Serikali itatoa msaada gani wa kiugani ili zao lilimwe, kibiashara pamoja na kuwapeleka Maafisa hao nchini Ghana kujifunza kilimo cha zao hili?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuwatafutia wakulima hao bei nzuri ya zao la kakao?

(c) Je, ni lini Serikali itaunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko ili kushughulikia zao hili la kakao, ufuta, alizeti na mengine yanayolimwa kwa wingi nchini?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ligallama, Mbunge wa Kilombero lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Halmashauri ya Kilombero ikishirikiana na wakulima wa kakao katika Wilaya ya Kilombero, inatekeleza mpango wa kuendeleza zao hilo ambapo jumla ya wataalam saba kati ya wataalam 45 waliopo katika Wilaya hiyo pamoja na majukumu mengine wamepangiwa majukumu ya uendelezaji wa zao la kakao. Majukumu yao ni pamoja na kuwafundisha wakulima mbinu bora za kilimo cha kakao, mbinu ya uvunaji na kuwapatia taarifa za upatikanaji wa masoko. Kutokana na juhudi hizo, uzalishaji wa kakao katika Wilaya ya Kilombero umekuwa ukiongezeka. Kwa mfano uzalishaji umeongezeka kutoka tani 35 za kakao zilizozalishwa mwaka 2005/2006 hadi tani 61 mwaka 2006/2007. Uzalishaji umeendelea kuongezeka na sasa kufikia tani 122 zilizowasilishwa katika mwaka 2007/2008. Wizara inakubaliana na wazo la kuwapeleka wataalam hao kusomea kilimo bora cha kakao nchini Ghana na nchi nyingine. Hivyo, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ikishirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko itaendelea kuwatafutia wakulima wa kakao masoko yenye bei nzuri ya zao hilo ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara itawasiliana na Halmashauri ya Kilombero kwa lengo la kuhakikisha wataalam hao wanapatiwa fursa za mafunzo kupitia ruzuku ya kuimarisha huduma za ugani inayopelekwa katika Halmashauri hiyo kwa ajili ya utekelezaji wa *DADPs*.

(b) Kakao yote inayozalishwa nchini hununuliwa na wanunuzi binafsi ambazo huuza katika soko la nje. Baadhi ya makampuni hayo ni Bioland, Olam, Biota na *Mohamed Enterprises* na kampuni ya Uhai ambayo hununua kakao iliyozalishwa katika utaratibu wa kilimo hai *(organic cacao*). Aidha, Wizara inawashauri wakulima wa kakao kujiunga katika ushirika ili waweze kuwa na sauti moja katika kujadiliana bei ya kakao wanayozalisha. Wizara itawasiliana na Halmashauri ya Kilombero katika kuhakikisha wakulima wa kakao wanahamasishwa kujiunga katika ushirika ili wauze kakao yao kupitia utaratibu wa stakabadhi za mazao ghalani (*warehouse receipt system*). Utaratibu huo pale unapotumiwa umeoneshwa kuwa na manufaa makubwa kwa wakulima katika kuwawezesha kupata bei nzuri ya mazao yao.

(c) Serikali imeridhia kuundwa kwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko na Wizara imeanza kutekeleza mchakato wa uundwaji wa Bodi hiyo unaohusisha uandaaji wa rasimu ya Muswada wa Sheria ya kuanzisha Bodi hiyo ambao utawasilishwa Bungeni mara ukiwa tayari.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mazao kama chai, kahawa huwa yanasindikwa hapa nchini na kuyaongezea thamani. Je, Wizara kwa kushirikiana na Biashara na Masoko wanaweza kuwasaidia wakulima hawa wa Kilombero na Kyela ili tukasindika zao hili hapa hapa nchini ili liongezewe thamani?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, mazao yote yanasindikwa hapa nchini au na sekta binafsi au Vyama vya Ushirika. Kwa hiyo, nashauri kwamba wakati zao la kokoa linaendelea kuongezeka ni vizuri kutazama uwezekano wa kushirikisha sekta binafsi katika kuliongezea thamani yaani *value addition*, lakini kama hiyo haitawezekana kwa sekta binafsi basi nawashauri wakulima wa kokoa waanze kujiunga katika Vyama vya Ushirika ili hatimaye wao wenyewe waweze kuwekeza katika uongezaji wa thamani ya mazao yao.

Na. 81

**Kukarabati Barabara ya Nyashimo –Shigala – Ngasamo**

**MHE. DR. FESTUS M. LIMBU (k.n.y MHE. DR. RAPAHEL M. CHEGENI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Nyashimo –Shigala –Ngasamo inatumika kupitisha magari makubwa yenye uzito wa zaidi ya tani 10 wakati uwezo wake ni mdogo:-

(a) Je, ni lini barabara hiyo itapandishwa hadhi na kuwa barabara kuu (*trunk road)* badala ya sasa ambapo ni barabara ya Mkoa?

(b) Je, ni lini barabara hiyo itakarabatiwa kwa kiwango cha kuwezesha magari yenye uzito mkubwa kupita muda wote?

**NAIBU WAZIRI MIUNDIMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Jimbo la Busega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Barabara namba 13 ya mwaka 2007, vigezo vya kimatumizi huzingatiwa kuainisha madaraja stahiki ya kila barabara nchini, kifungu na. 12 (2) kinatoa vigezo kwa Barabara Kuu na Barabara za Mkoa. Barabara za Mikoa na Barabara Kuu zote huhudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini –*TANROADS*.

Kwa kutumia tafsiri ya kifungu hicho, barabara ya Nyashimo – Shigala –Ngasamo inakidhi vigezo vya kuwa Barabara ya Mkoa ambayo inaendelea kuhudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini –*TANROADS*.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyashimo –Shigala –Ngasamo yenye urefu wa kilomita 40 inaendelea kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara kukidhi matakwa ya kupitika mwaka mzima na kwa kutegemea uwezo bajeti.

Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2008/2009, jumla ya shilingi 270.6 milioni zimetumika kwa ajili ya matengenezo ya kawaida, muda maalum na ukarabati wa sehemu korofi na madaraja. Matengenezo haya yamewezesha barabara hii kupitika mwaka mzima bila tabu.

**MHE. DR. FESTUS M. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Nyashimo –Shigala – Ngasamo ni muhimu sana kuunganisha Wilaya ya Bariadi na Magu pamoja na Mwanza katika usafirishaji wa mazao mbalimbali ikiwemo pamba, mahindi, mpunga na bidhaa za viwandani na kwa kuwa barabara ya kutoka Mwigumbi kwenda Lamadi inawekewa lami na kwa kuwa magari mengi sana yanapita katika barabara iliyotajwa. Je, Serikali haioni kuna umuhimu sasa wa kuiwekea lami barabara ya Ngasamo –Nyashimo ili kurahisisha upitaji wa mizigo pamoja na abiria?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii anayoiongelea ambayo imeulizwa katika swali la msingi na kwa kuzingatia kwamba barabara hii sasa inaunganishwa na barabara hiyo inayojengwa kwa lami Serikali ingependa kabisa na barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami. Lakini kama nilivyowaeleza katika jibu la msingi hapa ni uwezo wa bajeti ndiyo pingamizi kubwa. Kwa hiyo, niombe tu kwamba, Mheshimiwa awe na subira kadri

uwezo wa Serikali utakavyoimarika hapo baadae tunaweza tukaifikiria barabara hiyo ijengwe kwa kiwango cha lami.

Na. 82

**Kero Katika Makutano ya Barabara**

**MHE IDD M. AZZAN (k.n.y. MHE. CHARLES KEENJA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika makutano ya barabara ya Ubungo kuna kero kubwa inayosababisha watumiaji kukaa zaidi ya saa mbili kwenye misururu mirefu ya magari na kwamba baadhi ya watu hugongwa na magari yanayoendeshwa kwa kasi kati ya Ubungo na Kibaha:-

(a) Je, ni nini kinasababisha kero iliyopo kwenye barabara hiyo na nini ufumbuzi wake?

(b) Je, ni lini Serikali itaweka vipunguza mwendo kwenye maeneo zinakotokea ajali nyingi katika barabara ya Ubungo hadi Kibaha?

(c) Je, Serikali ina mipango gani ya kupunguza misururu ya magari kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam hususan katika makutano ya barabara?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati wa miaka ya 1990 na kurudi nyuma ununuzi wa magari kwa watu binafsi ulikuwa unasimamiwa na Serikali kwa kutoa vibali vya ununuzi wa magari na kusababisha ongezeko dogo la magari nchini. Hivyo usanifu wa barabara zetu ulizingatia viwango hivyo ambavyo ni vya magari machache. Baada ya miaka ya 1990, Serikali iliacha kusimamia uuzaji na uingizaji wa magari nchini na kazi hii iliachwa iendeshwe na watu binafsi. Hali hii ikichangiwa na ukuaji wa kipato cha wananchi, imewezesha watu kununua magari kwa ajili ya kuwawezesha kuendesha shughuli zao za uchumi ambalo kwa kweli ni jambo la maendeleo na kusababisha msongamano wa magari hasa katika barabara zetu za Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaliona tatizo hilo na kama tulivyoeleza humu Bungeni mara kadhaa, Serikali imekuwa na mikakati mbalimbali ili kupunguza msongamano huo. Mikakati hii ni pamoja na mradi wa mabasi yanayokwenda kasi, upanuzi wa ukarabati wa barabara kuu muhimu ya Sam Nujoma, upanuzi wa barabara za Kilwa na Mandela unaoendelea hivi sasa, ukarabati wa barabara viunganishi na barabara za pembezoni mwa Jiji, uanzishaji wa usafiri wa boti majini kandokando mwa ufukwe wa bahari na uboreshaji wa taa za barabarani na za kuongozea magari.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2008/2009, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara zitakazopunguza msongamano wa magari ambzo ni barabara za Ubungo –Kigogo – Jangwani – Jengo la *Club* ya Yanga (km. 9.6); Tabata –Dampo –Kigogo –Ubungo Maziwa –External; *Old* Bagamoyo (Morocco – JKT Mlalakuwa); barabara ya TPDC; Mbezi (Morogoro Road –Malamba mawili –Kinyelezi –Banana; *Jet Corner* –Yombo Vituka *Davis Corner*; Tegeta Kibaoni -Wazo Hill –Goba Mbezi Mwisho; Tangi Bovu – Goba; Kimara Baruti –Msewe –Changanyikeni na Barabara ya Kimara –Kilungule – *External* (Mandela). Barabara hizo zipo katika hatua mbalimbali za usanifu wa kina kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Aidha, uchunguzi uliofanywa kwa ufadhili wa *JICA* kwa ajili ya kutengeneza *'City Transport Master Plan'* umependekeza kuboresha makutano ya baadhi ya barabara muhimu Jijini Dar es Salaam kwa kujenga *fly-over* ikiwemo makutano ya Ubungo, Magomeni, Jangwani (*Fire*), Kamata, TAZARA na Makutano ya barabara ya Nyerere na Kawawa (Chang'ombe). Hivi sasa Serikali inapitia ushauri huo na kutafuta fedha za kutekeleza ujenzi wake.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hivi sasa Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) imeanza kuweka alama na matuta ya kupunguza mwendo katika maeneo mbalimbali zinakotokea ajali katika barabara ya Ubungo hadi Kibaha.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri nafikiri atakubaliana nami kwamba hivi karibuni Mheshimiwa Rais amekuwa akitoa maelekezo kutokana na hali ya msongamano iliyopo Dar es Salaam kwamba angalau tuangalie uwezekano sasa wa kujenga barabara za ghorofa hasa katika maeneo ya Ubungo inapoungana na Mandela Road. Je, Wizara ina mpango gani wa makusudi kabisa kuhakikisha tunaanza utekelezaji wa elekezo hilo la Rais wa kujenga barabara hizo za *fly overs*?

**NAIBU WAZIRI MIUNDIMBINU:** Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza kutekeleza mpango huo wa kujenga *fly overs* kama nilivyoeleza katika jibu la msingi hapa. Uchunguzi umeshafanyika na sasa hivi Serikali inaupitia huo uchunguzi na kuanza kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo. Kwa hiyo, kwa kweli utekelezaji wa agizo la Rais umekwishaanza.

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Sasa ni matangazo na tunaanza na wageni. Tunao wageni kutoka Bunge la Malawi nchi jirani ambao ni watumishi waandamizi katika Bunge hilo wanaongozwa na Bwana Leonard Mengezi Afisa Uhusiano Mkuu, *Principal Public Relation Officer, Welcome to Dodoma we are happy to see you.* Yupo pia Ndugu Brakson Mkupatira, Mhariri wa *Hansard* kule kwenye Bunge la Malawi; yupo Ms Judith Hassan Mwandishi wa Taarifa Rasmi za Bunge; yupo Bi, Helen Gondwe, yeye pia ni Mwandishi na Bwana Livingstone Tamani ambaye ni Mhasibu Msaidizi katika Bunge la Malawi. *It is pressure*

*to welcome you in the House here in Dodoma. We have excellent relations with you as neighbours Malawi and always is a pressure to exchange the experiences. Thanks very much and send our regards when you go back home.* (*Makofi*)

Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Emmanuel Luhahula na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa ni Ndugu James Seni Mwenyekiti, wa Tawi la CCM Kanegele, Kata ya Bukandwe, Jimbo la Bukombe. Karibu sana.

Baada ya kumaliza matangazo ya wageni sasa ni matangazo ya kazi. Kwanza niseme tu bila kutarajia inabidi tuwe na Kamati ya Uongozi sasa hivi nikimaliza kusoma matangazo haya. Ni dharura na naomba Wenyeviti wote tukutane hapa baada ya hapo mtaendelea na shughuli zenu. *Speaker's Lounge* sio kule tena, ni hapa hapa mambo mengine yanamalizwa hapa hapa kwa haraka, si mnajua tena *speed* za Spika hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji anahitaji Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji mkutane leo saa tano katika, Ukumbi namba 227.

Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Huduma za Jamii mkutane leo saa tano asubuhi, Ukumbi namba 219.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini anahitaji Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini wakutane saa saba mchana leo, Ukumbi namba 227.

Mheshimiwa Mohamed Misanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anaomba pia saa saba mchana katika Ukumbi Pius Msekwa Wajumbe wote wakutane humo kwa Kikao muhimu sana.

Huu ndio mwisho wa matangazo. Sasa namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama aje ili aendeleze shughuli za Bunge wakati tunaendelea na kikao cha dharura.

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea matangazo yaliyokuwa hapa mezani kwa Spika, naomba sasa tuendelee na utaratibu wa *order paper* yetu na naomba Katibu atupe mwongozo wa kuendelea na kazi zetu za leo. Katibu.

## MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada ya Sheria ya Serikali Uhifadhi wa Wanyamapori wa Mwaka 2008
### *(The Wildlife Conservation Bill 2008)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia suala hili nikiwa wa kwanza kwa leo. Kwanza, nataka kusema kwamba kwa wale watu ambao tunamwamini Mwenyezi Mungu, Mungu aliumba dunia na mbingu na aliwekwa binadam kuja kutawala dunia na kwa sasa dunia inatawaliwa na binadam. Sasa nashangaa ninapoona kwamba Mnyama anapewa nafasi kubwa kuliko binadamu mwenyewe. Nasema hili kwa sababu kule Kilwa kwa ujumla wanyama wanavyolindwa ni kuliko binadam wenyewe, maana yake hata wanapoingia hawa ndovu kuja kushambulia kwenye mashamba yetu, wanavuruga kila kitu halafu wengine wanaua.

Kwa mfano, yule aliyenisaidia katika uchaguzi katika mwaka 2005 alishawahi kukamatwa na simba, bahati nzuri wakamuwahi yule simba na wakamuua kwa mishale. Sasa kama pale ingekuwa labda tupige simu Wilayani ambapo Wilaya iko mbali kweli kweli au kama tungesubiri mpaka tupate Muswada huyu Msaidizi wangu Abdallah Maiki angeshakuwa marehemu, lakini ni kudra za Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Kijiji cha Somanga wanakuja pale tunapaita kwenye upenu, wanakunywa maji ya mitungi, sasa nikiwa na bunduki eti nisiwapige kwa sababu ya kuogopa Bwana Wanyamapori kuja kunishtaki eti kwa sababu nimeua ndovu ambaye amevunja hadi mtungi wa maji yangu. Hii si halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili ni kwamba unajua binadam mwishoni tunaamua kupata hasira. Tunapopata hasira tunafanya vitendo vingine ambapo watu na dini zingine wanashangaa na utasema labda sisi hatufikirii vizuri, lakini ni hasira. Hata leo kula nyama ya simba japo kuwa najua simba haliwi lakini nitakula kwa sababu mwanangu kachukuliwa na simba. Kwa mfano mama anapika, kaja simba kamdokoa mwanangu kakimbia naye, unafikiri huyo wakimpiga nitamuacha bila kumla? Nitamla. Halafu kwa mfano ndugu zangu wale wa Mbinga na sehemu nyingine, utakuta wanakula hata nyani, tumbili wanawaita viganja ile ni hasira. Wengine wanakula hata ndovu kwa sababu ya hasira. Sasa Sheria ingewekwa kiasi ambacho binadam kwanza wengine wote wanafuata. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunaandaa Sera za Maji mwaka 2002 kabla sijawa Mbunge tulikuwa tunasema hivi maji ni kwa ajili ya binadam kwanza, pili wanyama, vingine vitafuata. Sasa sisi hapa kwenye Muswada huu tunaanza kuweka wanyama mbele, pesa mbele, kila kitu mbele. Nashangaa sana kuona kwamba wanyama wanawekwa mbele *as if* ndiyo wanaotupigia kura. Sisi tunapigiwa kura na binadamu, wananchi wangu wa Kilwa na tunakaa karibu na Mbuga ya Selous. Sasa wanyama wengi wanavuka mipaka wanakuja kwenye majumba ya watu wanatikisha embe, maboga yote yanaliwa, mashamba mpaka tunashangaa. Sasa unasema ukiwaua Bwana Nyama atakuja unaogopa, unaishia kujificha uvunguni kwa nini mambo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na kile kitendo cha pale Mikindani bwana mmoja ameweka waya kabisa kulinda wale wanyama wasije wakaingia ndani wakati wanapita kwa sababu wakipita wanakutana na waya ambao labda una umeme au una nini maana sijagusa na sijui. Lakini nimeona ule waya umewekwa, ile ni kama raha ya maisha kila mtu na kwake, dunia imepangwa kila mtu na kwake. Wewe kama ni wa porini kaa porini na sisi tunaopita njia tunapita njia. Sasa kupigia kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kwa maoni yangu, namwomba sana Mheshimiwa Waziri au Katibu Mkuu siku moja twende kutoka pale Njinjo kwenda mpaka Zinga mpaka Liwale. Halafu apate bahati mbaya aharibikiwe na gari apate pancha aone wanyama wanavyopita karibu karibu kama watashuka chini. Ndiyo watajua kabisa kwamba hii dunia. Barabara ni ya kwetu, tumejenga wenyewe lakini wanavyopita karibu karibu pale kusema kweli inatutisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuhusu mipaka, pale Miguruwe, Selous wameweka mpaka wao na wananchi wameweka mipaka yao. Tumegombana mpaka nimekwenda Wizarani kugombania ule mpaka, lakini mpaka sasa hivi tamko rasmi halijatolewa. Sehemu tunayogombania ni sehemu ambayo wanapata chakula, wanalima mpunga, mahindi na kila kitu, sasa wao wanasema hapana hapa papite mpaka wa Selous ili wanyama wapite. Hii kusema kweli inanihuzunisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza ni kuhusu hii *retention*, hizi 25 *percent*. Hii asilimia 25 ni ndogo mno, watu wanaliwa na simba, halafu tunajitahidi kuchunga misitu kama nini lakini unakuja kupata *25 percent why?* Ingekuwa *the other way round* wangepata 25 *percent*. Halafu 25 ingeenda kwenye Serikali Kuu au popote wapeleke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitalu watu wanaficha, wanaficha, wanaficha mpaka utafikiri labda pengine kile kitu ni cha namna gani sijui, Watanzania hawapewi nafasi ya haraka. Vingekuwa vinatolewa waziwazi kiasi ambacho mtu yeyote, hata mimi nikitaka kupata kitalu changu pale cha kuwindisha, niweze kupata. Lakini kinafichwa fichwa wee, utastukia tu fulani ambaye ni mkubwa kabisa anapata kitalu wakati mzawa wa pale ambaye ndio mwenyeji wa pale nakosa na halafu yule bwana ananinyanyasa, ananiambia wewe una nini, wewe huna *generator*, huna *tent* huna nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu zangu kwa mfano, kama hapa Bungeni hapa ni wachache sana, najua wapo ambao wana uwezo wa kuweka ma-*generator* kadhaa ma-*Landrover* kadhaa na kadhalika. Lakini, walio wengi uwezo huo hatuna. Sasa lakini vitalu tunavihitaji. Kusema kweli, ningeomba hili waliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kitu cha mwisho, nilikuwa nauliza, tunaruhusiwa kununua bunduki, bunduki *rifle*, mimi nina bunduki ya *rifle*, lakini kwa sababu ya matatizo yangu ya macho nimeiweka Polisi na nikiwa na matumaini kwamba siku moja nitakuwa na macho na nitaitumia ile *rifle* na ile *rifle* nailipia kila mwaka. Sasa ninapoilipia kila mwaka, kwa nini sasa walinipa bunduki, basi bunduki tungenyang’anywa wote Tanzania nzima kwa sababu tuwalinde wanyama wetu. Bunduki

ile imewekwa, piga mnyama kama anaku...nini? Ukiwa na bastola piga adui yako kama anataka kudhuru maisha yako, ndivyo inavyotakiwa duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuliambiwa na Mwenyezi Mungu tuje kutawala dunia na dunia lazima itawaliwe na sisi ndio wenyewe. Kwa hiyo, kwa kufupisha nasema kwamba, naamini kwamba Kamati ya kudumu iliyojadili Muswada huu imefanya kazi yake vizuri lakini haikumaliza *assignment* yake. Wangeweza kuchukua muda kidogo wakaweza wakaongezea ongezea vitu vyote na vitu vingine ambavyo wangeweza kuvipata kutoka kwa wananchi wanaozunguka kwenye haya mapori, kwa mfano kama *Selous* nini...? Sasa unaambiwa kitabu kidogo….

*(Hapa kengele ya kuashiria kwamba muda wa kuchangia Mheshimiwa Mbunge umekwisha ililia)*

Aaaah! Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja lakini kwa shingo upande. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie Muswada huu wa Wanyamapori katika dakika za mwisho kabla pengine Muswada huu haujahitimishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, nimpongeze pia ndugu yangu Naibu Waziri, Mkurugenzi wa Wanyamapori, Katibu Mkuu wa Wizara na Kamati ya Maliasili na Utalii kwa kushughulikia Muswada huu hadi kuufikisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimshukuru kipekee kabisa Mheshimiwa Waziri kwa sababu amekuwa ni kati ya Mawaziri wachache sana waliotembelea Loliondo na kuzungumza na Wananchi wa Kijiji cha Soitsambu na baadaye kutembelea zahanati iliyojengwa na mwekezaji katika Kijiji cha Lolosokwani. Namshukuru sana kwa sababu viongozi wanaofika huko ni wachache sana sijui ni kwa nini, sijui ni kwa sababu tupo pembezoni mno au nini sielewi kwa hiyo, mpongeza sana yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimetoa mualiko kwa viongozi wengine, Mawaziri wengine kama Profesa Mwakyusa, Waziri wa Afya; Profesa Msolla, Waziri wa Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Waziri wa Mawasiliano na Mheshimiwa Ngeleja wa Nishati na Madini. Nafikiri na wao kwa nyakati tofauti watatembelea Wilaya ya Ngorongoro na kutusaidia katika matatizo tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie viongozi hawa kwamba, jamani kufika Ngorongoro pia mnakuja kupumzisha vichwa vyenu baada ya kazi kubwa na hatihati ya Serikali na vitu vya namna hiyo. Eneo lile sio la kutembelewa tu na Wazungu, waende *Crater* ya Ngorongoro, waende Serengeti, kwa hiyo karibuni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwangunga alipofika Wilaya ya Ngorongoro na hasa kule Loliondo, alituambia mambo mawili ambayo nayakumbuka

vizuri sana. Moja alisema, wakati ule alipokuja tulikuwa na migogoro ya ardhi na kampuni moja ya Tomsom Safari ya Boston ya Marekani iliingia mgogoro na wananchi wa Kitongoji cha Sukenya. Lakini akasema hakuna watu wowote watakoondolewa katika ardhi yao, lakini la pili alisema ardhi itumike kwa manufaa ya wadau wote wakiwemo wananchi na wawekezaji. Haya ni maneno ambayo ni mazuri sana na yametutia moyo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya meneno haya ya utangulizi, napenda niseme kwamba Muswada huu wa Wanyamapori umechukua muda mrefu sana kufikishwa kwenye Bunge lako Tukufu, umechukua takribani karibu miaka minane unaongelewa, unajadiliwa na wadau mbalimbali wamejadili katika kanda za nchi yetu, tumefanya *public hearing* mwishoni mwa mwaka jana kule Arusha na Dar es Salaam na wadau kwa kweli walitoa maoni yao na baadhi ya maoni ya wadau yameheshimiwa na kuwekwa katika Muswada huu. Muswada huu ulichukua muda mrefu kwa sababu ya unyeti wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie zaidi eneo la *WMA*, ile sehemu ya tano ya Muswada, ukurasa ule wa 28 kwamba ukiondoa mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro inayosimamia eneo la kilometa za mraba 8300, Wilaya nyingine yote ya Ngorongoro inakuwa na kilometa za mraba zaidi ya 14,000/=. Kwa hiyo ukiondoa eneo la Ngorongoro linalosimamia basi eneo lingine lote liko chini ya *game controlled area* ambayo ni maarufu sana kwa eneo la Loliondo. Miji yangu miwili midogo, Loliondo yenyewe na Waso, Ofisi ya *DC*, Ofisi ya Halmashauri, zote ziko ndani ya *game controlled area* na *game controlled area* iko chini ya *hunting block* ambayo inasimamiwa na *Otelo Business Corporation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiniambia kwamba, katika Muswada huu kwamba wafugaji sasa hawataruhusiwa kutembea na silaha zao pale, hawataruhusiwa kuchunga mifugo katika *game controlled area*, kwa kweli haitawezekana kwa maeneo ambayo tunatoka sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti mbadala ya *game controlled area* ni *WMAs (wildlife management areas)*, ndiyo ambayo tunafikiri itakuwa ni ukombozi badala ya hii *game controlled area* kwa sababu hizi *WMAs* zitakuwa chini ya vijiji na mwekezaji yeyote atakayetaka kuwekeza humo, lazima apite katika Serikali ya Kijiji apate kibali na hati ya Serikali ya Kijiji, mwekezaji huyo ni lazima athibitishwe na Mkutano Mkuu wa Kijiji ndipo pengine Serikali ya Kijiji imgawie eneo la kuwekeza, kama ni eneo la kuwekeza utalii wa kiwindaji au *photographic* au vyovyote lakini itakuwa ni chini ya vijiji na hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna manufaa na wawekezaji wenyewe watakaopewa maeneo yale kupitia Serikali za vijiji, *actually* watakuwa wanawaheshimu wananchi na wataheshimu maeneo yanayomilikiwa na vijiji, tofauti na ilivyo sasa ambapo vibali vya namna hiyo vinatolewa na Mkurungezi wa wanyama pori kutoka Dar es Salaam, anakuja tu na kibali anaonyesha hii hapa, hamna lolote la kumfanya. Lakini kwa mabadiliko haya, tutakuwa tunawezesha vijiji na Wizara itakuwa tu inaangalia na kusimamia zile *regulations* ili hawa wawekezaji wasije wakaenda kinyume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi *WMAs* zitakuwa na manufaa kadhaa. Kwanza, maeneo ya vijiji yatathaminiwa, mapato ya vijiji yatakuwa ni makubwa zaidi na vijiji vitatakiwa pia vilipe kodi ya Serikali badala ya utaratibu uliopo wa kukusanya na kupelekwa Serikali Kuu na labda kidogo tena irudi baadae katika vijiji au Halmashauri zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji nao kama tulivyosema wataheshimu maeneo ya wananchi kwa sababu hawatapata maeneo ya kuwekeza kama hawataelewana na vijiji. Lakini pia utaratibu huu unaweza ukapunguza rushwa kwa namna fulani na kurubuniwa kwa viongozi wanaonyemelea ardhi za vijiji kwa sababu itakuwa tena sio watu wachache wataokuwa wanakwenda kubuni muhtasari na kumpa mtu eneo kwa sababu tu amepewa kitu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi pia kwa kutumia *WMAs* watakuwa wana uwezo wa ku-*renew* mikataba walioingia na wawekezaji au kuto-*renew*, tofauti na hali ilivyo sasa ambapo akipewa mwekezaji mahali, atakaa milele mpaka labda Mkurungezi wa wanyamapori aote ndoto sasa amwondoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nane ya Muswada, ukurasa ule wa 48 inahusu *Human Wildlife Conflict* na hasa kifungu cha 68 kipengele cha kwanza. Hii inahusu mambo ya fidia au kifuta machozi. Sisi huko Ngorongoro ni kweli kwanza nakubaliana na hoja kwamba huwezi ukafidia maisha ya mtu kwa *amount* yoyote ya pesa. Lakini serikali inajitahidi sana kwa sababu imeweka shilingi 200,000/= kwa mtu anayeuliwa na wanyamapori. Lakini kwa sisi Ngorongoro, naishukuru Bodi ya Ngorongoro kwa sababu hata mtu akiuawa na wanyama kule ndani ya eneo, ile fidia ilikuwa inatolewa laki moja, lakini sasa Bodi imekubali na imeshaanza kutekeleza hili, imepandishwa kutoka 100,000/= kwenda 500,000/=. *Alhamdulillah*, walau sio mbaya sana, inasaidia. Lakini hii nayo inatokana na mapato yanayopatikana na shirika lile kutoka kwa watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa wale watu ambao wanaumizwa tu bila kuuliwa na wanyama, vilevile wanalipa matibabu ya hospitali mpaka mtu aliyejeruhiwa awe amepona, jukumu hilo linachukuliwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Kama Serikali pia inaweza ikaiga utaratibu huu kwenye maeneo mengine itakuwa vizuri, kwetu inafanyika kwa sababu tunaishi na wale wanyama ndani, tofauti kabisa na maeneo ya *National Park* ambapo wananchi wamezunguka maeneo yale. Lakini sisi tuko nao toka asubuhi mpaka jioni na siku hizi wanyamapori wamezoea, unajua mnyamapori pia usipomsumbua kwa kumpiga au kumuua au kumjeruhi, hana shughuli yeyote na wewe hata kama ni simba au ni chui, unafika mahali mnazoeana, mnaheshimiana, wote ni madume tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri eneo hili tunaloishi na hasa eneo la wafugaji eneo la Ngorongoro, wanyamapori kama nilivyosema kwa kweli tunaungana nao kwa mambo mengi kwa maana ya mifugo yetu, majani huko porini yanatuunganisha, tunakutana nao kwenye maji, kulamba chumvi na vitu vya namna hiyo. Kwa hiyo,

tumezoeana na wanyamapori hasa wale wanaokula majani wamegundua kwamba ukiwa karibu na mifugo ndio unakuwa na usalama kwa sababu mifugo inachungwa na simba pia hawezi kukaribia karibu  na mifugo, kwa hiyo huyo mnyama atakuwa salama. Hata ikifika jioni tunaondoka kwenda nyumbani, tunasindikizana mpaka karibu na mlango wa boma, wao wanalala nje, mifugo inalala ndani. Hiki kimekuwa ni kitu cha kawaida kabisa na ndio hiyo faida ya kuwa na kitu kinachoitwa *multiple land use*, matumizi ya ardhi mseto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hawa tunawaita *problem animals* kama simba, chui, ndovu, mbogo na kadhalika. Nataka nipendekeze, kwa sababu inatokea tu *problem animals* akija akiua mifugo pale au akamuua mtu au akafanya nini, lakini ni baada ya kuchokozwa mahali fulani, basi kwa sababu anapita tu maeneo fulani anaweza kuumiza mifugo.  Kwa hiyo, nataka nipendekeze kama inawezekana shilingi 50,000 mpaka 70,000 mpaka 100,000 ikalipwa kwa mifugo ambayo imeumizwa au imeuliwa kabisa na wanyama hawa, ingekuwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, kule Lolosokwani wale wanyama ambao sasa hivi karibu watatoweka, mbwa mwitu walikula mbuzi karibu kumi huko. Sasa kwa sababu hakuna fidia, Wamasai wale wakaona utaiambia nini Serikali, haitasikia, kwa hiyo wakawauwa mbwa mwitu kati ya 21 na 25 na wale ni wanyama ambao wanaelekea kutoweka. Sasa hii ni mbaya na ndiyo maana tunajaribu kusema kwamba wanyama hao wakiharibu mazao au wakiua mifugo kitafutwe kifuta machozi angalau kidogo kufidia hawa ili hawa wafugaji wanunue hiyo mifugo japo kidogo na ku-*replace* mahali ambapo mnyama yule aliyeuliwa ametoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwindaji wa kitalii katika maeneo ya vijiji, vitalu vya uwindaji, nashauri kwamba vitolewe kwa wawekezaji na vijiji husika kama nilivyokwisha kusema chini ya usimamizi na uratibu wa Kamati za *WMAs* ambazo pengine kuna wataalam wa maliasili, kuna wataalam wa wanyamapori.  Wataalam pia wa ardhi  na maliasili watoe ushauri na utaalam juu ya uanzishwaji wa vitalu na mipangilio ya uwindaji ili kukwepa ile migogoro wakati wa *hunting* na mifugo iko hukohuko na wazingatie pia *grazing patterns* ya mifugo  ili visiingiliane na kipindi cha uwindaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ile *article number* 15, kipengele cha 3, ukurasa wa 22, inazungumzia habari ya *wetland areas* (ardhi owevu). Maeneo haya ni maeneo ya wananchi na kwangu  ni eneo la Ngaresero, eneo la Kijiji cha Pinyiny na eneo la kijiji cha Monik. Eneo hili liko ndani ya eneo la *Lake Natron*, pia kule ni *Ramsa Site* kwa mujibu wa *IUCN (International Union for Conservation of Nature)*. Sasa kama maeneo haya yanatakiwa yaangaliwe na sheria hii, ni vizuri basi kuzungumza vile vile na wadau muhimu wanaoishi katika maeneo haya ambao ni wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili pia ni eneo ambalo lina utalii mkubwa kwa sababu ya Mlima Lengai,  *Lake Natron* na *Flamingo* walioko huko. Lakini kuna vijiji viwili tu vilivyopimwa ndani ya Wilaya ya Ngorongoro kati ya vijiji 33, eneo hilo la Ngaresero na Kijiji cha Ololosokwani.  Ni vizuri Muswada huu kabla ya kupitishwa, ikazungumziwa

pia namna ya kutafuta maoni ya wananchi ili waweze kushirikishwa ili kupunguza migogoro ya maeneo hayo

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kama haya yataingizwa kwenye marekebisho, basi nitaunga mkono hoja. Ahsante sana! *(Makofi)*

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi asubuhi ya leo. Kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Mkurugenzi wa Wanyamapori kwa kutuletea Muswada huu ambao mimi binafsi naona Muswada umepitia maeneo karibu yote yanayohusu wanyamapori. Pia, binafsi, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu na hasa wale waliochangia kuhusiana na mbuga yetu ya wanyama iliyoko kule Mara, Mbuga ya Serengeti. Ni hakika kwamba Wizara itaona ni jinsi gani Wabunge hapa ndani walivyoona matatizo mengi yaliyoko kule Serengeti. Nina hakika kabla sijayasemea, Wizara itachukua hatua na kuhakikisha matatizo hayo yanapungua kule Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi, pamoja na Wabunge wenzangu, Muswada huu umetutia wasi wasi, lakini nafikiri kwa ushauri wangu binafsi, labda tukizingatia mambo kama mawili, matatu vile, Muswada huu unaweza kuwa ni Muswada mzuri na utatusaidia kupunguza matatizo yote kwenye mbuga zetu. Kwa mfano, binadamu wanaoishi kwenye maeneo ya wanyamapori ambao ni wakulima, kama kule kwangu Serengeti, wananchi wengi wanajishughulisha na shughuli ya kilimo. Sasa, tumekuwa na tatizo kubwa sana la wanyamapori hasa tembo, kwa sababu tembo wamekuwa wengi sana katika Mbuga ya Serengeti na hivyo huvamia mashamba ya wananchi na kula mazao yao. Hali hii inatusababishia tatizo la njaa kwa Wilaya hii mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia katika ukurasa 49 wa Muswada, hautaji kiwango maalum ambacho mwananchi huyu atalipwa na hiki kimekuwa ni kilio cha siku nyingi sana, watu hawalipwi mazao yao. Sasa sijui Wizara ilikuwa inafikiria nini, mnyama akiuawa, basi yule binadamu anatakiwa alipe. Lakini mnyama huyu huyu akivamia shamba la binadamu huyu, basi inakuwa ni mpaka majadiliano. Kwa kweli tunaomba Wizara ijaribu kulitafutia tatizo hili ufumbuzi ili sheria hii iweze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusiana na migogoro. Kwenye mbuga zetu hasa kule kwangu Serengeti kuna matatizo mengi sana ya migogoro ya ardhi. Tumepata matatizo mengi, wananchi wamekuwa wakigombana sana na wawekezaji. Kwa mfano, wananchi wa Kijiji cha Pakinyigoti na pori la Ikolongo, hili tatizo ni la siku nyingi sana. Nimpongeze tu Mkurugenzi wa Wanyamapori alijaribu kulitafutia ufumbuzi, lakini kwa sasa ni muda umepita, hatujajua ufumbuzi wake ni nini? Kwa hiyo, naomba wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, anieleze *situation* ipi iliyoko Wizarani katika suala zima la kuzuia huu mgogoro ulioko katika Kijiji cha Pakinyigoti na pori la Ikolongo

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechoka kusuluhisha migogoro kila siku, wananchi wanamvamia mwekezaji, mwekezaji anaona kama anaonewa na vile vile wananchi wanaona kama wanaonewa. Kwa hiyo, sheria sijui itatumikaje kama itatoke mwananchi

ataingia pale kwenye lile pori na wale Askari sasa hivi wameruhusiwa kutumia risasi. Kwa hiyo, naona wananchi wangu wengi wa Serengeti wanaweza wakadhurika na hiki kifungu kwa sababu watapigwa risasi. Kwa hiyo, naomba ufumbuzi upatikane, mpaka uwekwe kati ya Kijiji cha Pakinyigoti na hilo pori la Ikolongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho ambalo naona lingesaidia sana katika kutekeleza Muswada huu ni mafunzo ya uhifadhi. Kule kwetu Serengeti tulikuwa tunapewa mafunzo ambayo yalikuwa yanafadhiliwa na *NORAD* na mafunzo yenyewe yalikuwa yanaitwa ni mradi wa *SRCP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ulitusaidia sana hasa wananchi kwa ujumla. Wananchi walijua nadharia nzima ya uhifadhi, walijua faida zinazotokana na uhifadhi, vile vile walijua faida zote zinazotokana na mwekezaji. Hivi sasa mafunzo haya hayapo, sasa wananchi wanaishi pale, hawaruhusiwi kuwinda, wakilima mazao yao, tembo wanavamia wanakula. Hawaoni faida yoyote, hoteli ziko pale, lakini hazilipi chochote kwa Halmashauri. Matokeo yake wananchi waliopo pale wanakuwa na hasira. Hivi karibuni kwa mtazamo wangu, yatatokea mambo kama yanavyotokea kwenye machimbo, hawa watu wanaweza wakawavamia wawekezaji na kuwafanyia vurugu, jambo ambalo si la busara. Kwa hiyo, Wizara izingatie mafunzo, watu hawa wapewe mafunzo ili wajue faida zote zinazotokana na wale wanyama kuwepo pale Serengeti na wajue wao kwa nini wapo pale Serengeti, na wajue wale wawekezaji wanaipatia faida gani Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi na nitaunga mkono hoja kama nitapata taarifa kuhusiana na huu mgogoro wa Kijiji cha Pakinyigoti na pori la Ikolongo. Nakushukuru! *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Idara ya Wanyapori na Watendaji wote waliohusika kuandaa Muswada huu. Pamoja na pongezi hizi nina maoni yafuatayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau iwatangazie Wananchi ili wajue fursa mbalimbali zilizoko katika Muswada huu kwa lengo la kuwawezesha kimaarifa na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara iandae matangazo mbalimbali kama vipeperushi, vijarida kwa lengo la kuelimisha umma kuhusu dhamira ya Serikali yao na faida ya uwindaji itakavyosaidia wananchi wetu wakulima wa mbogamboga, matunda, wenye magari na wafugaji watakavyofaidika na uwindaji kwa wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kuleta Muswada mzuri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo ninayo machache ya kupendekeza ili Muswada huu uweze kuwa na manufaa kwa Wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 70 chote kifanyiwe marekebisho kwani kifungu hiki ni kibaya sana na kinadhalilisha utu wa Mtanzania kwa maana kwamba mnyamapori amepewa heshima na hadhi kubwa kuliko binadamu wa Kitanzania. Muswada huu unamlinda mnyamapori kuliko binadamu. Napendekeza Muswada useme wazi (*state categorically*) ni kiasi gani cha fedha kitalipwa kwa familia ya marehemu aliyeuawa na mnyamapori. Muswada uzingatie mchango wa mtu huyo kwa familia yake na jamii kwa ujumla. Hapa napendekeza malipo yawe kati ya Shilingi za Kitanzania milioni ishirini hadi milioni hamsini na zibadilike kutokana na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania. Pia Muswada uangalie wale wote wanaoumizwa na wanyamapori. Mfano mtu akikatwa mkono wa kulia anaoutumia kuandikia alipwe kiasi tofauti na yule aliyekatwa kidole. Pia kuna wale waliojeruhiwa na mamba kwa kuliwa sehemu zao za siri (wanaume), je, hawa wanastahili kulipwa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanyamapori kuharibu mazao. Muswada/Sheria iwafidie wakulima kwa bei ya soko kwa mazao yote yaliyoharibiwa na wanyamapori hata kama ni ekari mia moja au zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 17(4) na 17(1) adhabu inayopendekezwa hapa ni kubwa sana hasa kwa kuzingatia kuwa ng'ombe mmoja akiingia kwenye hifadhi pia adhabu ni ileile na kifungo cha miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kifungo kisizidi mwaka mmoja na faini iwe kati ya Sh. 100,000/= hadi Sh. 200,000/=. Kifungu 17(1) sheria iangalie wananchi wanaopenda kwenda kuchukua dawa za asili (za kienyeji).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napongeza na kuunga mkono Muswada huu.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Kilwa kuna pori la uhifadhi wa wanyamapori liitwalo Selous ambalo limetambaa hadi Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pori hilo lipo katika sehemu ya Kijiji cha Miguruwe, ndani yake kuna kitalu kimoja hivi ambacho kinamilikiwa na mtu mmoja. Kitalu hicho kinaleta mgogoro sana ndani ya kijiji. Wananchi hugombana na mhifadhi huyo kutokana na vitendo vyake, kimojawapo ni cha kuchoma moto ovyo, hivyo kusababisha madhara kwa raia na vilevile kujiongezea maeneo. Ningeomba Wizara iende ikalione tatizo hilo kama bado lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kifungu cha 91 cha Muswada huu kutaundwa Bodi ya Udhamini (*Trustee Board*) ambayo moja ya kazi zake ukiangalia kifungu 91(5)(a) ni kuwekeana mikataba (*contract*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kawaida katika taasisi nyingi huwa Bodi ya Udhamini huwa ni Bodi inayodhamini na huwa ni chombo ambacho kinasubiri matatizo yatakayojitokeza kwenye taasisi husika ili Bodi hiyo itatuwe. Pia Bodi aina hizi huwa ndio washtakiwa wa mwisho katika taasisi husika. Sasa iweje Bodi hiyo ipewe jukumu la kuwekeana mikataba wakati wao ndio wadhamini wa taasisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 13(1)(2) kinampa uwezo Rais kuanzisha ardhi oevu maeneo tengefu na kadhalika baada ya kutangazwa katika gazeti rasmi la Serikali na kifungu 24(1) Waziri wa Maliasili na Utalii baada ya kutangazwa katika gazeti rasmi la Serikali anao uwezo na kutangaza mnyama wa Taifa ambaye hatopaswa kuwindwa, kuuliwa, kukamatwa na kadhalika, je, uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa (*National Park*) uko kwa nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine Muswada huu pia una lengo la kukuza mapato katika tasnia hii ya wanyamapori. Ili mapato yawe na tija ni lazima pia matumizi yadhibitiwe. Fedha nyingi zinatumika katika kujenga na kukarabati barabara kwenye Hifadhi za Taifa kwa kiwango cha kifusi ambapo barabara hizo zinaharibika kutokana na ufundi hafifu. Kwa hiyo, umefika wakati sasa barabara zilizoko kwenye Hifadhi ya Taifa hasa zile barabara kuu zijengwe kwa lami kama vile ilivyo Hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria karibu zote katika nchi yetu zinamchukulia mwananchi anayeshukiwa hana kosa mpaka pale Mahakama itapothibitishwa kuwa amekosa. Sasa ilikuwaje katika Muswada huu kifungu 99(1) kikamtaka mwananchi kuwa ni juu yake kuthibitisha kuwa si mkosa baada ya kuwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Muswada huu pia huwafanya Watanzania washiriki kikamilifu katika tasnia ya uwindaji wa kitalu. Naomba nitahadharishe kama watu wenye uzoefu, umaarufu na fedha wanapewa miaka miwili ya kutafuta soko la watalii, wawindaji basi hawa Watanzania wapewe muda mrefu zaidi wa kuweza kujitangaza na hasa ukitilia maanani tasnia hii ina na mzozo baada ya Serikali kushindwa kuvigawa upya vitalu vya uwindaji mwaka 2007.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuwasilisha Muswada huu wenye lengo la kuhifadhi rasilimali hii adimu ulimwenguni kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusisitiza mambo machache ambayo ni muhimu sana katika kudumisha amani baina ya viongozi wa Hifadhi za Wanyamapori na wanavijiji katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yanayotakiwa kufanyika katika kudumisha amani ni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, uwepo utaratibu wa mikutano ya ujirani mwema kila baada ya miezi mitatu baina ya vijiji (uongozi) na uongozi wa Hifadhi ili kudumisha mahusiano mema kwa kero zinazojitokeza baina ya pande hizi baada ya muda kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Askari wanaosimamia ulinzi katika mipaka wanafanya ukatili mkubwa sana wa unyanyasaji wanapowakamata wanavijiji wanapokosea na kuingia katika maeneo ya hifadhi. Namuomba Mheshimiwa Waziri auelekeze uongozi wa Hifadhi za Wanyamapori, Askari wa Hifadhi wawe na ubinadamu katika kuwashughulikia wakosaji kwa kuwa wanavijiji na wanahifadhi wote wanategemeana katika kulinda utajiri uliomo katika hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mipaka baina ya Hifadhi na vijiji jirani iwekwe wazi zaidi kwa kupanda miti maalum katika mstari kuzunguka maeneo ya hifadhi ili kuondoa kisingizio cha wanavijiji kuwa mipaka ya hifadhi haionekani vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kumweleza Mheshimiwa Waziri kuwa, tatizo la mpaka baina ya Hifadhi ya Mikumi na vijiji katika Kata za Mikumi, Kidodi na Ruhembe bado halijamalizika kutokana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kuchelewa kurekebisha mpaka kwa kuzingatia maelekezo yaliyomo katika G.N. husika ya 1975.  La sivyo misuguano baina ya uongozi/askari wa Mikumi *National Park* na wananchi haitakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kumhamasisha Waziri wa Ardhi kukamilisha upimaji sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu kuhusu maliasili ya nchi yetu kwa faida ya wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana shaka kila mmoja wetu anapaswa kuelewa umuhimu wa hifadhi endelevu kwa wanyama wetu ambao Mwenyezi Mungu amewaumba kwa faida yetu sisi wanadamu, ndiyo maana tunaunda sheria mbalimbali. Ifahamike kwamba sheria zote zipo kwa ajili ya binadamu na siyo kwamba binadamu yupo kwa ajili ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini sheria hii itakuwa na inapaswa kuwa ufumbuzi wa upungufu uliowahi kuwepo hususan migogoro kati ya mamlaka husika na wanyamapori kwa upande mmoja dhidi ya mwananchi jirani au anayepakana na wanyama au hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia Muswada huu, sehemu ya II (*PART II*) kifungu cha (5) karibu chote kinazungumzia madhumuni/malengo (*objectives*), kifungu hiki cha 5(g) – (k) kinazungumzia ushiriki wa wananchi wa maeneo husika kwamba ni lazima washirikishwe kwa sababu wanyamapori pia ni mali ya wananchi kama sehemu ya Taifa na hivyo ulinzi wa wanyamapori ni wajibu wao wa msingi wakiwa jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa kusisitiza kwamba katika kutatua migogoro na katika mipango ya maendeleo inayohusisha maliasili hizi (wanyamapori) wananchi wahusishwe katika majadiliano na mapendekezo yote yanayofanywa. Hii iwe ni pamoja na kutoa elimu na ufahamu kwa jumla. Uzoefu unaonyesha kwamba upanuzi wa Hifadhi ya Ziwa Manyara haukushirikisha wananchi wa Vijiji vya Mayoka na Magara ndiyo maana kumejitokeza malumbano na kitu kilichoonekana kuwa mgogoro, tuepuke yote haya.

Mheshimiwa Mweny ekiti, wakati Muswada huu unaendelea bado ufumbuzi wa mgogoro wa Tarangire *National Park* na wananchi wa Vijiji vya Ayamango, Gedamar na Gijedabung haujapatikana. Kaya 245 wameachwa hawana chakula na makazi salama kwa miaka mitatu sasa. Mtazamo wa wananchi ni kwamba wamepuuzwa lakini wanyama wamepewa nafasi ya juu zaidi. Mpaka sasa wanyama wale wanaendelea kufurahia maisha lakini mwanadamu ambaye wanyama wameumbwa kwa ajili yake anateseka, hana chakula (amezuiwa na binadamu mwenzake) hana pa kulala kwani analazimishwa kuondoka katika mazingira magumu. Naomba leo hii Waziri awasaidie wananchi wale kwa kuwapa ruksa ya kuendelea kulima ili kujipatia chakula msimu huu wakati Serikali inaendelea na mambo mengine ya kuwahamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kuona ushiriki wa wananchi katika mgogoro huu uliowakuta pamoja na kuishi zaidi ya miaka 30 (thelathini) kwa amani na hifadhi ya Tarangire. Hata kama kumetokea hitilafu katika mipaka Serikali imehusika sana pamoja na TANAPA wenyewe. Naomba mazungumzo ya haraka yafanyike kwa kila hatua na wananchi wawe pia sehemu ya ufumbuzi wa tatizo hili, Kifungu 5(1) (k).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 13(1) kinaeleza kwamba Mheshimiwa Rais kwa mashauriano na '*local authorities*' wanaohusika, atatangaza eneo lolote la Tanzania kuwa '*Game Reserve'*. Naomba au kushauri kwamba Halmashauri hususan Madiwani watajwe na wahusike maana ndiyo wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nane (*PART III*) migogoro ya binadamu wanyama, kifungu 70 (2), Serikali iwe na uso wa kibinadamu katika kusaidia walioathiriwa na wanyama. Inaonekana Serikali inajificha kwenye kifuta machozi badala ya fidia!  Muswada uje na ufumbuzi wa maana utakaojali pia haki ya msingi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naunga mkono Muswada huu.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya fidia kwa uharibifu wa mali, kujeruhi au kuua binadamu. Katika sheria hii sijaona ni nani hasa anawajibika kuokoa maisha na mali za wananchi kwa kuzuia au kufukuza uvamizi wa wanyama katika makazi ya binadamu. Ufafanuzi wa *authorized officer* nini hasa? Katika Wilaya, Afisa Wanyamapori humtupia mpira *Game Reserves Officer*. Hata hivyo wilaya zinalalamika kukosa magari ya kupambana na wanyama, hawana askari wa kutosha, kwa upande mwingine kwa maana ya *Game Reserves* magari ya kutosha na askari wa kutosha, ni kielelezo tosha Serikali inawajali wanyama zaidi.

Kifungu 12 kipengele cha 3(a) na (b), 4 na 5, sheria inampa mamlaka Afisa wa Wanyamapori kutumia silaha ya moto kwa mtuhumiwa anayeweza kujaribu kukwepa au kuzuia kukamatwa. Sheria haijasema silaha hiyo ya moto itatumika kutishia au kupiga sehemu gani ya mwili au kuua, kwa kosa la aina gani? Akiwa amekutwa na silaha au hata anachunga au ameingia kwa bahati mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *commits an offences*. Sheria hii lazima iwe *clear* katika suala hili vinginevyo watu watamalizwa kuuawa, mipaka ya uhifadhi na shughuli za kiuchumi na kijamii zimetenganishwa tuta, hii sheria tunatunga ikatumike wapi au Serikali imeamua na kudhamiria watu wake kuuawa kwa risasi, Waziri na Naibu Waziri msijifanye kwamba hamzijui jamii zinazoishi mpakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 17(2) kinakataza kabisa kuchunga ndani ya *Game Reserve*, Kifungu cha 20 kinakataza kabisa kuchunga ndani ya *game controlled area* isipokuwa kwa idhini ya Mkurugenzi. Sheria haijasema chochote kwa wananchi wanaoishi kandokando ya *Game Reserves*. Je, hatma ya wananchi hao ni nini inapotokea ukame?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria haijatoa suluhisho la kudumu katika upatikanaji wa malisho kwa wafugaji waishio kandokando, sheria imekaa kimya, tumetunga sheria leo ambapo wananchi wapo pale wanaishi sambamba na uhifadhi, kwa sheria zetu hizi wananchi hawawezi kuwa *happy* na mhifadhi na migogoro haiwezi kwisha. Kama ilivyo katika kifungu cha 44 ambacho kimempa Waziri uwezo wa kutenga maeneo ya kuwinda kiraia, hivyo hivyo sheria hii inatakiwa kumpa uwezo Waziri wa kutenga maeneo *buffer zones* ambazo zitatumika kwa malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 17(4), adhabu ya miaka mitano kwa mfugaji wa ndani inafanana na wa *foreign,* hata ya yule aliyechoma moto, bora ingekuwa miaka miwili mpaka mitatu. Adhabu ya milioni tano ni kubwa sana, hii ni adhabu kubwa kuliko zote lakini katika Muswada huu aliyechoma msitu shilingi mia tano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii katika Kifungu 17(2) neno *livestock* limetafsiriwa kwa maana nyingine, hata mbuzi mmoja milioni tano, sheria haijampa haki kabisa mfugaji, Wabunge wenzangu tukataeni Muswada huu, hakuna *timeframe* ya kibali cha kuchangia toka siku ya kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kifungu kinachompa uwezo Afisa wa Wanyamapori kuendesha mafunzo ya uhifadhi pamoja na sheria mpya kwa wananchi waishio kandokando kupitia Serikali zao za vijiji na mikutano ya hadhara ili kuwapa ufahamu wa kutosha juu ya uhifadhi na sheria zinazotusubiri kuhukumu kabla ya kuelimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naukataa Muswada.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Wizara ishirikishe jamii zinazoishi katika maeneo jirani na hifadhi husika washirikishwe katika ulinzi wa wanyamapori na pia jamii hizi zinufaike na mapato yatokanayo na wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *WMAs* yasukumwe ili ziuzwe kwani ndiyo '*future'* ya *wildlife conservation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ramani ya *ecosystems* zilizo muhimu kwa uhifadhi wa wanyamapori zibainishwe na zitunzwe ili kilimo na makazi holela zisiruhusiwe kuharibu hizi *ecosystems* muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia iwekwe wazi na iwe *appropriate proportional* na *timely,* Wizara ihakikishe kuwa fedha ya fidia inaoana na hasara iliyosababishwa.

**PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi kwa kutambua lazima rasilimali na zawadi kubwa tuliyopata kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa kuanzishwa sheria hii ya mwaka 1974 ni ishara tosha kuwa Serikali yetu imezinduka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 21 kuhusu ulinzi, nashauri kuwa askari wa wanyamapori waliopo sasa wapatiwe motisha ya kutosha hasa mishahara yao irekebishwe. Ahadi ya nyongeza ya mishahara yao kwa asilimia 40% itekelezwe na kama ahadi haikutolewa iwekwe bayana ili kuepusha manung'uniko na kuwavunja moyo. Itengwe asilimia fulani kutoka mfuko wa hifadhi wanyamapori kwa lengo la kuboresha vitendea kazi kwa Askari wa wanyamapori, ujenzi wa makazi, huduma za afya, ununuzi wa magari, elimu na maslahi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha (9), uanzishwaji kikosi dhidi ya ujangili, ushauri, katika maeneo yanayopakana na hifadhi ya wanyamapori, wananchi washirikishwe katika uanzishwaji wa kikosi dhidi ya ujangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida yake ni kwamba, wananchi wanafahamu maficho na mbinu za majangili, hivyo wakishirikishwa kwanza itapunguzia gharama kwa kuwaajiri maaskari kutoka nje ya maeneo hayo, katika wilaya zinazopakana na hifadhi ya wanyamapori, wako wanajeshi wastaafu, polisi wastaafu, vijana waliopitia mafunzo ya

JKT na mgambo, hivyo wanatosha kabisa kuanzisha kikosi hicho na watafaidika kwa sababu watapata ajira na kuinua uchumi wa wanakijiji waishio katika maeneo ya wanyamapori yaliyohifadhiwa (*buffer zone*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria iwe na kanuni ambayo itawawezesha wananchi wafaidike na nyama ya wanyamapori kwa kuanzisha mabucha katika sehemu mbalimbali ya kuuza nyama ya wanyamapori ili kujenga afya ya wananchi. Hakuna faida wananchi wa Mikoa inayopakana na hifadhi ya wanyamapori hasa wanaoishi katika maeneo ya wanyamapori yaliyohifadhiwa (*buffer zone*) wasipate kitoweo kitokanacho na nyama ya wanyamapori. Utaratibu huu utekelezwe kutokana na msimu ambapo idadi ya wanyamapori inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Muswada na hongera.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpa pole Mheshimiwa Mwangunga kwa huu Muswada mrefu unaojadiliwa kwa siku tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hicho Kifungu cha mwanadamu kuuawa fidia yake itamkwe ni kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kifungu cha kuwapiga risasi watu wanaopita kwenye eneo la uhifadhi kifutwe, watu wasio na hatia watauawa bure.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga; Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige; Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Muswada huu wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori wa Mwaka 2008.

Natumaini kuwa ushauri nitakaotoa utafanyiwa kazi pamoja na maoni mbalimbali ya Wabunge waliochangia kwa niaba ya wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kifuta jasho cha Uharibifu wa Mazao na Wanyamapori. Pamoja na pongezi nilizozitoa hapo juu, napenda kutoa maoni yangu kama ifuatavyo: Ni mara nyingi wananchi wamepata hasara ya mazao yao kuharibiwa na wanyamapori. Nasikitika sheria inasema itatoa kifuta jasho hekta tano tu bila kujali mazao yaliyoharibiwa yalikuwa ni ya ukubwa wa shamba la hekta ngapi au shamba lilikuwa na mazao yenye gharama gani. Huenda shamba lilikuwa la hekta 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Muswada huu utazamwe upya, kinachotolewa kwa mwenye shamba isiwe ni kifuta jasho bali iwe ni fidia ya gharama ya mazao yaliyoharibiwa na ilingane na gharama yake. Kwa Serikali kutoa kifuta kijasho itakuwa ni kutowatendea wananchi haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kifuta machozi kwa ajili ya marehemu aliyeuawa na wanyamapori au kujeruhiwa na wanyama. Bado naendelea kutokubaliana

na Serikali juu ya kifuta machozi kinachotolewa kwa ndugu wa marehemu aliyeuawa na wanyamapori kwa sababu binadamu aliyefariki mara nyingi huwa ni tegemeo la familia katika kuzalisha kipato cha familia. Hivyo basi, naiomba Serikali katika Sheria hii itoe neno kifuta machozi iwe fidia kwa marehemu. Serikali itakapogharamia fedha nyingi kumfidia marehemu itakuwa makini kuhakikisha wanyamapori wanadhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu muda maalum wa kutoa kifuta jasho au kifuta machozi. Pamoja na kuishauri Serikali kutoa fidia, napenda kuishauri sana Serikali kuweka muda maalum wa kutoa kifuta jasho na kifuta machozi. Nashauri suala hili kwa vile utaratibu wa kutoa huchukua muda mrefu sana wakati mwingine ndugu hukata tamaa kufuatilia kifuta machozi cha marehemu ndugu yao aliyeuawa na wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nimalizie kwa kuunga mkono Muswada huu nikiwa na mategemeo kuwa mchango wangu utapatiwa majibu mazuri.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inapendekeza usimamizi wa mapori ya akiba uwe chini ya Mkurugenzi wa Wanyamapori. Je, *role* ya Halmashauri za Wilaya yalipo mapori haya ya akiba itakuwa ni nini kimamlaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikosi dhidi ya ujangili, *KDU*, vilivyoko hivi sasa vimeshindwa vipi kazi mpaka kianzishwe kikosi kingine kinachohitaji idhini ya Rais? Kikosi hiki kitaruhusiwa kubeba silaha na hata kutumia silaha inapobidi. Kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi jinsi wanavyoteswa na wafanyakazi wa vikosi vya sasa kwa kupigwa na kunyanyaswa. Je, hawa wapya *(kikosi)*, watakapoanza kazi si watakuwa wanaua mara kwa mara kwa visingizio vya kudhibiti ujangili? *Cases* za *mistaken identity* kati ya majangili na raia wema zitaongezeka. Wizara imejipanga vipi? Vikosi vipya visije kufanya kazi ya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna tafsiri kamili ya *Nyara za Serikali*. Wananchi wengi wameumia kwa kubambikizwa kesi za nyara mbalimbali bila kujali ni nyara zipi na ni za muda gani. Kwa mfano, yule raia wa Muhanga, Itigi, aliyekamatwa na gamba la ngozi ya kiboko. Alilipata wakati wananchi wameruhusiwa kupata kitoweo. Alipohifadhi gamba hilo nyumbani kwake walikuja watumishi wa Idara ya Wanyamapori wakamkamata na kuishia kwenye vyombo vya sheria na baadaye alipokuwa chini ya ulinzi, walikuja Polisi wakatwaa mifugo yake hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono juu ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mapori ya Akiba, ikizingatiwa kuwa kuna *National Parks 15* na *Game Reserves 17. Part I, Section 5*, haifafanui vyema kuhusu mmiliki wa wanyama wanaokutwa wamekufa au kukaribia kufa. Hata kukiwa na kijiji jirani pale, wananchi hawaruhisiwi kujipatia kitoweo. Vilevile wananchi bado wanashindwa kumudu ada za uwindaji, zirekebishwe na pia *issue* ya kifuta machozi bado ni mbichi kabisa.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri, Mheshimiwa Mwangunga na Naibu wake kwa maandalizi mazuri

ya Muswada, hasa baada ya kuzingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na yale ya Kamati ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi naunga mkono hoja isipokuwa yapo mambo yanahitaji kufanyiwa marekebisho na msisitizo. Mwelekeo katika Muswada huu unampa thamani zaidi mnyama kuliko mwananchi, jambo ambalo kinyume na maadili yetu. Haiwezekani Muswada useme mwananchi akiua mnyama apigwe risasi, lakini mwananchi akiuawa na mnyama Muswada haupo wazi bali unakaribisha mjadala. Hii ni mbaya sana. Hili ni lazima lirekebishwe, vinginevyo sitauunga mkono Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia kwa vifo vya wananchi sasa liondolewe bali familia ya marehemu ilipwe fedha za kutosha ambazo sio chini ya milioni kumi. Aidha, mashamba yanayoharibiwa na wanyamapori, mazao yaliyokuwemo yathaminiwe na ndipo mwananchi alipwe kulingana na thamani ya hasara aliyoipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka inayoonesha *Game Reserves* na Hifadhi ya Misitu iwekwe bayana ili kuondoa matatizo yanayojitokeza sasa ya wananchi kusumbuliwa kuwa wameingia katika hifadhi ya misitu, wakati mipaka haieleweki ama haikubainishwa. Aidha, watumishi waongezwe hasa Askari wanyamapori, ikiwezekana kila Tarafa zenye hifadhi ya misitu na *Game Reserves* ziwe na Askari wanyamapori. Kwani uzoefu uliopatikana Singida, Tarafa ya Ikungi, walipouawa wananchi 13 kwa kuwa Askari hao hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri sana katika Mazingira na Maliasili kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, natoa shukrani za dhati kwa mamlaka ya Hifadhi Wanyamapori (*TANAPA*), kwa mchango wao mkubwa kuendeleza elimu yetu kwa kuchangia ujenzi wa Sekondari ya Karambi, bila *TANAPA* Sekondari hii ambayo mwaka jana imetoa vijana wa Kidatu cha nne, isingekuwepo. Tunaishukuru Serikali na *TANAPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kutafakari kwa makini michango ya Waheshimiwa Wabunge na kuchukua ushauri wa Wabunge kwani unaletwa kwa niaba ya wananchi. Serikali yetu ni sikivu sina shaka katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga Mkono hoja.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana kuletwa Muswada huu na ninaunga Mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya ya Kasulu Vijiji vya Kagera, Nkanda, Mugombe, Nyakitonto na Muvinza, Wanalalamika kuwa Askari wa

Wanyamapori, wanawanyanyasa sana na kuwatoza pesa wanapokewenda mashambani kwa madai kwamba wamepita kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 0/02/2009 wananchi wa Kagera, Nkanda na Nyakimtonto wamenipigia simu kuomba nikaeleze hili ili uweze kuwasaidia. Naomba sana wananchi hao wasisumbuliwe ili waweze kuhudumia mashamba yao kwa ajili ya kujipatia chakula na mahitaji mengine. Msimu huu wa Kilimo si wakati wa kuwabugudhi wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga na Naibu wake. Napenda kuwapongeza kwa hatua mbalimbali, pia napenda kuwapa pole kwa msukosuko mdogo wa hivi karibuni kuhusu hoja binafsi ya kufuta kibali ya Mheshimiwa Dokta Mzindakaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muichukulie hiyo ni haki ya Bunge kuamua tofauti kadri ya mawazo ya wengi na busara, wote tuna nia ya kujenga nchi na sio kubomoa. Naamini hiyo haitawakatisha tamaa na badala yake ni sehemu ya kujifunza, kwani: "*Every no is a start of yes,* " *The words of potential entrepreneurs.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 12 (3) (a) naona ni leseni, kinamhukumu mtu *instantly.* Hivi kwenye Sheria za Wanyamapori hakuna suala la mtu kujitetea mbele ya Mahakama? Huyo mtu anayekimbia atakuwa na silaha? Kama wanaoua *Albino* wanatetewa vipi huyo anayekimbia tu? Naomba majibu kwani kuna mtu pia wa maeneo ya uwindaji alinipigia simu akilalamikia kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** suala la mtoto Faraja Rose aliyetunzwa na nyani limefikia vipi juu ya matunzo ya mtoto huyo? Kwa kuwa Askari aliyemtoa kwa mama yake hakutumia busara zote, yawezekana kwa ajili ya uelewa mdogo juu ya mama nyani huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara yako kuchukua jukumu la kumtunza mtoto huyo kwa kutenga kiasi cha pesa kila mwaka ili asome ikiwa ni sehemu ya fidia ya kifo cha mama yake (mzazi au mlezi) ambaye ni nyani. Naomba pia majibu juu ya suala hili (nyani wa Bukoba).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu wa kusema humu Bungeni, jana tarehe 2 Februari, 2009, naona ni vyema nikaandike yale ambayo niliona si vyema kuyazungumza ili yaweze kufanyiwa kazi kwa unyeti wake.

Kwanza, mtoto huyo afanyiwe pia *research* ya kisayansi kama vile *DNA* ili kujua ni mtu kamili au na nyani ana mchango wake.

Pili, kuona *immunity* yake na kama inaweza kusaidia tafiti za kinga kwa binadamu na kadhalika, kwani kitendo cha kukaa porini kwa muda mrefu akiwa hana nguo na kuumwa na wadudu wa aina mbalimbali bila kuathirika, inaleta hoja ya msingi.

Tatu, kwa kuwa wenzetu wa Kenya sasa hivi hawawezi kuongea bila kuzungumzia Rais wa Kwanza Mweusi wa Marekani, Barrack Obama kuwa ametoka Kenya ni pamoja na kutangaza fursa za kitalii; hivyo basi, nashauri yule mtu (askari) ambaye alimwona yule nyani, afanyiwe *interview* ya kina (maelezo) ya kutosha, yakihusisha pia eneo la tukio na Pori hilo la Bukombe, ili kuingiza katika kumbukumbu zetu za maajabu na utalii. Naamini huko baadaye hiyo itakuwa ni fursa tosha ya kuingiza kipato kwa taifa, kama ambavyo watalii hutembelea Olduvai Gorge, Mapango ya Amboni na kadhalika.

*I might be exaggerating, but I believe this can work.*

Pole kwa maelezo yangu marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja ya Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori wa mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuwa “proactive” katika kukokotoa hoja hii na kwa kuwashirikisha wadau wengi kuliko Miswada mingine ya Sheria iliyowahi kuletwa katika Bunge lako Tukufu kuhusu uhifadhi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki na umiliki wa moja kwa moja katika shughuli za uhifadhi utakaofanywa na wananchi utafanya uhifadhi wa wanyamapori nchini uwe endelevu na wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri Mheshimiwa Shamsa Mwangunga Naibu Waziri Ezekiel Maige, Katibu Mkuu na watalaam wote.

Kwa kuwa wawindaji wako karibu na wananchi na wananchi ndio wanaohifadhi wanyama ningeshauri, kabla ya sheria hii kutumika wapewe masharti ya kusaidia wananchi maendeleo yao ili kuondoa kero zao kama vile barabara, zahanati, mashule na kushirikiana na Halmashauri zilizopo kwenye eneo husika. Shirika la *TANAPA* limeonyesha kazi nzuri ya kuchangia maendeleo ya wananchi kwa kujenga shule, zahanati na pia kutoa asilimia, ni vema wote wakafanya kama wanavyofanya *TANAPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aangalie jinsi gani *TANAPA* watapewa upendeleo wa hifadhi nyingi zaidi kwani ni wazoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhifadhi wa *WMA,* kwa kuwa Wilaya ya Urambo imeonyesha uhifadhi wa wanyamapori na mazingira, ningeomba Serikali iangalie jinsi ya kuwawezesha hasa, kupewa misaada kama vile gari, Askari, pia wapewe mafunzo ili waweze kufanya vizuri.  Katika Kata ya Uyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari Wanyamapori wapewe vitendea kazi, waongezwe hususan kwenye hifadhi za Serengeti, Selous, Mikumi, kwani wako wachache na majangili wanaongezeka, waongezwe mishahara iwe mizuri ili wafanye kazi yao vizuri kwani kazi yao ni hatari ambayo inataka mtu ajitume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote wenye mahoteli katika eneo husika watoe michango yao kwa kulingana na mapato yao wakati wa kutoa asilimia kwenye maendeleo ili wanachi waone jinsi Serikali inavyowajali. Pia itasaidia kutoa mgongano baina ya wananchi na wawindaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ardhioevu, kwa kuwa Tabora kuna maeneo mengi yenye misitu na ardhioevu, Kijiji cha Mpandamlowoka, Urambo imeonekana ni sehemu yenye majangili  wengi na kuna sehemu ya uhifadhi na ardhioevu, ni vema Serikali ikaangalia mambo yafuatayo:-

- Miundo mbinu iboreshwe ili kukabiliana na ujangili huo.
- Askari wanyamapori wapelekwe maalum katika Kijiji hicho ili kuzuia ujangili huo na kulinda mazao ya wananchi yasiharibiwe na wanyama.

- Fidia kwa wafiwa na wale wanaoharibiwa  mazao yao ni ndogo na ni ya muda mrefu hivyo, iongezwe  kutokana na wakati uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAWIRI wapewe motisha ya kutoka kwenye Idara hii kwani wanafanya kazi katika hali ngumu na wengi hawaendi kuripoti na kama wakifika huondoka hasa Serengeti kutokana na mazingira yalivyo. Kuwepo na Zahanati za kutosha kwenye maeneo hayo ili familia zao zipate huduma ya kutosha. Kwa wakati huu tulionao ningeshauri wapelekewe *SOLAR* ili iwe ni kivutio wanapopata ajira.  Bajeti yao izingatie hali halisi ya maeneo waliyokuwepo kutokana na jiografia.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaelekea kuwa "*Concept ya Exclusivity*" haieleweki hasa kuhusiana na uhifadhi na faida zake. Inatakiwa  ielezwe kuwa mapato yanakuwa makubwa zaidi kuliko matumizi ya kawaida na ni maamuzi tu kuwa na utaratibu huo au hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mawazo kuwa tufute utaratibu (biashara) ya kuwinda bali tuhifadhi watu wanachanganya uhifadhi na kudhani ni *protection* wakati dhana hizi mbili zina maana tofauti.  Ukizingatia *protection* wanyama Watazaliana na ku-exceed *carrying capacity* ya maeneo yao na watateketea.  Kwa hiyo, badala ya kuwaacha wateketee, tunawinda ili ku-*regulate population* yao ili waendane na *carrying capacity"* ya maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mawazo yanayopendekeza kuwa wanyamapori ni bugudha kwa wananchi na kwamba hawaoni kuwa wana haki ya kuwepo kama sisi binadamu tulivyo na kwa kweli tuna tegemeana yaelekea kuna haja ya elimu kwa wananchi kuhusu hifadhi ya wanyamapori. Lakini la msingi ni kuzingatia *viability* ya hifadhi zetu ili tuone kama ni lazima tuendelee kuwa na hifadhi zote tulizonazo na kwa kuzingatia uwezo wetu kama Taifa na kama wananchi katika maeneo yao kuishi na wanyama hawa na kuwahifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Muswada huu tayari umepata dhoruba kutokana na hoja ya Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, kuna haja ya kufanya *Regulatory Impact Assessment* au *EIA* ili kutambua faida na athari ya Sheria tunayoiunda ili kujiandaa kwa yatakayojitokeza.

Athari moja iliyo wazi ni gharama ambazo Serikali itaingia kupitia *direct intervention* kwenye uhifadhi, kwenye vitalu na kupitia Mahakama, kwani bila shaka Mawakala na wenye vitalu, wanaweza kwenda Mahakamani; ni vyema kujua hayo yatakayotokea.

Athari nyingine kubwa ni kuvuruga biashara ya uwindaji, kupoteza heshima na hadhi ya nchi yetu kwenye mizania ya Kimataifa. Hivyo ni vyema kuandaa mapema, namna tutakavyojinasua kwenye vurugu na hali hiyo.

**MHE. MARIAM S. MFAKI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mwanasheria Mkuu, Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wa Kamati kwa kushughulikia Muswada huu mpaka umekamilika na leo umewasilishwa katika Bunge lako Tukufu, bila kuwasahau watendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii itakuwa ni nyenzo kubwa ya kulifanyia kazi suala zima la kuhifadhi Wanyama pori. Naomba nishauri Serikali kufanya uchambuzi wa ujenzi wa mahoteli unaoongezeka katika mapori ya hifadhi ili ikiwezekana baadaye wanyamapori au maeneo hayo yabaki kwa ajili yao.

Kwanza, naomba Seikali ijitahidi kukamilisha kutunga kanuni ambazo zitawasaidia kutumika mapema.

Pili, tuombe Serikali kukamilisha uundaji wa *Wildlife Authority* ambalo litasimamia maeneo husika.

Tatu, Serikali iongeze fedha kwa ajili ya kuwezesha uhifadhi huu kuwa endelevu na hasa kuboresha maslahi ya watumishi ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nipongeze Wizara kwa Muswada huu, japo yapo mambo madogo madogo muhimu sana ya kuzingatia ili Sheria hizi mpya za Wanyamapori ziweze kuwa *effective*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matangazo mengi yahusianayo na wanyamapori pamoja na binadamu hutokana na matatizo makuu matatu ambayo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, shughuli za maisha ya binadamu za kila siku.

Pili, matatizo makubwa ya migogoro ya ardhi kati ya vijiji vinavyozunguka *game reserve areas*.

Tatu, uhaba wa mafunzo juu ya uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika namba 1 hapo juu moja ya shughuli kubwa ya binadamu ni kilimo. Wananchi waishio jirani na maeneo ya wanyamapori wamekuwa wakikumbwa na tatizo kubwa la njaa. Sasa iwapo sheria haitaji kiwango muhimu ambacho mtu atalipwa kama fidia ni dhahiri kwamba Muswada huu utaendeleza kilio hicho kikubwa kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya mipaka pia ni tatizo kubwa sana ambalo kama Wizara haitalipa umuhimu wa kulitauta haraka basi laweza kuleta upotevu wa amani kati ya wananchi, wawekezaji na hata wanyama kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mfano wa tatizo la mpaka lililopo katika Kijiji cha Park – Nyigoli na pori la Ikorongo (Serengeti) ambalo mpaka huo umekuwa ukisababisha kutokuelewana mara kwa mara kati ya wanakijiji na mwekezaji na hivyo kupelekea ukosefu wa amani na kwa kuangalia Muswada huu ni dhahiri kuwa watu wengi watapoteza maisha au kufungwa kwani kwa sasa wananchi huingia kwenye pori hilo kwa kutojali mpaka uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipendekeze kuwa Wizara iunde utaratibu wa kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ya wanyama pori. Lengo ni vizuri wananchi hawa wakaelewa vizuri dhana nzima ya uhifadhi kwani katika eneo langu la Serengeti amani imeanza kupotea kwa vile wananchi wanahisi kama wananyanyasika katika ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwapatia mafunzo hayo ya uhifadhi, hatari inayoonekana kuwapata wananchi kwa labda kufungwa au hata kupoteza maisha kutokana na sheria hizi mpya itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha huku nikimwomba Waziri anieleze ni lini suluhu ya mpaka kati ya Kijiji cha Park-Nyigori na pori la Ikorongo itapatikana ili kuwanusuru wananchi kuguswa mara kwa mara na sheria hizi mpya zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia Mheshimiwa Waziri majibu mema na Mungu akupe nguvu na hekima ya kujibu yote.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza sana wewe, Naibu Waziri, Watendaji wa Wizara na Idara zote za Maliasili, kwa kazi nzuri mnazofanya, pamoja na matatizo mengi yanayowakabili hasa wakati huu.

Mheshimiwa Waziri, umefika wakati sasa wa kuijenga upya Idara hii ya Wanyamapori, ambayo huko nyuma ilikuwa inatoa mchango mzuri sana kwenye Pato la Taifa, lakini sasa hivi imerudi nyuma. Sababu kubwa zinazofanya Idara hii irudi nyuma ni kutokuwa na watumishi wa kutosha, kwenye mapori yote yaliyopo hapa nchini (Mapori ya Taifa na Mapori yote yaliyopo chini ya Halimashauri za Wilaya); vikosi vya kuzuia ujangili kukosa vitendea kazi; na vikosi hivyo kujenga maeneo ya mijini ambako ni mbali na maeneo wanayotakiwa kuyalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni uundwaji wa Bodi za *TWPF*, Ngorongoro na *TANAPA.* Bodi hizi zimekuwa zinaundwa kisiasa, badala ya kuwaweka Wajumbe wa Bodi wenye taaluma ya Uhifadhi, wengi wanaowekwa ni watu wasio na taaluma hii, kwa hiyo, maamuzi yana kuwa si ya kitaalam. Nashauri mtindo huu, uachwe mara moja ili kuokoa uhifadhi hapa nchini.

Mheshimiwa Waziri, vijana wanaoajiriwa kuwa *Game Scouts*, wawe wale wenye elimu ya Pasiansi na wawe wale wanaotoka kwenye maeneo yenye wanyamapori. Tuache kuajiri watoto wetu, ambao hawana sifa na hawana uvumilivu wa kukaa maporini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumie mabwana nyama wastaafu, ambao bado wana mapenzi na uhifadhi, wawasaidie kwenye kuendeleza na kutunza wanyamapori na maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi wa Idara hii na Idara nyingine za maliasili waache ubinafsi, ubabaishaji, chuki zisizo na msingi, bali watumie taaluma zo kulinda maliasili zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Watumishi wa Idara ya Wanyamapori, wanafanya biashara za uwindaji na kadhalika na hao ndio wanaofanya kazi ya Idara isiendelee kwa manufaa yao, wakisaidiana na wawindaji wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuandika kwamba, bila kuimarisha Ofisi zetu za Wilayani, uhifadhi utaendelea kwisha kama ambavyo wanyama wanavyotoweka kwenye maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakikisha Pori la Yaeda Chini linakombolewa na kuwa kimbilio la wanyama toka Manyara na Ngorongoro. Corridor ya Ngorongoro Yaeda Chini ifunguliwe na Corridor ya Yaeda Chini Manyara kupitia Pori la Marangi ifunguliwe.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono Muswada huu. Tatizo lililopo ndani ya Muswada huu ni pamoja na kuwa na

upungufu upande wa fidia, mara wananchi wanapodhurika na wanyamapori hawa. Naishauri Serikali iangalie upya Sheria hii inayozungumzia maamuzi ya Waziri kufikiria, badala ya sheria kuweka moja kwa moja. Sheria irekebishwe, badala ya Waziri kufikiria fidia, Muswada utamke wazi fidia kisheria ya binadamu na mazao.

La pili, wananchi wanaoishi jirani na wanyama hawa, hawana elimu thabiti waishi vipi na wanyama hao. Kwa mfano, mipaka yao na wanyama hao, aina ya wanyama wanaotamkwa kuwa wakali katika sheria, wafanye nini kujihami, kwa sababu wapo karibu na wanyama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Moja, kifungu cha 115(1) mpaka (6 ni kifungu hatari sana:-

(a) Kinatoa mamlaka makubwa sana kwa *Director,* kutamka mtu mwenye makosa kulipwa faini na Mkurugenzi bila kumfikisha Mahakamani, kiasi kisichopungua shilingi 200,000 hadi 10,000,000. Hii ni hatari sana, hasa kwa kuzingatia uelewa wa wananchi wetu, ambao wakibanwa tu wanaweza kukubali kukiri kosa kwa maandishi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili litaalika sana rushwa. Nashauri Waziri akubali kurekebisha ili faini zilipwe Mahakamani tu au basi ikiwa lazima kuwe na *fixed sum* badala ya kuacha kwa *discretion* ya *Director*.

(c) Hata sasa Wilaya ya Karatu tumeathirika sana, kwani watu walipigwa faini tena bila risiti.

Pili, kifungu cha 105(4) kinapingana na Sheria ya Mwenendo wa Jinai, ambacho mtu anakamatwa tu baada ya uchunguzi kukamilika. Naamini ni muhimu kuwa na *consistence* katika sheria zetu. Marekebisho hayo tumeyafanya, hata mwaka haujapita tumerudi pale pale. Ni jambo la hatari, sheria zinapoanza kubagua na isitoshe tunajua kabisa nchi yetu bado ina kesi nyingi za kubambikizwa. Kifungu hiki kitawafanya watu wengi wakamatwe, kwa sababu tu wanakosana na *wardens*. Karatu tumepata adha kubwa kwenye eneo hili kwa upande wa *TANAPA* na *NCAA.*

Tatu, kifungu cha 102, *presumption,* ni jambo baya sana katika sheria. Isistoshe mtu akikamatwa kwa kosa la silaha inayohusishwa na uhalifu hata dhamana ni ngumu. Siamini ni jambo jema sheria inayotungwa 2009 izungumzie *presumption* wakati sheria zetu zinazumgumzia *beyond reasonable doubt*. Kwa maana nyingine, mtu akibambikiziwa ataozea *lockup* na baada ya muda mrefu anaachiwa, kwa kukosekana *beyond reasonable doubt*, isitoshe hawezi hata kudai fidia.

Ninaamini Waziri atatafakari hoja hizi na kuzifanyia kazi, kwa kurekebisha maeneo husika, kabla Watanzania wema hawajaathirika. Tutafute namna nzuri ya kuwashughulikia wahalifu.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kuleta Muswada huu muhimu, ambao malengo yake ni pamoja na kuifanya Sekta ya Maliasili na Utalii kuwa endelevu zaidi na kuifanya iweze kuchangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa. Naunga mkono hoja hii kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, nashauri Wizara ifanye utafiti wa kutuwezesha Wilaya ya Lushoto hususan Milima ya Usambara, kunufaika na utalii wa kuzunguka milima kwa magari na kwa miguu. Hili likifanyika litasaida kuvutia watalii, baada ya kuona mbuga za wanyama. Nchi ya Shelisheli *(Seychelles)*, inapata mapato mengi kutokana na utalii wa kuzunguka milima kwa magari *(JEEP)*.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa Muswada huu. Naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Hoja yangu hapa ni juu ya uhai wa Wanyama na Uhai wa Wananchi, wanaoishi katika maeneo husika. Kwenye jimbo langu katika Kata ya Luduga, Wilaya Njombe na pia Kata ya Wangama, Wilaya Njombe, wananchi wangu wanaishi kwa wasiwasi na mateso makubwa, juu ya kuongeza mipaka ya Kifadhi ya *Kipengere Mpanga Game Reserves*. Mikapa ya zamani haina matatizo. Naomba kauli ya Serikali juu ya tatizo hili; ni lini ufumbuzi wa kudumu utafanyika?

Vijiji vinavyoathirika na kuongeza mipaka ni Kata ya Luduga, Mambegu, Luduga, Mpango Mpya, Malangali, Imalilo na Hifadhi ya Kipengere Milimani

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwa vile wananchi tayari walishahamishwa hasa wa Vijiji vya Mpanga Mpya, Mambegu, Luduga, Mlangali na Iwahilo, wananchi hao wanaishauri Serikali itumie ile mipaka ya zamani na ikibidi zoezi hili lishirikishe Mbunge husika na Madiwani wa Kata za Ludiga na Wangama. Mimi binafsi kama Mbunge, sijashirikishwa kabisa na zoezi hili la mipaka mipya.

Kama Serikali itashindwa kukubali ushauri wa wananchi na sisi wawakilishi, basi wananchi wataendelea kuteseka na kuishi kwa wasiwasi na kupelekea kutoshiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi hii.

Pia kunaa Benki ya COCOBA imeanzishwa kwa ajili ya vijiji vilivyopo maeneo ya Hifadhi ya *Kipengere Mpanga Game Reserve*, kwani uchumi wao ulitegemea sana mkaa na asali. Kuanzisha benki hii, inaweza kuwa nafuu kwa uchumi wa maeneo husika.

Suala la fidia kwa wahusika bado ni tatizo, walilipwa kidogo sana na wengine hawakupata kabisa.

**MHE. LUDOVICK J. MWANAZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umekuja kwa wakati muafaka, hasa katika kuanzishwa Mamlaka itakuwa na

mtazamo mpana na kujumuisha hifadhi zisizo na mamlaka kama Ngorongoro. Katika Mkoa wa Rukwa, tunazo hifadhi na mapori ya uwindaji, ambayo yanavunwa kiholela na yamo katika hatari ya kutoweka. Halmashauri hazina fedha za kulinda mapori haya, mfano Pori la Lwafi, Wilaya ya Nkasi, ambalo *extension* yake inaingia katika Jimbo la Kalambo, likiungana na Msitu wa Kalambo (*Forest Reserve*). Eneo hili ni Shamba la BIBI, kila mtu anavuna rasilimali humo bila wasiwasi, kwani hakuna mwenyewe. Afisa Maliasili katika Wilaya ya Sumbawanga, amechoka mno hajui kinachofanyika. Pori la Hifadhi katika Bonde la Rukwa, linafilisika na watu wanalima na kufugia mle, hakuna anachofanya. Amekaa miaka mingi Sumbawanga kiasi amefikia *the highest stage of incompetence. Peter Principle*. Je, mnatusaidia vipi, wanyama wamekwisha, misitu imekwisha lakini waajiriwa wenu wanaranda randa mjini badala ya kulinda maliasili? Tusaidieni.

Hakuna linalofanyika kulinda mimea na Wanyama katika eneo dogo la *Kalambo Falls Reserve* na sasa watu wameingia pale wanajenga na wengine wanaharibu msitu unaozunguka eneo hili. Je, tuache eneo hili nalo liteketee? Wenzetu Zambia wanatucheka hatupo makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na Mashirika yake, kwa kazi nzuri ya utayarishaji wa Muswada huu, napendekeza maboresho yafuatayo:-

Sehemu ya 7(8) ibadilishwe kwa kuandikwa upya kwa utaratibu wa kuiunda sasa *Wildlife Authority*, kwa mpangilio unaofanana na *Tanzania Wildlife Protection Fund.*

Naunga mkono hoja ya kuupitisha Muswada wa *Wildlife Conservation Act, 2008*.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu, japo kwa kuchelewa. Pili, naomba nichangie mambo machache sana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na sheria na kuitekeleza sheria kikamilifu ni mambo mawili tofauti. Tunaweza kuwa na sheria nzuri kama Muswada huu ukipitishwa kuwa sheria, lakini kama usimamizi na utekelezaji wake utakuwa mbaya, itakuwa haijatusaidia hata kidogo. Kwa mfano, mwaka jana kuna watu ambao wamekuwa wanakamatwa wakijihusisha na uwindaji haramu; hata hivyo, wanapokamatwa wengi huachiwa kwa kile kinachoitwa kukosekana kwa ushahidi! Ukweli nyuma yake kunakuwa kuna rushwa. Naomba sheria hii itakapoanza kufanya kazi, utekelezaji na usimamizi wake uwe makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ifanye *decentralization* ya majukumu hasa ya ugawaji wa vitalu vya uwindaji. Kazi ya Wizara ibaki ya kutoa sera tu. Nasema hivi kwa sababu Muswada huu unampa Waziri, madaraka makubwa sana katika utekelezaji

wake utakapokuwa sheria. Pamoja na kwamba, sehemu ya tatu ya Muswada inampa Mkurugenzi madaraka makubwa, lakini nachelea kusema kwamba, Waziri anaweza kwa kiasi kuingilia utendaji kazi wa Mkurugenzi huyo na hivyo tija ya Muswada huu utakapokuwa sheria isionekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na uwindaji haramu, nashauri Kikosi Maalum cha Kupambana na Uovu huo, kama kinavyotajwa katika kifungu cha 9(3), kipewe vifaa vya kutosha, kama vile magari na pikipiki ili wafanye vizuri zaidi. Aidha, wapewe motisha, yaani mazingira mazuri ya kazi na marupurupu zaidi. Hii itasaidia waone kwamba, wanyamapori ni sehemu ya maisha na hii itawafanya wafanye kazi kwa bidii sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 8 (*Part VIII*) ya Muswada, inazungumzia mgongano wa binadamu na wanyama. Kifungu cha 70 kinazungumzia kwamba, iwapo wananchi wataharibiwa mazao yao, watapewa kifuta jasho.

Kifungu cha 70(2) kinazingatia kupewa kifuta jasho kwa ekari si zaidi ya tano. Kifungu hiki, hakimtendei haki mwananchi hata kidogo. Aidha, napendekeza kwamba, wananchi ambao mashamba yao (mazao) yataharibiwa na wanyama kama ndovu, basi wapewe fidia halisi ya mazao/shamba lililoharibiwa na si kifuta jasho *(Consolation)*, kama ilivyo kwenye Muswada. Aidha, Waziri mwenye dhamana ya wanyamapori, asilazimike kushauriana na Waziri wa Fedha na Uchumi ili kulipa kifuta jasho kwa wananchi ambao mazao yao yataharibiwa. Nashauri Waziri mwenye dhamana na wanyamapori, atenge bajeti ya malipo ya namna hii kwenye bajeti yake. Hii itasaidia kupunguza urasimu wa malipo kwa waathirika.

Naunga mkono Muswada. Ahsante sana.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Pamoja na ukweli kwamba, Sheria hii imechelewa; ni vizuri sasa imeletwa. Sheria hii haitakuwa na maana na mafanikio kama mambo fulani hayajatimia. Askari wa Wanyamapori au *Gamescouts* wa kutosha ni muhimu wawepo. Hivi sasa hakuna askari hao ambao nimewataja.

Ingawa Sheria hii inazungumza juu ya kuwepo Kikosi Maalum, yaani cha aina ya kijeshi; Kikosi hiki hakitaweza kuwa kikubwa cha kutosheleza ulinzi.

Serikali iache kuruhusu wanaopewa vitalu wawe pia walinzi wa vitalu hivyo, wakati wa kuacha uwindaji. Kama wenye vitalu wataendelea kubakia, basi wataendelea kuwinda. Sheria inazungumzia masuala ya fidia, kwa binadamu waliopata maafa kutokana na madhara ya wanyama. Hata hivyo, Sheria hii inazungumzia wanyamapori kama vile Watanzania, tunathamini wanyama kuliko binadamu kwa kile kinachojitokeza kwenye faini na fidia, kwa mtu aliyeumwa ama aliyemjeruhi mnyama. Faini na kifungo ni vikubwa sana.

Sheria inazungumzia *WMA* sasa kama ni Mradi Maalum kwa nchi. Hii itasaidia sana kulinda wanyama na kunufaisha sana vijiji vyenye kuzunguka mapori yenye wanyama.

Sheria ingefaa kutamka wazi wazi, sehemu za kuzalia wanyama hapa nchini na pia kutambua na kulinda njia ambazo wanyama hupitia wakati wa kuhamahama kwao, ambao ni utaratibu wa mazingira ya wanyama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 25 ambayo inatolewa na Wizara haitoshi, hasa ukichukulia ukweli kwamba, fedha hizi hazifiki kwa wahusika kutokana na mgawanyo ulivyotoka Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inatoa nafasi kwa Wizara kuwa na Kamati ya Ugawaji wa Vitalu. Kamati hii kazi yake kubwa ni ushauri tu; hivyo, bado maamuzi ya ugawaji wa vitalu upo mikononi mwa mtu mmoja tu. Mtu huyu ana hiari ya kukubali ushauri ama kuukataa. Je, Mkurugenzi wa Wanyamapori akiamua anavyotaka, hata kama ni vibaya, Waziri atafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya sheria ingeifanya Wizara ifanye kazi vizuri sana, kama sehemu hii ingekuwa ya kuundwa kwa Mamlaka ya Wanyamapori na madaraka yote yawe ya Mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika vitalu si jambo la siri; hivyo ni vyema mgao wa vitalu uletwe Bungeni hapa, itolewe taarifa kuwa nani amepewa kitalu gani. Pia watoe masharti ya kumiliki wa vitalu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sisi tunatoa vitalu vya kuwinda kitalii; hivyo basi, upo umuhimu wa kuvipumzisha vitalu hivi kwa miaka miwili ili wanyama waongezeke.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipatia uzima siku ya leo. Ninawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Serikali, kwa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia katika maeneo yafuatayo:-

Sehemu ya nne, usimamizi wa maeneo ya wanyamapori; nashauri Serikali ijenge mahusiano mazuri na wananchi wanaoishi jirani na hifadhi, kwani hawa ndio watakuwa wasimamizi wazuri wa rasilimali zetu.

Mheshimiwa Waziri, anieleze ni kwa namna gani Wananchi wa Bukombe watasaidia kusimamia na kulinda wanyamapori, kama idara inapowaahidi wananchi haitekelezi, kwa mfano, Meneja wa Kigosi/Myowosi aliahidi Sh. 8,000,000 za ujenzi wa Shule ya Msingi na hazitolewi leo mwaka wa tatu; kulikoni?

Kama wananchi wamekosa eneo la kunyweshea mifugo yao na umbali wa nusu kilomita toka kijiji kwenda kwenye hifadhi kuna bwawa halikauki; je. watakwendaje?

Je, kama wananchi wanahitaji kupata mnyama kwa ajili ya kitoweo hawapewi kibali; ni nini maana ya ujirani mwema?

Sehemu ya tano, chombo cha ushauri wa maliasili ya Wilaya, hapa naunga mkono na chombo hiki kipewe nguvu ya kutekeleza baadhi ya masuala ya Kiwilaya.

Sehemu ya saba, uvunaji wa wanyamapori ngazi ya Wilaya. Naishauri Serikali 25% inayotolewa haifiki na haitoshelezi; ni vizuri kuwepo na fungu rasmi linalotolewa kwenye Halmashauri ya Wilaya. Kuna ugumu gani wa kutoa asilimia kama wanavyofanya kwenye madini?

Wilaya wapewe mamlaka ya kutoa vibali vya kuvuna kitoweo kwa wananchi. Tunaona shida kuwepo kwa hifadhi hizi, kwani hazitusaidii. Mimi binafsi nimewahi kuomba mnyama kwa ajili ya kitoweo jimboni kwangu, nilikuwa nina sherehe sikupewa. Kama mimi Mbunge ninanyimwa, je, wananchi wa kawaida itakuwaje?

Sehemu ya nane, kifuta machozi; Serikali lazima itamke kiwango rasmi cha fidia. Kwa nini adhabu ya waharibifu, kifungu cha 14(2) kiwango kimetajwa? Serikali itamke kiwango rasmi leo.

Sehemu ya 18, utoaji wa tuzo kwa watoa taarifa. Lazima Serikali ijenge mahusiano mazuri na wananchi ndipo wataweza kutoa taarifa. Kama hata ahadi hazitimizwi nani atatoa taarifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, wakati Muswada huu utaanza kufanya kazi, Sera iangalie uwezekano wa kuhusisha ongezeko la watu. Mfano, Bukombe 40% ni makazi ya watu, 60% ni Hifadhi ya Kigosi/Myowosi, wakati huo huo ongezeko la watu ni 7.4% kwa mwaka. Kwa hali hiyo, lazima tupanue eneo la makazi, tumege toka 60% za hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naipongeza Wizara hii kwa Muswada huu, hasa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa kazi nzuri na kuwasilisha Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi, naunga mkono sheria hii ipitishwe. Naiomba Serikali kwa usimamizi mzuri wa Wizara, basi Muswada huu ukipitishwa, usimamiwe kwa elimu, miundombinu, utalaam na kadhalika kuepuka hasara na ukosefu wa fedha za kigeni kwenye sekta, mapato ya nchi, pia kujali uzalendo, kwa maana Serikali ifaidike na wananchi wenyewe na kujali mtu kuliko mnyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitalu vitakapofika wakati wa kugawiwa, vigawiwe vizuri kwa manufaa ya Tanzania na Watanzania wenyewe. Kwa hiyo, naomba kuwe na usimamizi mzuri wa mikakati ya kufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, natumaini Muswada utapita ili tufaidike na Sheria hii Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata maelezo ya ziada ya kifungu cha 115, ambacho kinampa madaraka Mkurugenzi kwa wale watakaokiri kufanya kosa, kulipa faini kuanzia kaisi cha Sh. 200,000. Pia anaweza kutoa amri ya kutaifisha mifugo, kifungu kidogo cha 3(a); nini nafasi ya Mahakama katika nchi hii; je, kipengele hiki hakitoi fursa ya kuendeleza rushwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia majedwali No. 1 hadi IV, sikuona neno Twiga kama mnyama, ndege, mnyama hatari au wanyama wa taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa wangu mdogo, Twiga amebeba nembo ya Taifa hili na kutoonekana katika Sheria, inanipa hofu ni ama mnyama huyu hana umuhimu huo tena au ni upungufu wa kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa WMA ni mzuri na utawanufaisha sana wananchi na kuona sababu za kuhifadhi wanyamapori. Kwa maoni yangu, ningependa mpango huu uende sambamba na uhifadhi wa misitu, badala ya kuwa na mpango wa kila Sekta pekee na uwezo wa kiuendeshaji vijijini kama itakuwa ni mpango mmoja, unaweza kuleta tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya misitu ni mbaya kama wanyamapori kutokanana na ukataji wa miti holela na ujangili; hivyo, uwepo mkakati wa pamoja na hususan misitu na wanyama kwa sababu misitu ndio makazi ya hao wanyama tunaowajadili katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika nchi yetu wanyama wanapungua, binadamu wanaongezeka na ardhi inaendelea kutengwa kwa ajili ya wanyamapori. Leo karibu 30% ya eneo la nchi ni hifadhi. Sasa ni vyema Wizara ikaandaa mpango wa kuweza kujenga mazingira mazuri na kuepusha migogoro kati ya binadamu na misitu ya hifadhi na mapori ya wanyama. Vinginevyo, katika miaka michache ijayo, migogoro hii itaibuka kwa kasi ambayo Serikali haitaweza kuizuia. Pia uwepo mkakati wa makusudi wa kusimamia Sheria zilizopo, badala ya kusubiri wananchi ambao wakishaanzisha shughuli zao za kibinadamu halafu mnakuja kuwaondoa, hawaelewi utendaji kazi wa Serikali

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kukumbushia juu ya kifuta machozi kwa ajali ya mtu aliyeliwa na mamba toka Nyanguge. Nilimpelekea ombi hili Mheshimiwa Waziri, muda sasa umepita, kila mara naulizwa na wahusika kuwa suala hili limefikia wapi.

Tafadhali sana naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kuleta Muswada huu.

Naomba kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Hifadhi ya Sokwe. Kwa kuwa historia ya kale inaonyesha binadamu walianza kuishi kwa mfano wa sokwe; Wizara ifanye Mkakati Maalum wa Kuhifadhi Sokwe. Bado wapo sokwe wachache maeneo ya Kigoma. Tusiache wanyama hao wakatoweka.

Pili, Usafirishaji wa Pembe za Ndovu. Kwa kila pembe ya ndovu inayosafirishwa nje kwa kutolewa leseni Kisheria, kunaidhinisha kifo cha tembo. Lazima Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, itambue kuwa kwa kila leseni inayotolewa kwa idadi ya pembe, inatoa idhini rasmi ya kuuawa kwa tembo mmoja kwa kila pembe mbili.

Tatu, kutambua na kuhifadhi wanyama adimu katika Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Amani – Muheza.

Muswada lazima uelekeze kutambua kuwepo wanyama wachache maalumu wanaopatikana katika sehemu chache Duniani. Katika Hifadhi Asili ya Msitu wa Amani, wapo aina chache ya wanyama wa aina hiyo. Naishauri Wizara ifanye utafiti kuwatambua na kupanga mkakati wa kuwahifadhi.

Nne, Hifadhi ya nyoka na Vipepeo. Muswada huu hauonyeshi kutambua nyoka na vipepeo ambao wapo katika Hifadhi za Taifa. Wapo aina ya nyoka na vipepeo ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Amani Muheza. Vipepeo wanavunwa na kusafirishwa nje ya nchi na kuwapatia kipato Wananchi wa Milima ya Amani, Muheza na wapo ndani na nje ya HIfadhi ya Asili ya Msitu wa Amani. Je, ni Sekta gani inawajibika katika hifadhi zao wakati ambapo Wizara ya maliasili na Utalii ndio msimamizi wa Hifadhi za Taifa na Misitu ya Asili?

Tano, ukomo wa kuongeza maeneo ya Hifadhi. Ni vyema Sheria ikatambua kwamba, idadi ya mifugo ya nyumbani ikiwa ni pamoja na ng’ombe mbuzi na punda inaongezeka wakati ardhi haiongezeki. Kwa msingi huo, lazima uwepo ukomo wa kuongeza maeneo ya Hifadhi na wakati huo huo kuona upo uwiano wa kudhibiti

ongezeko la wanyama, sambamba na Sheria hii inajenga dhana ya kuwalinda wanyamapori.

Sita, uhamasishaji wa matumizi ya nyama ya wanyamapori. Tuhamasishe na kuruhusu matumizi ya nyama ya wanyamapori kwa mpango unaofanana na ule wa *Cannavon Hotel* iliyopo Nairobi Kenya. Yawepo maeneo ya uwazi na halili, ambapo wananchi wataweza kuondoa hamu ya kula nyama za wanyamapori. Sheria itambue na kuweka leseni maalumu kwa mpango kama huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, mjadala huu umechukua kasi kubwa na umechukua takriban siku tatu tukiendelea kujadiliana na kuiboresha hoja ya Muswada huu muhimu sana. Sasa, tuingie katika hatua inayofuata, nayo ni kumpa nafasi mtoa hoja ili aweze kuanza kuhitimisha hoja yake. Sasa kwa kadri ya utaratibu, mtoa hoja anatakiwa awe na saa nzima ya kufanya hivyo, lakini kwa taarifa niliyonayo hapa mezani, Mheshimiwa Naibu Waziri atatumia dakika 20 kuchangia hoja hii na vile vile kutoa majibu kwa Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Waziri atatumia dakika 40.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa msaada mkubwa ambao wamekuwa wakitupa si katika hatua hii ya mwisho ya kujadili Muswada huu hapa Bungeni, lakini katika hatua nyingi ambazo Muswada huu umepitia kama ambavyo wengi wamekuwa wakisema kwamba Muswada huu umekuwepo kwa takriban miaka kumi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kabla sijaendelea sana na Muswada, ningependa nigusie jambo moja ambalo linahusu wananchi wangu wa Jimbo la Msalala. Pia naomba nitoe pole sana kwa familia ya Mzee Horogosho, mkazi wa kijiji cha Masabi ambaye usiku wa kuamkia jana kulitokea tukio la mauaji ya wanafamilia wake watatu, akinamama watatu kukatwa mapanga kwa sababu zisizojulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili ni kubwa na kwa mara nyingine tena imeonyesha tu ni jinsi gani nguvu zinahitajika za pamoja za kukabiliana na matatizo gani. Natoa pole sana kwa familia hiyo na wananchi wenzangu wa Jimbo hilo. Niseme nimeguswa sana na tatizo hili na kwa sababu hiyo, nitatafuta namna ya kuhakikisha kwamba walau ikiwezekana kesho niweze kufika kuwaona na kuwapa pole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niombe sana vyombo vya dola kwa maana ya Polisi na Sungusungu wajaribu kusaidiana kuimarisha ulinzi na kuhakikisha wenye tatizo hili kwa maana kwamba watuhumiwa wanafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano ambao amekuwa akiuonyesha na kwa kupokea maoni kama ambavyo

Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba katika majadiliano ya Muswada huu, yamefanyika mabadiliko makubwa sana, ukiangalia tokea ulipowasilishwa kwa mara ya kwanza mwaka jana hadi hivi sasa, kumekuwa na mabadiliko mengi ambayo Mheshimiwa Waziri amekuwa akipokea na kwa kweli amekuwa akikubali kufanya marekebisho. Kwa hiyo, namshukuru sana na namshukuru pia kwa kutoa wigo mpana wa ushiriki *(participation)* hata kwetu sisi ambao ni wasaidizi wake pale Wizarani. Mtindo huu wa ufanyaji kazi unanipa moyo sana na kwa kweli unaniimarisha kwa sababu nimepata nafasi nzuri ya kuweza kushiriki kikamilifu katika kuandaa na kuratibu uwasilishaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijagusia baadhi ya hoja ambazo zimewasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, nitoe wito tu au nizungumzie suala zima la uhifadhi kwa ujumla wake. Tuna matatizo makubwa sana katika uhifadhi, matatizo haya msingi wake ni ongezeko la binadamu na pia yanatokana na ongezeko la matumizi ya ardhi. Tatizo hili, dawa yake haiishi katika kupunguza maeneo ambayo yamehifadhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tunahitaji kufanya jitihada za pamoja sisi kama viongozi kuona nini cha kufanya ni changamoto kubwa sana ambayo tunayo na niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba Wizara yangu tuna nia ya dhati kabisa ya kutimiza majukumu ambayo wananchi Watanzania wametutaka tufanye, majukumu hayo ni kulinda rasilimali tulizonazo na kuratibu matumizi yake ili zitumike kwa sasa na kwa kusaidia vizazi vitakavyokuja

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, Muswada huu uliowasilishwa hapa hata wakati mmoja hauna nia hata kidogo ya kuweza au kukusudia kuwaumiza wananchi kama ambavyo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameonyesha hisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Muswada huu ni kwamba tumekusudia kufanya mapinduzi makubwa katika sekta nzima ya Wanyamapori, tumekusudia kuongeza ushiriki wa wananchi ukiangalia kwa mfano *part* ya kumi na mbili inazungumzia kuanzisha vitu vipya kabisa ambavyo havikuwepo, kwa maana ya kuanzisha mambo kama *ZOO*, *ranches*, *WMAs*, haya yote yanatoa nafasi ya wananchi kushiriki, kwa kujiongezea kipato kutumia wanyamapori tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala zima la migogoro ambalo limekuwepo kwa muda mrefu kuhusu mipaka, maeneo ambayo ni *corridors*, maeneo ambayo ni *buffer zones* nalo limezungumziwa kipekee kabisa katika sheria, naamini kwamba Waheshimiwa Wabunge wakituunga mkono katika kuipitisha sheria hii, matatizo ambayo tunayo hivi sasa yamepungua kwa kiasi kikubwa. Nataka niseme tu kwamba kwenye sheria imempa nafasi Waziri kuangalia upya hali ya uhifadhi ilivyo, hali ya mipaka na mapori ilivyo, kwa maana ya kutafuta namna ya ku-*create buffer zones* na kulinda maeneo ya mtawanyiko ya wanyama na maeneo mengine ambayo ni ya muhimu kwa ajili ya wanyama, kwa hivyo, matatizo ambayo tumekuwa nayo Muswada unakusudia kuyaondoa na si kuyaongeza au kuyalinda. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tushirikiane na kwa pamoja tupitishe Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niwaombe sana Waheshimwa Wabunge wenzangu kwamba pengine baadhi ya maneno tunayotumia kwa kweli yanakuwa ni makali sana. Kwa mfano, tunaposema Serikali inakusudia kwenye suala la matumizi ya silaha ile *section* ya kumi na mbili kwamba wananchi watapigwa risasi na kadhalika. Nafikiri *section* ile tukiisoma na ukisema hivyo kwa mwananchi anayesikiliza redioni au anatazama bila kuona sheria yenyewe, anaweza akasema kwamba kwa kweli hawa wenzetu walioko huko Wizarani wanafanya vitu vya ajabu. Tumejaribu kila hali kuangalia namna nzuri ya kuhifadhi maeneo yetu lakini kwa kuzingatia usalama wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binadamu Tanzania yuko juu ya kitu chochote, kwa hiyo, hisia za kwamba Muswada unakusudia kulinda wanyama zaidi kuliko binadamu, binadamu wapiga kura wetu watapigwa risasi na kadhalika, hizo ni hisia tu lakini sheria imeliweka jambo hili vizuri sana. Kwa hiyo, naomba pengine ni vizuri Waheshimiwa Wabunge maneno ambayo kimsingi yanaweza yakaleta hofu kwa wananchi na kujenga hisia mbaya kwa Serikali yao, si vizuri tukayatumia kwa sababu yanaweza yakafanya wananchi wakajenga chuki ambayo kwa kweli si nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nipitie baadhi ya hoja ambazo Wabunge wameziwasilisha, hoja zilizo nyingi Waziri atazizungumzia, nami nitagusia baadhi ya maeneo ambayo Waziri amenitaka niyazungumzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ambaye amezungumzia suala la watumishi kutokuwa wengi kutoka kwenye mamlaka ya Wilaya ya Kilindi, Watumishi walioko kwenye Halmashauri wako chini ya TAMISEMI na kama mwenyewe alivyosema jana kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi iliruhusiwa kuajiri na alisema kwamba waliruhusiwa kuajiri watumishi wane. Kwa bahati mbaya hawakupatikana, kwa hiyo, tatizo si la kwetu kwamba sisi tunakataa au hatuna nia, isipokuwa tatizo kwa jinsi lilivyowasilishwa ni kwamba watumishi wenyewe hawakuweza kupatikana kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaongeza jitihada za kufundisha wataalam lakini pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, kwenye Halmashauri zetu tutoe kipaumbele kwa Maafisa wa Wanyamapori na Maafisa wa Maliasili ili waajiriwe na tuwapatie vitendea kazi kwa sababu sehemu yao ya kazi ni kwenye Halmashauri, ni waajiriwa wa Halmashauri ambayo wapo chini ya TAMISEMI. Kwa hiyo, tukifanya hivyo tutaweza kushirikiana na kuweza kupata ufumbuzi wa pamoja kwenye matatizo tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Anastazia Wambura kwanza ameshukuru na kupongeza wazo la kuwepo *WMA* na amesema kwamba litaweza kuongeza ustawi wa jamii. Ni kweli tunashukuru kwa kuliona hilo, amesema ibara ya 73 inaweza ikapunguza migogoro lakini akashauri kwamba, kwenye Kanuni tuweke mwongozo utakaosaidia uchimbaji wa mabwawa ili wanyama wasitoke kwenye hifadhi wakaenda kwenye maeneo ambayo binadamu wanaishi. Ni ushauri mzuri, tutauangalia kwenye Kanuni lakini kwa kuzingatia *general management plans* za *reserves* zetu pia mambo mengine

kama *EIA* pamoja na uwezo wa kifedha wa Serikali. Lakini hii ni hoja nzuri ambayo tutaichukua katika utekelezaji wa sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rished Abdallah amezungumzia uchelewaji wa malipo kwamba yamechelewa sana. Ni kweli na kama nilivyojibu swali hapa jana, kulitokea matatizo ambayo kimsingi ni ya kutokuelewana, utaratibu uliokuwepo haukuwepo ndani ya sheria, ulikuwa unawekwa kwa ajili ya *Administrative convenience,* sasa kwa sababu jambo hili tumeliweka kwenye sheria. Suala la kifuta machozi liko sasa kwenye sheria, naamini kwamba baada ya sheria hii kupita utekelezwaji na ulipwaji wa fidia au tunavyoita sisi ulipaji wa kifuta machozi utakuwa unafanyika kwa kasi zaidi. Lakini pia hata uelewa wa wanachi kuhusu taratibu za kufuata ili kuweza kulipwa utawekwa bayana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema pia kwamba wananchi wanaozunguka hifadhi ya Sadani wapewe elimu namna ya kuanzisha *WMA*. Hili tumelichukua na kulifanyia kazi na ndio nia yetu hasa. Vilevie amezungumzia tatizo la mipaka kwenye maeneo ya hifadhi, hilo tutaongea na wenzetu wa *TANAPA* na tutafuatilia kwa karibu tuone jinsi matatizo haya yanavyoweza kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Gosbert Blandes, rafiki yangu huyu amesema kwamba ibara ya 17(4) kinatoa faini kubwa mno kwa wanyama hasa mifugo kuingizwa kwenye hifadhi au kuingizwa kwenye maeneo ambayo yanazuiliwa kisheria kwa mujibu wa sheria hii. Jambo hili kwa kweli ni gumu, ukilinganisha kwamba umeingiza mbuzi mmoja, kweli unaweza kuona kwamba linaweza likawa ni tatizo lakini *practical cases*, yanaingizwa makundi ya mifugo. Mheshimiwa Blandes anatoka Mikoa ya Magharibi ya nchi yetu, makundi makubwa ya mifugo na mengine yanatoka nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Waheshimiwa Wabunge mnakumbuka kwamba, mwaka jana tulikuwa na tatizo kubwa sana la mifugo, sasa bila ya kuwa na sheria na katika sehemu nyingi mara nyingi tumekuwa tukipata matatizo ya utekelezaji wa sheria zetu kutokana na udhaifu wa adhabu zilizowekwa. Kwa hiyo, tukaona kwamba pengine kiasi hiki cha fedha ambazo tumeweka kama faini kinaweza kikasaidia. Naomba Mheshimiwa Mbunge atuelewe huu ni mwanzo tutaona utekelezaji wake. Lengo si kupata faini lakini lengo ni ku-*avoid offence,* kwa hiyo, nafikiri ni vizuri wananchi wakajikita zaidi katika ku-*avoid* kufanya tukio au kufanya uhalifu zaidi ya kuzungumzia kupunguza adhabu inayotokana na kosa lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni vizuri nimwombe Mheshimwa rafiki yangu huyu kwamba, pengine kwa sasa hizi adhabu ambazo tumependekeza zinaweza zikatusaidia sana hasa kwa matukio makubwa ambayo yanatishia uwepo wa hifadhi zenyewe, hifadhi ya Kigosi, Moyowosi ziko kwenye hali mbaya sana, hifadhi za Burigi, Kimisi ni hifadhi ambazo zimeshavamiwa kwa kiasi kikubwa sana na uvamizi unafanyika na mifugo. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri Mheshimiwa Mbunge akatuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rafiki yangu Mheshimiwa Killimbah amezungumzia kuhusu maeneo ya Wembere kwamba yaongezwe kwenye hifadhi. Ni ushauri mzuri, tutauchukua na nia kama hii kwa kweli inatusaidia na naamini kwamba tutatoa ushirikiano kama alivyoomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, amezungumizia nyani aliyemtunza mtoto na kwamba Wizara iweze kutoa matunzo kwa mtoto huyo. Ni jambo ambalo kwa msingi linahitajika litazamwe kwa na jamii kwa ujumla wake. Nyani yule amefanya kazi yake, ametoa mchango na kwa kweli ni bahati mbaya tu kwamba kumpata mtoto yule, ilifikia hatua kwamba akauawa yule mnyama lakini nia hasa ambayo tunapaswa tuwe nayo kwa sasa ni namna ya kumwangalia mtoto huyu na hili jukumu ningeomba liwe la jamii kwa ujumla wake na sisi kama Wizara, kama Watanzania tutashirikiana lakini ningeomba lisiwe jukumu letu peke yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee wangu Hamza Mwenegoha amezungumzia Askari Wanyamapori kwamba wanatesa wananchi, wakati mwingine wanawarusha kichurachura wazee. Niseme sheria hata ile ambayo tunazungumzia kuifuta kwa Muswada huu hairuhusu vitu kama hivyo, inataratibu za kumkamata mtu na ina taratibu za kutoa adhabu kwa mtu ambaye amefanya kosa na utaratibu ni kumpeleka kwenye vyombo vya sheria. Kwa hiyo, Askari wanaofanya hivyo naomba niwakemee sana na niseme tu kwamba kama wapo wanaofanya tabia hii kimsingi haiko kwenye sheria ni uvunjaji wa sheria waache mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Raphael, Mheshimiwa Luhaga Mpina, ndugu yangu huyu amezungumzia sana matatizo ya Meatu, ni kweli nilifika, suala la mpaka lilivyo ni moja ya maeneo ambayo yanatia changamoto sana. Mpaka ulivyo wa Maswa *Game Reserve* na Wilaya ya Meatu na Bariadi ni eneo ambalo lina tatizo, kwenye sheria tumependekeza kwamba baada ya kuwa sheria imepitishwa basi tutaangalia upya hali ilivyo ya *buffer zones,* kwa kuanzia tumesema angalau pawepo mita mia tano angalau lakini kwenye maeneo ambayo yana hali mbaya kama eneo hili Serikali kwa maana ya Wizara, tutakuwa na mpango mwingine ambao tutaangalia ni namna gani kwa sababu sheria itakuwa inatupa nafasi ya kufanya maamuzi na kuona nini cha kufanya, basi tutalitazama katika utekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Luhaga, ameuliza Afisa Wanyamapori yupi ana jukumu la kuwadhibiti wanyama waharibifu. Kwa *set up* ilivyo ni kwamba, katika kila Wilaya kuna Afisa Wanyamapori yaani *District Game Officer,* Afisa huyu pamoja na majukumu yake mengine ni kusaidia kuratibu uvunaji wa wanyamapori kwa maana ya kutoa vibali, lakini pia kusaidia pale ambapo kunakuwa na matatizo ya wanyama waharibifu na ndio maana kwenye ule mgawanyo wa zile asilimia 25 ambayo inarudi asilimia 40 ya hizo asilimia 25 zinazorudi zinabaki kwenye Wilaya lengo ni kusaidia huyu Afisa wanyapori kwenye ngazi ya wilaya ili aweze kununua risasi na vitu vingine ambavyo ni vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia, kusudio la kuwepo *District Game Officer*s ni kusaidia kuratibu shughuli za wanyamapori kwenye ngazi ya Wilaya,

amezungumzia kwamba hawana gari. Hili ni tatizo la kifedha ambalo tutaliangalia ni namna gani tufanye lakini ningeomba pia Halmashauri nazo ziangalie namna ya kusaidia kwenye maeneo yao kwa sababu kama nilivyosema kwamba Maafisa hawa wapo ngazi za Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shellukindo amesema Wizara ifanye utafiti kuwezesha Wilaya ya Lushoto hususan milima ya Usambara kunufaika na utalii. Hili tutalifanyia kazi na alishawahi kuuliza swali kuhusu jambo hili na akatoa mfano utalii wa kutembea kwenye maeneo kama nchi za Shelisheli. Hili ni wazo zuri ambalo tumelichukua na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma Mikidadi amezungumzia migogoro kati ya wananchi wa Kijiji cha Miguruwe na mmiliki wa kitalu. Tuseme migogoro ambayo ipo kwa sasa hivi ni mambo ya kiutendaji na tumesema kwenye sheria utaratibu utakaokuwepo wa kutoa na kusimamia uwindaji wa kitalii utakuwa ni tofauti, baada ya sheria hii kupita migogoro kama hii itaweza kuondolewa, lakini kwa hatua za kuanzia tutachukua hatua sisi kama Wizara kujaribu kufuatilia ni nini tatizo na kuona ni namna gani tuweze kulitatua hata kabla sheria haijaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Masaburi amesema Serikali itangaze fursa zilizopo katika Muswada ili kuwawezesha kunufaika kiuchumi. Fursa zilizopo ni nyingi kama nilivyosema, nimegusia mwanzoni kabisa, tumesema sheria inatoa nafasi kwa wananchi kushiriki kuanzisha *wildlife, zoo* na inaruhusu kuanzisha *WMA's*. Hizi ni baadhi tu ya fursa kwa hiyo ni vizuri wananchi wakazitumia na elimu baada ya sheria kuwa imepita tutaendelea kuitoa.

Mheshimiwa Mntangi amesema sokwe waliopo maeneo ya Kigoma wasiachwe wakatoweka. Tunashukuru kwa ushauri, tutaongeza jitihada za kuwahifadhi na kwa kweli *threat* iliyopo ni kubwa lakini na sisi tunajaribu kujipanga na ndiyo maana tumeleta Muswada huu ili tuweze kupata nguvu zaidi ya kuweza kusimamia. Amezungumzia pia Wizara ifanye utafiti wa kuwatambua na kufanya mkakati wa kuhifadhi wanyamapori adimu katika msitu asili wa amani. Hili tutalifanya, tunashukuru kuona ni namna gani tunaweza tukalihifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mntangi amesema Serikali iweke ukomo wa maeneo ya kuhifadhi ili kuweka uwiano wa kudhibiti ongezeko la wanyamapori hili tutalizingatia na ndiyo maana tumeweka sheria hii na katika sheria hii tunakusudia kuwa na maeneo ambayo tunaweza tuka-*manage* ndiyo maana kwa mfano *game controlled areas* ambazo ziko kwenye maeneo ya wananchi yaani kwenye *general rent* tumesema kwamba tutaziondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii nimshukuru Naibu Waziri kwa kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu. Lakini naomba niseme jambo moja kwamba, hoja iliyopo mbele yetu kwa maana ya Muswada ambao

umeendelea kujadiliwa, ni Muswada wenye maslahi makubwa sana kwa Taifa letu na ni Muswada ambao utatunga sheria na sheria hiyo ni muhimu sana kwa maslahi ya nchi yetu na wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kwa kuzingatia hayo niliyoyasema, naomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote wajue na waelewe hatua hii ambayo nataka kuitangaza hivi punde. Katika Kanuni yetu ya Bunge ya 2(2) ambayo inasema: "Iwapo jambo au shughuli yeyote haikuwekewa masharti katika kanuni hizi, Mwenyekiti ataamua utaratibu wa kufuata katika jambo hilo au shughuli hiyo kwa kuzingatia Katiba, sheria nyinginezo za nchi na Kanuni nyinginezo zilizopo, maamuzi ya awali ya Mwenyekiti ya Mabunge pamoja na mila na desturi za uendeshaji bora wa shughuli za Bunge na uamuzi huo utaingizwa katika kitabu cha maamuzi ili kuongoza mwenendo wa baadaye wa uendeshaji wa shughuli za Bunge letu".

Waheshimiwa Wabunge, kwa kanuni hiyo naomba tusitishe shughuli za Bunge asubuhi hii ili suala lifuatalo liweze kuchukua nafasi. Tumepokea majedwali ya mabadiliko katika sheria hii ya kutosha sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wengi, lakini vilevile michango ya Waheshimiwa Wabunge mingi imelenga kukusudia kufanya mabadiliko katika vifungu mbalimbali vya sheria hii. Sasa nadhani tutoe nafasi nzuri kwa muda huu uliobakia ili Waziri, Wajumbe wa Kamati inayohusiana na Muswada huu na Waheshimiwa Wabunge ambao wanafikiri Muswada huu ufanyiwe tena mabadiliko katika maeneo kadhaa wapate nafasi ya kukaa pamoja kuanzia muda huu hadi saa kumi na moja jioni, na hivyo basi tutumie nafasi ya uwakilishi wetu ili tutakapoingia hapa ndani saa kumi na moja tuweze kuwa tumepata muda wa kutosha wa kufanya mashauriano na makubaliano ambayo yatawezesha sheria hii kutungwa ikiwa bora zaidi kwa manufaa ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba mridhie hilo na kwa kuwa nimetumia hiyo kanuni namba 2(2), naomba tena nitumie Kanuni namba 28(2) ya kusitisha shughuli hizi za Bunge asubuhi hii. Kwa mujibu wa kanuni, naomba nimwite Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Utaratibu na Bunge aweze kutoa hoja ya kusitishwa kwa shughuli hizi mapema na nikisha wahoji basi nitasitisha shughuli hizi ili nitoe nafasi kwa timu hizo ambazo nimezitaja ziweze kukutana na zitakutana mara tu baada ya kusitishwa kwa Bunge kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa.

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI

**WAZIRI WA NCHI SERA, UTARATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema mwenyewe kwamba Muswada huu ni Muswada muhimu sana na Waheshimiwa Wabunge wametoa maoni mazito kuhusu Muswada huu na majedwali mengi yameandaliwa ili kufanya mabadiliko katika Muswada.

Hivyo, ili kumpa Waziri nafasi ya kutafakari haya yote na pia kutenda haki kwa wale ambao wameandaa majedwali haya, naomba kwa masharti ya kanuni ya 28 kanuni ndogo ya pili kutoa hoja kwamba Bunge lako lisitishe shughuli zake kwa sasa ili Kamati husika ikutane na turejee hapa saa kumi na moja jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri nakushukuru, Waheshimiwa Wabunge hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono na sasa ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni ili Kamati na makundi hayo yaweze kushauriana vizuri.

*(Saa 05.50 asubuhi Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Muswada wa wanyamapori wa mwaka 2009 kwa maana ya mjadala. Kama nilivyosema mchana wakati nilipotumia vifungu vyangu kusitisha shughuli za Bunge nilikuwa nimemaliza na uchangiaji wa Naibu Waziri. Kwa hiyo, kabla sijaendelea sasa na shughuli inayofuata naomba nimwite Katibu atuongoze katika hoja ya jioni ili tuweze kuendelea na shughuli ya jioni.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa ya kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa.

Kwanza, kabisa napenda kuishukuru sana Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Uenyekiti wake Mheshimiwa Job Ndugai kwa jinsi ambavyo imekuwa msaada mkubwa katika kuuchambua na kuuboresha Muswada huu hadi kufikia hapa tulipo. Kama Waheshimiwa Wabunge mnavyofahamu Muswada huu umekuwa kwenye mchakato wa kuandaliwa kwa kipindi cha takriban miaka kumi iliyopita. Matokeo yake ni kwamba umekuwa ni Muswada wa namna ya pekee uliohusisha wadau wengi sana kuliko Miswada mingi iliyowasilishwa katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya Kamati pamoja na wadau mbalimbali wakati wa warsha za kanda na mikutano ya wananchi imekuwa na manufaa makubwa katika kuboresha Muswada huu. Aidha, michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, wakati wa semina iliyofanyika hapa Dodoma tarehe 2 Novemba, mwaka 2008 imeboresha sana Muswada huu.

Napenda kusema pia kwamba tangu Ijumaa iliyopita wakati Muswada huu umewasilishwa kwa mara ya pili hapa Bungeni Waheshimiwa Wabunge mmekuwa na michango na maoni mengi yaliyokuwa na manufaa makubwa katika kuuboresha na hivyo kuweza kujenga mazingira bora zaidi ya kuendeleza rasilimali yetu ya wanyamapori hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba pia nimshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwa michango mizuri wakati alipochangia katika Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Katibu Mkuu wangu, Dr. Komba, watalaam na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano na kazi kubwa waliyoifanya katika kuandaa Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia ama kwa maandishi au kwa kuzungumza moja kwa moja wakati wa mjadala wa hoja hii. Katika hili, napenda kuwatambua waliochangia kwa kuzungumza moja kwa moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, ambaye alikuwa Msemaji wa Kamati; Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambaye alikuwa Msemaji wa Upinzani; Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Benedict Ole- Nangoro, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Said Amour Arfi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Samson Mpanda, Mheshimiwa Kaika O. Telele, Mheshimiwa Rosemary Kirigini na Mheshimiwa Ezekiel Maige, Naibu Waziri wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Fatma Mikidadi na Mheshimiwa Gosbert Blandes. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya,

Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Mariam Hewa, Mheshimiwa Vuai A. Khamis, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Benedict Ole- Nangoro, Mheshimiwa Profesa Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba na Mheshimiwa Wilson Masilingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango iliyotolewa yapo mambo mengi ya msingi ambayo yamejitokeza. Hata hivyo kwa muda tuliopewa ni mfupi inawezekana mengine tusiweze kuyafikia katika kujibu na kuyatolea maelezo. Lakini, naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, kwamba tutayazingatia yote katika msingi wa manufaa ya nchi yetu na wananchi wake katika kuhakikisha suala zima la uhifadhi wa maliasili ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kujibu hoja moja baada ya nyingine kama zilivyowasilishwa wakati wa mjadala, naomba kutoa maelezo ya jumla kwa yale masuala ambayo yanaingiliana au yameulizwa na idadi kubwa ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ni suala la kifuta machozi. Napenda kulihakikishia Bunge hili Tukufu kwamba Serikali ina thamini sana maisha na mali za wananchi wake. Kama mtakavyokumbuka katika semina ya Waheshimiwa Wabunge iliyofanyika tarehe 2 Novemba, 2008 suala hili lilijadiliwa kwa kina ikiwa ni pamoja na wakati wa mijadala yote ya warsha za Kanda katika mchakato mzima wa kuandaa Muswada huu. Kwa rejea hiyo ningependa kuwambusha Waheshimiwa Wabunge, masuala ambayo kimsingi tulikubaliana kama ifuatavyo:-

Kwamba ni kweli kwa baadhi ya maeneo nchini wanyamapori wanaathiri kwa viwango vikubwa mali na maisha ya wananchi. Kwamba rasilimali ya wanyamapori ni mali ya umma wa Tanzania wote ambapo usimamizi wake umekasimiwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo wanyamapori wanaolalamikiwa kusababisha madhara ni sehemu ya mali ya wananchi wote. (*Makofi*)

Kwamba katika nchi yetu thamani ya maisha ya binadamu haina kipimo na hivyo haiwezekani kufidia maisha ya mwananchi kwa sababu thamani ya uhai wa binadamu hatuwezi kuifahamu ni kitu ambacho ni kigumu kwa kweli kwa kuwa hakuna nchi yoyote ambayo inaweza ikafahamu bei ya roho ya binadamu iliyotoka ni kiasi gani au maisha ya binadamu aliyopoteza, ni kiasi gani kwa sababu kile ni kitu kitakatifu na kitu ambacho kwa kweli kinaheshimika sana. Kwa hali hiyo ningependa pia kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba suala la fidia wala kifuta machozi haijawahi kuwepo kwenye Sheria ya Wanyamapori.

Kilichofanyika ni kwamba katika utaratibu wa kiutawala Serikali kwa kipindi cha takribani miaka 10 iliyopita kwa kupitia Wizara yangu imekuwa ikitoa kifuta machozi

cha Sh. 50,000/= kwa kupoteza maisha ya binadamu kutokana na wanyamapori. Kuanzia mwaka 2007 kiwango cha kufuta machozi kilipandishwa kuwa Sh. 200,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mazingira hayo na kwa kutambua kuwa haiwezekani kukaa kimya wakati wananchi wanaathiri kutokana na rasilimali hii ya umma. Serikali imeona kuna umuhimu wa kulipa kifuta machozi kwa madhara yanayosababishwa kwa binadamu na kifuta jasho kwa madhara ya wanyamapori kwenye mashamba ya mazao.

Aidha, kwa mara ya kwanza Serikali imeamua kuweka suala la kifuta machozi na kifuta jasho kwenye Muswada wa Sheria ya Wanyamapori ili iwe ni uhalali wa kisheria kwa mwananchi kudai madai hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuongeza kwamba kama nilivyobainisha awali rasilimali ya wanyamapori ni mali ya umma ambapo sehemu yake Watanzania wanaathirika kutokana na wanyamapori hao. Ni katika kuzingatia kuwa rasilimali hii ni mali ya umma na hivyo ndiyo sababu mapato yanayotokana na wanyamapori yanapelekwa Hazina ambako mgawanyo unafanyika kwenda kugharamia sekta mbalimbali zinazowanufaisha wananchi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa Wizara nyingine utaratibu huu wa mgao ndiyo unaofanya hata Wizara yangu kupata mgao kidogo kuliko mahitaji yake kiasi cha kushindwa kutimiza baadhi ya majukumu yake kama vile ujenzi wa miundombinu stahiki, kupata vitendea kazi vya kutosha na hata kushindwa kutoa maslahi stahiki kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari yote hayo na katika kutilia maanani kwamba sheria hii itaunda mamlaka ya wanyamapori ambayo inatarajiwa kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kifedha. Serikali itaweka utaratibu wa kulipa kifuta machozi cha kati ya Sh. 50,000 hadi Sh. 100,000 kwa ekari moja zisizozidi ekari tano ya mazao yaliyoharibiwa na wanyamapori na kiasi kisichozidi Sh. 500,000/= kwa mwananchi aliyejeruhiwa kwa ajili ya matibabu mbalimbali na kiasi cha Sh. 1,000,000/= kwa ajili ya mwananchi aliyepoteza maisha kutokana na wanyamapori hatari. (*Makofi*)

Utaratibu huu utabainishwa katika kanuni zitakazoandaliwa baada ya sheria hii kupitishwa aidha, hatua hii itakuwa ni ya mpito kabla ya kuanzisha mamlaka mpya itakayoandaa utaratibu mpya wa kuboresha zaidi kifuta machozi na fidia, malipo haya ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa bima maalum kwa ajili ya kufidia mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hatua hiyo, Serikali imeweka mikakati ya kupunguza uharibifu wa mashamba kwa kuweka vipengele vya sheria vitakavyowezesha usimamizi bora wa maeneo yenye wanyamapori wengi. Njia za mapito ya wanyamapori na maeneo ya kuzaliana. Maeneo haya yatalindwa na wananchi kwa kushirikiana na Serikali kwa kuhimiza uanzishwaji wa maeneo ya jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori na kuweka mazingira ya kuendesha shughuli za utalii wa picha kama vile

ujenzi wa kambi za utalii ambazo mapato yake yatakuwa ni manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchukua hatua hizo Serikali ina imani kwamba kwa ushirikiano wa wananchi athari za kuharibiwa mazao na wananchi kushambuliwa na wanyamapori zitapungua. Hivyo, pale itakapotokea kwamba zinatokea athari za uharibifu wa mashamba Serikali italipa kifuta machozi kwa utaratibu ambao utakuwa umebainishwa kwenye kanuni kama nilivyoeleza awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la ushiriki wa Watanzania katika matumizi ya wanyamapori. Kwa vile uwindaji wa kitalii umekuwa ni gumzo kubwa katika mjadala wa Muswada huu, Serikali imeweka mkakati wa kuhakikisha kwamba Watanzania wanakuwa na nafasi kubwa ya ushiriki kwenye biashara hii. Hali hii imebainishwa kwenye sheria katika kuhakikisha kwamba wananchi wenye uwezo wanaendesha shughuli za uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wawindaji bingwa wa Kitanzania ambao walikuwa hawajapata fursa ya kisheria kushiriki kwenye tasnia ya uwindaji wa kitalii watapata ajira na Serikali kujihakikishia mazingira mazuri zaidi ya kukusanya maduhuli kutokana na tasnia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia juu ya matumizi ya silaha za moto. Katika hili ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika miaka ya karibuni kumekuwepo na wimbi kubwa la majangili wanaotumia silaha za kivita ambazo zimesababisha madhara makubwa na hata vifo kwa watumishi wa sekta ya wanyamapori na wananchi kwa ujumla. Katika kutafakari hali hii Serikali imebaini kuwa, japokuwa kipo kikosi dhidi ya ujangili lakini sheria iliyopo ya wanyamapori haijaainisha uwezo na stahiki zake. Kwa mfano, bila kupata kibali maalum sheria iliyopo hairuhusu kikosi hiki kutumia silaha za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imesababisha ugumu katika kukiwezesha kikosi hiki kupata mafunzo na vitendea kazi stahiki vya kufanikisha majukumu ya kupambana na majangili hususan wanaotumia silaha za kivita. Kwa msingi huo Muswada wa sheria hii unatoa fursa ya uanzishwaji wa kikosi maalum kitakachoweza kupata mafunzo na vifaa maalum na ambacho kisheria kitafanya kazi katika mfumo wa kijeshi katika kupambana na majangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo napenda kuwaondolea Waheshimiwa Wabunge wasiwasi kwani silaha za moto zinalenga kupambana na majangili wenye silaha za kisasa na kwamba matumizi yake yatakuwa ya makini kulingana na mafunzo na utaratibu unaotumiwa na vikosi vingine kama Jeshi la Polisi. Kwa hali hii usalama wa raia wema utalindwa ipasavyo na ndiyo maana matumizi ya silaha ya moto yana masharti na tahadhari zilizowekwa bayana kama ilivyo sheria ya Jeshi la Polisi. Kwa utaratibu huu tuna imani tutaweza kupunguza kwa kiwango kikubwa tatizo la ujangili unaosababishwa na majangili wanaotumia silaha kali na hivyo kulinda rasilimali ya wanyamapori kwa faida ya wananchi na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kusisitiza kwamba, wananchi wasiwe na wasiwasi kwani Askari hawa wamepewa mafunzo na pia kuna masharti ambayo wamewekewa hawawezi kuua mtu bila sababu na dhamira kubwa ni kupambana na majangili na kwa hali hiyo na sisi kama Wizara tutaweka taratibu kwenye kanuni ya kuhakikisha kwamba wananchi pia wanapewa semina na elimu ya kuweza kutahadharishwa na kuelekeza kuhusu matumizi ya maaskari hawa ili kwamba wasiwe na hofu hata kama kwa bahati ameingia kwenye mbuga au ameingia kwenye sehemu hizo asiwe na hofu ya kukimbia kwani hawa maaskari hawataweza kumuua au kumjeruhi raia mwema ambaye hakimbii isipokuwa wenyewe wanapambana na majangili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi huo sasa nianze kujibu hoja moja baada ya nyingine kama zilivyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge. Nitaanza na hoja za Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Mheshimiwa Fuya Kimbita ambaye alikuwa ni Msemaji wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira alitoa hoja tatu.

Hoja ya kwanza, Wizara ishirikiane na Wizara ya Ardhi kuondoa migongano kwenye vijiji, kwenye hati ya ardhi hasa katika maeneo yenye mapori tengefu. Majibu ni kwamba, suala la migogoro ya mipaka ya vijiji na mapori tengefu limeshazingatiwa kwenye Muswada huu na marekebisho yatafanyika kwenye mipaka ya mapori tengefu mara baada ya sheria hii kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Wizara iharakishe utungaji wa kanuni mpya baada ya sheria kupitishwa. Mchakato wa kutayarisha kanuni mpya utaanza mara moja baada ya Muswada huu kupitishwa na kuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, mikataba ya maliasili na utalii ambayo Serikali inategemea kuingia iwasilishwe mbele ya Kamati ili itoe mapendekezo yake. Jibu ni kwamba, mikataba ya maliasili na utalii ambayo Serikali inaingia, itaendelea kufanywa kwa mujibu wa sheria na taratibu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambaye Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani alikuwa na michango ifuatayo: Sheria iainishe wazi majukumu ya Mkurugenzi wa Wanyamapori yatakayohamia chini ya Mamlaka hiyo. Jibu, lake baada ya mchakato wa kuanzisha mamlaka kukamilika sheria itafanyiwa marekebisho ili kuainisha majukumu ya mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Serikali ishirikishe jamii katika ulinzi wa wanyamapori na Wizara iboreshe mfumo wa utendaji kazi kwenye mapori ya akiba kwa kuweka vitendea kazi vya kutosha na usimamizi makini. Jibu lake ni kwamba, Wizara inashukuru kwa ushauri huu na inaendelea kuwashirikisha wananchi katika shughuli za uhifadhi kwa njia mbalimbali ikiwemo wa uanzishwaji wa maeneo ya jumuiya ya hifadhi za wanyamapori yaani *WMAs*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine inahusu ibara ya 18(2)(b), sehemu ya faini kuongezwa maneno *thousand* baada ya maneno *hundred*. Napenda nikiri hilo ni kosa la kimaandishi na uchapishaji, tumepokea ushauri huu tutaweka marekebisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine Serikali ijenge uwezo wa *WMA* katika nyanja mbalimbali ili kusaidia wananchi kutumia rasilimali iliyopo kupambana na umaskini na kuongeza pato la Taifa. Kwa sasa Serikali imekwishaanza kutoa hali ya matumizi ya rasilimali za wanyamapori kwa maeneo ya jumuiya ya hifadhi za wanyamapori sambamba na kuanza kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine inahusu ibara ya 31(1), tathmini za mazingira zitakazofanyika zifanyike kwa kuzingatia uhifadhi na maslahi ya Taifa. Serikali imepokea ushauri huu na itazingatia ushauri huu kwa kadri itakavyowezekana na kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Mwanawetu na Mheshimiwa Gosbert Blandes, hawa walikuwa na hoja iliyofanana inayosema kwamba Serikali ianzishe mchakato wa kuanzisha mamlaka ya uhifadhi wa wanyamapori mara baada ya Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2008 kupitishwa. Jibu, hiyo ndiyo dhamira ya Serikali, hivyo baada ya Muswada huu kupitishwa kuwa sheria mchakato wa kuanzisha mamlaka hiyo utaanza mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Raynald Mrose, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia na Mheshimiwa Lucy Owenya, hawa walikuwa wote wana hoja moja ambayo ilikuwa inasema kwamba Serikali ilipe fidia halisi ya madhara yaliyosababishwa na mnyama husika

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu kama ifuatavyo: Kimsingi ni vigumu kulipa thamani halisi ya binadamu kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali kwa sababu ya uthamani ulivyo na heshima ya utu wa binadamu na roho ya binadamu. Kutokana na ukweli kwamba huwezi kulinganisha maisha na uhai wa binadamu aidha kulingana na uwezo wa kifedha wa Serikali, kiwango kinacholipwa ni kifuta machozi au kifuta jasho, viwango hivi vimekuwa vikiongezwa kulingana na hali halisi ya uwezo wa Serikali na itaweka katika kanuni viwango kama nilivyoshauri wakati nilivyoongea katika Bunge la mwezi wa Novemba na pia leo wakati nilipoanza kuongea sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Mariam

Mfaki, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Gosbert Blandes na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha hawa wote ndiyo walikuwa katika hoja hiyo ambayo inasema kwamba Serikali ibakize asilimia kubwa ya fedha ya mapato kutokana na uwindaji wa kitalii katika mapori ya akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu kwamba Wizara yangu katika kipindi cha mpito kuelekea kuanzisha mamlaka itaendelea kuwasiliana na Waziri wa Fedha ili kuongeza kiwango ili kuhakikisha kuwa kiwango kinachotolewa katika bajeti *ceiling* ndicho kinacholetwa kwa ajili ya uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Blandes na Mheshimiwa Mwanawetu, wenyewe walikuwa wana hoja inayosema kwamba ibara ya 99 sehemu ya kwanza inaweka mzigo kwa mtuhumiwa kuonyesha kuwa ana hatia na hivyo kupingana na sheria nyingine za nchi. Napenda kujibu kwamba, kifungu hiki hakipingana na sheria nyingine. Utaratibu kama huu pia unatumika katika sheria nyingi za nchi, kwa mfano, Sheria ya Madini, sheria zinazosimamia miundo ya simu na pia na sheria mbalimbali ambazo zipo. Hata hivyo, napenda kuongeza kwamba, baada ya kutafakari jibu hilo tunasema kwamba badala ya kuendelea na kuweka mzigo mkubwa kwa mtuhumiwa tunapendekeza kwamba kuanzia sasa tutafuata sheria za kawaida za Mahakama zinazotumika kama kwenye kesi zenyewe badala ya kumwachia huyu mtuhumiwa ambaye yeye abebe lawama ya kuweza kujisafisha kwamba yeye hakufanya kosa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo na Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, wenyewe wanasema kwamba asilimia 25 ya mapato ya vijiji ni ndogo iongezwe hadi asilimia 60. Napenda kujibu kwamba, katika asilimia 100 za ada za wanyama wanaowindwa kitalii, asilimia 25 zinabakizwa kwenye mfuko wa kuhifadhi wanyamapori na asilimia 25 hupelekwa Hazina. Kati ya fedha zinazopelekwa Hazina asilimia 50 hurudishwa Wizara ya Maliasili na Utalii na asilimia 25 ya asilimia 50 iliyobaki hupelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kulingana na mwongozo uliopo asilimia 60 ya hizo fedha ya mapato haya Halmashauri yanapelekwa moja kwa moja kwa wenye vijiji ambavyo uwindaji umefanyika na asilima 40 hubaki Wilayani kwa madhumuni ya shughuli za uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha asilimia 25 kinatokana na aina ya wanyama waliowindwa. Kama wanyama hao ni wenye bei ndogo basi kiwango hicho huwa kidogo. Aidha, miaka mitatu iliyopita kiwango hiki kilikuwa kinawasilishwa Wizarani kutoka Hazina bila makato. Baada ya Hazina kuanza kupunguza mgao wa Wizara kiwango hicho pia kilipungua. Kwa sasa Wizara yangu inawasiliana na Hazina ili fedha hizo ziwe zinatumwa moja kwa moja kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Mgana I. Msindai yeye alikuwa na hoja tatu: Idara iendeshwe kijeshi, ianzishwe mamlaka ya kulinda wanyamapori, idara ya

Serikali ishughulikie sera na sheria. Napenda kumjibu kwamba ushauri huu unazingatiwa katika Muswada huu hususan ibara ya 9 ambapo inapendekezwa kuunda kikosi ambacho kitafuata muundo wa *paramilitary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine alisema *village game scout* waanzishwe nchi nzima na jibu ni kwamba, utaratibu huu utaendelea kufuata mfumo wa *WMAs*, pale ambapo *WMAs* zitaanzishwa, kutakuwepo na *village game scouts*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine idara ya wanyamapori itolewe kwenye Halmashauri za Wilaya na iendeshwe moja kwa moja na Mkurugenzi wa Wanyamapori. Napenda kujibu kwamba Wizara yangu itaangalia mfumo mzima wa usimamizi wa wanyamapori waliopo nje ya Hifadhi za Taifa na Ngorongoro wakati wa mchakato wa kuanzisha mamlaka ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hasnain Dewji alikuwa ana hoja zake tano, ya kwanza inahusu ibara ya 17, sehemu ya kwanza, sheria iwabane wanaochoma moto na watoe fidia za hasara za moto huo na faini iwe kubwa. Napenda kujibu kwamba, Muswada huu unahusu moto unaochomwa ndani ya hifadhi za wanyamapori. Aidha, moto unaochomwa nje ya maeneo hayo zipo sheria nyingine hususan Sheria ya Misitu, Sura ya 223, ambazo zinazuia na kutoa adhabu kwa kosa linalohusiana na kosa na la uchomaji moto hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake nyingine Serikali iwe inatoa nyama kwa wanakijiji ili kupunguza uharibifu angalau mara tatu kwa msimu. Napenda kujibu kwamba kupitia utaratibu wa *WMA* Serikali itaendelea kutoa mgawo wa wanyamapori ambapo wananchi watapanga utaratibu wa kuwinda wanyamapori hao kwa ajili ya kitoweo na uwindaji wa kitalii wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake nyingine ni elimu itolewe kwa wananchi kupitia *WMA*. Napenda kusema ushauri huu umepokelewa, aidha Muswada huu umezingatia suala la utoaji elimu kwa umma katika Ibara ya 97.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni Waziri atoe maelezo Serikali ina mpango gani wa kuongeza *game wardens?* Napenda kujibu kwamba mchakato wa uanzishwaji wa Mamlaka umelenga kutafutia ufumbuzi wa tatizo la uhaba wa watumishi na kuboresha mishahara yao. Kwa hiyo, Mamlaka itakapoanzishwa Mamlaka ndio itakayopanga hayo yote na kuweza kuyashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Castor Ligalama, ana hoja mbili na anasema wananchi wapate fidia ya malipo kwa kuwalinda wanyama kama ilivyo kwa madini, ambapo ametoa na mfano kwamba madini wanapewa *USD 200,000* kwa mwaka. Napenda kujibu kwamba Wizara ina utaratibu wa kutoa 25% ya mapato yanayotokana na uwindaji wa kitalii kwa Halmashauri za Wilaya ambazo uwindaji umefanyika na pia miradi ya ujirani mwema iliyo chini ya *TANAPA*, Ngorongoro na *TWPF* inalenga katika mwananchi kunufaika zaidi na rasilimali za wanyamapori. Mapato haya husaidia katika shughuli za maendeleo za vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ya Mheshimiwa Ligallama ni Serikali iajiri *game scouts* katika vijiji. Napenda kujibu kwamba utaratibu wa ulinzi wa wanyamapori kwa kutumia *game scouts* unafanyika katika maeneo ya jumuiya ya hifadhi za wanyamapori. Wananchi wanahimizwa kuunda jumuiya hizi ili kusaidia kuajiri *Village Game Scouts* kulinda rasilimali za wanyamapori na kufaidika zaidi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, alikuwa ana hoja tano. Hoja ya kwanza inasema, kupanuliwa kwa mipaka ya pori la akiba la Mpanga Kipengele na kujumuisha Kata za Luduga na Wangama katika Wilaya ya Njombe kunasababisha wananchi wakazi wa Kata husika kuishi kwa wasiwasi na mateso makubwa, Serikali irudishe mipaka ya zamani. Napenda kusema kwamba pori la akiba la Mpanga Kipengele, limeanzishwa kisheria kwa tangazo la Serikali la namba 483 la mwaka 2002 wakati zoezi la kuweka mipaka lilithibitika kwamba kuna baadhi ya vijiji vimo ndani ya hifadhi. Ili kutatua tatizo hilo Serikali itashirikiana na wadau kupitia upya mipaka hiyo ili kuhakikisha kuwa maeneo ya vijiji husika yanakuwa nje ya pori husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake ya pili ni kuwa, wananchi wanalipwa fidia kidogo. Hili ni kama nilivyoanza kwa kuongelea kwamba, kwanza kuna matatizo mengi mojawapo likiwa ni uwezo wa Serikali, lakini pia tumeona kwamba kwa sababu tutaingia kwenye Mamlaka, Mamlaka yenyewe itaendelea kupanga jinsi itakavyoona. Kwa sasa hivi kwa kipindi cha mpito sisi tumeongeza kiwango cha kufikia kama nilivyokieleza hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake nyingine ni *wildlife corridors*, vijiji vya Ndembwe na Lyankana, Serikali iimarishe njia hizo kwa kutoa hela ili zihifadhiwe vizuri. Napenda kwamba, suala la mapito ya wanyama na maeneo ya mtawanyiko, vimeainishwa katika Muswada ambapo Waziri atayatambua maeneo hayo na kwa kushirikiana na wadau atasimamia na kuyatungia kanuni za kuyahifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hoja yake nyingine ni kwamba, ni lini Serikali itapeleka wanyama Mpanga Kipengele ili kuongeza wanyama? Napenda kujibu kwamba, Serikali inasisitiza uhifadhi wa wanyamapori katika maeneo yao ya asilia na inaendelea kuhimiza uhifadhi wa asili katika pori la Mpanga Kipengele ili kuongeza idadi ya wanyama wa asili walioko hapo kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake ya mwisho kuhusu suala la miundombinu kama vile umeme, uwanja wa ndege wa Ilembula viboreshwe, Makao Makuu ya Mpanga Kipengele pia alikuwa anahoji yako wapi? Napenda kumjibu kwamba Wizara kwa kuona umuhimu wa Kiwanja cha Ndege cha Ilembula imeanza kukitengeneza ambapo fedha taslimu sasa hivi shilingi milioni saba za awamu ya kwanza zimetumwa na fedha za awamu ya pili shilingi milioni kumi na mbili zitatumwa ili kukamilisha ukarabati wa uwanja huo. Makao Makuu ya Mpanga Kipengele, yako Ilembula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Dokta Slaa, ambapo aliulizia kuhusu Ibara ya 115, sehemu ya kwanza mpaka sehemu ya sita.

Napenda kutoa jibu kwamba ni kweli dhana ya *Compounding of Offences* ni dhana inayohitaji uadilifu mkubwa katika utekelezaji wake. Kwa kuzingatia uzito wa dhana hiyo na muundo wa Idara ya Wanyamapori, inapaswa kutekelezwa na Mkurugenzi wa Wanyamapori kama ilivyo katika Sheria za Serikali za Mitaa ambapo Mamlaka hiyo ipo kwa Wakurugenzi. Sharti kubwa la *Compunding of Offences* ni kukiri kosa, hivyo basi bila ya ridhaa ya mtuhumiwa huwezi kutekeleza utaratibu huu. Tunamwahidi Mheshimiwa Mbunge, kuwa tutakuwa waangalifu katika utekelezaji wa eneo hili, hususan namna ya upatikanaji wa ridhaa ya mkosaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa sehemu ya pili napenda kujibu kwamba, utaratibu huu ni muhimu sana kuwepo kwani unapunguza muda na gharama kubwa za kusimamia suala hili na kuendesha kesi Mahakamani. Hata hivyo, bado mtuhumiwa anayo haki ya kukataa utaratibu huu na kutaka suala lake lifikishwe mbele ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu, napenda nijibu, ili utaratibu wa *compounding of offences* ukamilike, ni lazima risiti au stakabadhi itolewe kwa mkosaji kama inavyoainishwa katika Ibara ya 115(2)(c) ya Muswada. Kutokuwa na stakabadhi ni kosa na linapotendeka mhusika anapaswa kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 105(4) ina dhana ambayo naomba niinukuu inasema: "*It shall be lawful for any authorised Officer to stop and detain any person who he sees doing, or suspects of having done, any act for which the licence permit, permission or authority is required under the provision of this Act for the purpose of requiring such person to produce the same or to allow any vehicle, vessel or air craft of which he is the owner or over which he has control to be searched.*" Napenda kusema kwamba, dhana ya ibara hii ni kuruhusu kumzuia, kumkamata mtu au chombo cha usafiri kwa dhamira ya kuonesha leseni, kibali, ruhusa au mamlaka kwa ajili ya uhakiki au uhalali wa matendo au shughuli yake katika eneo husika au kufanya upekuzi katika chombo cha usafiri na si vinginevyo. Haikusudii kumtia mtu hatiani kama mtendaji wa kosa. Hii ni kuhakiki tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia alizungumzia Ibara ya 102 ambayo iko ukurasa wa 68. Napenda kujibu kwamba dhamira ya Ibara hii ni kuhakikisha kuwa pale mtu anapokuwa na silaha katika maeneo husika haitumii silaha hiyo kinyume cha sheria inayopendekezwa. Kinachotakiwa ni kuithibitishia Mamlaka kuwa haitatumika au haikutumika kinyume cha sheria. Suala hili hujitokeza pale tu kunapokuwa na dalili za uvunjaji wa masharti ya sheria hii kwa kutumia silaha hiyo ambayo mtu anakutwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo napenda nijibu hoja ya Mheshimiwa Zitto Zubeir Kabwe, ambapo alisema kwamba, Miswada inayogusa rasilimali za maliasili inapaswa kuwa inafanyiwa *impact studies* kubainisha *impact* mbalimbali za Miswada hiyo. Napenda kusema kwamba ushauri huu umepokelewa na tumeukubali na tutauzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake nyingine alihitaji takwimu za mapato ya uwindaji kwa Halmashauri za Wilaya zilizo Mkoa wa Kigoma kwa miaka mitatu

iliyopita. Napenda kusema kwamba, Mheshimiwa Zitto Kabwe, takwimu hizi nimekuorodheshea na ninazo hapa, kwa sababu muda ni mdogo, naomba nikukabidhi baada ya kumaliza hapa lakini ninazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Estherina Kilasi, yeye alitoa pendekezo lake la kuunganisha Ibara ya 37 na sehemu ya 3 na moja ya majukumu ya Mamlaka iwe ni kugawa vitalu. Napenda kusema kwamba Mamlaka itakayoundwa, itaratibu masuala yote ikiwa ni pamoja na kugawa vitalu. Napenda nirudie tena kwamba, Mamlaka ikishaundwa kazi nyingi ambazo sasa hivi zinafanywa na Mkurugenzi wa Wanyamapori, zitahamia kwenye Mamlaka na pia hata watumishi watahamia kwenye Mamlaka na halikadhalika hata shughuli za ugawaji vitalu zote zitahamia kwenye hiyo Mamlaka, hazitakuwa tena ziko chini ya Kamati ya Ushauri au chini ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Raynald Mrope na Mheshimiwa Lekule Laiser, walitoa hoja zao mbili zilizofanana. Kuna haja ya kufanya *Regulatory Impact Assessment* ili kutambua faida na athari ya sheria tunayounda ili kujiandaa kwa yatakayotokea, kwa mfano kuvuruga biashara ya uwindaji wa kitalii. Napenda kusema kwamba Serikali inapokea ushauri huu na tutaufanyia kazi kuhusu mambo ya *Regulatory Impact Assessment* ili kutambua athari na kuwasilisha mapendekezo yoyote yatakayopatikana hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hoja yao nyingine ilikuwa ni wananchi watakaopewa vitalu wapewe elimu na wawezeshwe kifedha ili waweze kuuza safari na kujitangaza. Napenda kujibu kwamba, Wizara haina uwezo kifedha kwa ajili ya kuwawezesha wananchi watakaopewa vitalu. Aidha, Wizara itatoa elimu na ushauri wa kuwaelekeza wahusika kwenda kwenye vyombo vya fedha kupata mikopo na kuweza kuwezeshwa kwa shughuli kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdallah Mtutura na Mheshimiwa Mwanawetu, wana hoja mbili ambazo zimefanana nazo ni moja, kuhusu Ibara ya 71 (2), vyeo vilivyotajwa hakuna cheo cha Afisa Mtendaji. Napenda kusema kwamba Ibara hii inahusu mnyama aliyejeruhiwa na kukimbilia kwenye maeneo ya hifadhi na si mnyama aliyekimbilia katika ardhi za vijiji au kusababisha madhara kwa wananchi.

Hivyo, watu waliotajwa katika Ibara hii ni wale tu wenye mamlaka katika hifadhi tajwa. Ndio sababu hawakuwekwa Maafisa Watendaji kwa sababu hii ni kazi ya kitaalam na ndio sababu wamewekwa wale wataalam ambao wana uwezo wa kushughulikia hawa wanyama na ikibidi kuwaswaga au kuwauwa ili waweze kwa sababu wana madaraka hayo. Swali lao la pili ni ufafanuzi wa Ibara ya 2 ya Sheria kuwa, itatumika Tanzania Bara, hakuna sehemu iliyotafsiri Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yao ya pili walisema kwamba, Ibara ya 5(1)(a) inaongelea Tanzania na si Tanzania Bara. Napenda kujibu suala hili kwamba ili sheria itumike Zanzibar ni lazima iwe na masharti yanayotamka hivyo ili yatimize masharti ya Ibara ya 64(4) ya Katiba. Muswada huu kulingana na Ibara ya 2, utatumika na kusimamia uhifadhi wa wanyamapori Tanzania Bara tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Job Ndugai, yeye alichangia na kusema kwamba Idara iwezeshwe katika maeneo ya *anti pourching.* Tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, kwa maoni hayo na tumeupokea huo ushauri. Mheshimiwa Hasnain Gulammabas Dewji pamoja na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha pamoja na Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, wenyewe walikuwa na hoja moja ambayo inasema kwamba Serikali iboreshe mishahara ya *game wardens* na watumishi wote wa Idara. Napenda kujibu kwa kusema kwamba kuboresha mishahara hii kutatokana na uwezo wa Serikali wa kifedha.

Lakini hata hivyo, tutaendelea na mawasiliano na Waziri wa Fedha ambaye ndiye mwenye dhamana ya kushika fedha tuweze kuona hili tutaweza kulitenda namna gani. Lakini ni kweli kwamba watumishi hawa mishahara yao midogo na hata vivutio walivyonavyo ni vidogo na ni jambo ambalo tunalifahamu na tunajitahidi katika kila njia kulishughulikia na tumeupokea ushauri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Martha Umbula, ana hoja tano. Ya kwanza anasema, wananchi wanaozunguka hifadhi wanufaike nazo ili kupunguza mikwaruzo na migongano. Napenda kujibu kwamba utaratibu wa kuwawezesha wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye wanyamapori ikiwemo *WMAs* upo kwenye kanuni zilizopo hivi sasa na hata hivyo, kanuni hizo zitapitiwa upya ili kuziboresha baada ya Muswada huu kupitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo napenda kusema kwamba kuna baadhi ya mengi ambayo sikuyamaliza kwa sababu muda ni mdogo Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tumeyapokea na wote nitawapelekea kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 2008
### (*The Wildlife Conservation Bill, 2008*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye hatua inayofuata, hatua ya kuupitisha Muswada huu kama Kamati ya Bunge Zima na tutaendelea kuzipitia sehemu zote za Muswada huu na kuna majedwali yaliyoletwa na Serikali ya kufanya mabadiliko ya maeneo kadhaa ya Sheria hii. Kwa hiyo, nitamuomba Katibu atuongoze kama ilivyo kawaida yetu kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge, Katibu.

Ibara ya 1

Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Niliwasilisha *schedule of amendments,* lakini kabla ya hapo naanza na kifungu kidogo cha (13). Katika kifungu hicho Rais wa nchi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anapewa Mamlaka ya kutangaza eneo lolote katika nchi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sendeka, twende taratibu. Unazungumzia kifungu cha ngapi?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kifungu kidogo cha (13).

**MWENYEKITI:** Cha kifungu kikubwa cha ngapi?
**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, cha (4).

**MWENYEKITI:** Hatuna kifungu hicho cha 13 Mheshimiwa Sendeka, bado hatujafika huko unakosema. Kifungu hiki cha (4) kina vifungu saba tu, hicho cha 13 chako wewe kimetoka wapi?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kiko *Part Four.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, fungu hilo linaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*

*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru hapa ndio mahali pake. Katika kifungu hicho kipya cha 14, Rais amepewa Mamlaka ya kutangaza sehemu ya Tanzania baada ya kushauriana na Mamlaka zinazohusika kuwa ni *game reserve* au pori la akiba.

Nilipokuwa nikichangia nilielezea juu ya tangazo namba 307 la kuundwa kwa Mkungunero *game reserve* ambayo ilikuwa imebainisha wazi kwamba Mkungunero *game reserve* itaishia mipaka ya Kondoa. Kwa bahati mbaya katika utekelezaji wake ilivuka mipaka ya Kondoa na mipaka ya Mkoa wa Dodoma na kuingia katika vijiji viwili kimoja cha Wilaya ya Kiteto cha Rikiwishbwar na kimoja cha Wilaya ya Simanjiro cha Kimotorok.

Baada ya kueleza vitongoji vile nilimuomba Waziri atoe tamko la kuhakikishia kwamba tangazo hilo lililotolewa na Rais litaheshimiwa na kwamba mipaka iliyotangazwa na Rais itaheshimika na kwamba ardhi ya vijiji vilivyovamiwa na pori hilo sasa irejeshwe kwa wananchi kwa mujibu wa sheria. Nilitaka maelezo ya Waziri katika hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, shida yako si kufanya mabadiliko ya kifungu hiki, lakini shida yako kubwa ni matumizi ya kifungu hiki katika hali halisi iliyojitokeza kwenye eneo lako. Sasa kwa sababu ni tatizo la hali halisi kwenye eneo lako Mheshimiwa Mbunge, nafikiri suala hili liletwe sasa katika taratibu zile nyingine za

Kibunge za kushughulikia kero za wananchi zinazotokana na kanuni na sheria ambazo tumezipitisha. Lakini kama hoja ya msingi ingekuwa ni kurekebisha kwamba hukubaliani na kifungu hiki kwamba Rais asiwe na Mamlaka ya kufanya hivyo, hiyo ndio ingekuwa ni hoja rasmi hapa Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi).*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 16

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu kipya cha 16 nimeleta marekebisho yafuatayo: Kwanza nilikuwa nimeomba tafsiri ibainike ya maneno *Relevant Authority,* ambayo imetumika kifungu hicho cha 16 kipya kifungu kidogo cha (4).

Lakini ili kuepusha mkanganyiko niliomba pia kwa mujibu wa kifungu hicho yafanyike marekebisho ili kuhakikisha kwamba Waziri, badala ya kupitia orodha ya mapori Tengefu, Muswada ufute kwanza miongozo au *Regulation* iliyoanzisha mapori hayo ili yatambulike upya kwa mujibu wa kifungu hiki kipya na nikapendekeza hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sendeka, hapo tunakwenda sawasawa. Mheshimiwa Waziri, naomba maelezo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukiri kwamba Mheshimiwa Sendeka, alileta marekebisho hayo na tumeyajadili na tukakubaliana kwamba katika lile ambalo alisema *Relevant Authorities. S*asa kwa sababu neno *Relevant Authority* ni neno pana ambalo linaweza kutumika katika mambo mengi na *Relevant Authority* sasa inaweza ikatumika katika ngazi ya mpaka kwa Rais, ngazi ya Mkoa, ngazi ya Wilaya na mpaka Ngazi ya Vijiji. Tulikubaliana kwamba, tukiliweka hilo litakuwa lina maana zaidi kuliko tukilibadilisha, ina maana kwamba ikiwa wenzetu wa Wizara ya Ardhi au Wizara ya *TAMISEMI* wakiweka marekebisho tutajikuta kwamba tutashindwa kufanya kazi. Kwa sababu kisheria tumeona hili neno ndio ambalo linafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu tukishapitisha sheria ya Mamlaka yeye alipendekeza kwamba tufute ili tuweze kuanza kuvi-*register* upya. Lakini sasa tunasema kwamba, kuvifuta na kuvi-*register* upya itakuwa ni kazi ambayo ni tofauti na ile iliyodhamiriwa na tukakubaliana kwamba tufanye tunachofanya kwa sababu Serikali inajua *game controlled areas* zote na inajua hizi *game controled areas* zote ni zipi ambazo zinakaliwa na ni mali ya vijiji na ni zipi ambazo sio mali ya vijiji.

Sasa ni ile tu kwamba Serikali tutachukua jukumu letu kuweza kuvipitia vyote upya ili tutenganishe vile ambavyo ni vya vijiji na *controlled area* ile ambayo inakaliwa

na vijiji, ndio hiyo tunaitoa na wanaendelea nayo wenyewe na ile nyingine ni kwamba tutaanza kuendelea kuimiliki namna hiyo.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Waziri ameweka kwenye *Hansard* kwamba tafsiri itaendelea kubaki hiyo *Relevant Authority* kwa maana kwamba pale ambapo itahusu ardhi za vijiji basi maeneo hayo itabidi ipatikane *consent* au idhini ya Mamlaka hayo basi sitakuwa na ugomvi ikiwa imekuwa *recorded* hivyo, nakubaliana nayo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ile 17 mpya nadhani sasa ndio ile *section* ya tano inayohusu *Foreign Livestock*, nadhani tuko pale. Kwa vile imeleta mkanganyiko *foreign livestock* ni kitu gani...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, Waheshimiwa Wabunge naomba tuende taratibu, kifungu cha 17 kina sehemu tatu tu hakina sehemu tano. Sasa sehemu hiyo ya tano nadhani utaikuta mbele kwa sababu vifungu hivi sasa vimekuwa vikibadilishwa badilishwa.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sio ukurasa wa 23 eeh?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hicho kipya cha 17, kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo cha (5) ambacho kinaanza na *Notwithstanding....* inaishia na *involving foreign livestock.* Kuna uwezekano wa watu ku-*translate foreign* kwa kumaanisha kwamba hata ng'ombe wanaotoka Ihefu wakija Ludewa sisi watu wa Ludewa tutawaita ni *foreign livestock,* yawezekana kwamba hatuna maana hiyo. Nilidhani neno *foreign livestock* lingetolewa ufafanuzi au *definition* ili liweze kueleweka lina maana gani kama halijafanyiwa hivyo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuupokea ushauri wake na kwenye *amendment* hiyo ipo na hapa tulichomaanisha ni mifugo inayotoka nchi za jirani.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 22

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *schedule of amendments* niliyokuwa nimeiwasilisha niliendelea kukumbushia suala la *relevant authority* kwa maana moja tu kwamba, katika kifungu hicho inapendekezwa kuwepo kwa uanzishwaji wa maeneo ya mazalia na maeneo ya mtawanyiko.

Kwa kuwa maeneo haya yatakuwa kwenye ardhi za vijiji, namshauri Waziri, baada ya kukubaliana na pendekezo alilokuwa amelitoa kwamba kwenye *regulations* atakazokuwa amezitoa abainishe hizo *relevant authority* iendelee kuwa ni mikutano mikuu ya vijiji kama ilivyo kwenye Sheria ya Ardhi na hii itaweka bayana kuwashirikisha wananchi kwenye ardhi inayobadilishwa matumizi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukubaliana na Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba tutafanya hivyo. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27

Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 32
Ibara ya 33

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sisikii sasa kama mnakubali hivyo vifungu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 35

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu nilizungumzia kuhusiana na utaratibu unaotumika hivi sasa wa mwekezaji kulipa fedha kwa ajili ya kufanyiwa *Environmental Impact Assessment* na nikaeleza kwamba, utaratibu huu umekuwa unatoa mwanya kwa wawekezaji kuweza kushawishi na hivyo kuweza kupitishiwa mapendekezo yao hata pale ambapo hapastahili. Kwa hiyo, napenda Serikali itoe tamko kwamba, utaratibu huu utafanyika vipi ili kuweza kuondoa mianya hiyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni utaratibu wa Wizara ya Mazingira na mimi nimeupokea, nitampelekea mwenzangu kwa ajili ya suala hilo. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya*

*Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilizungumzia kuhusu kifungu cha 37(2) kwamba, Mwenyekiti wa ile Kamati asitokane na Watumishi wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shelukindo, kifungu cha 37 hakina *part one* wala *part two.*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Hiyo *amendment* nimeitafuta katika zote nilizonazo sijaiona, sijui labda nipewe maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shellukindo, hebu subiri utakutana nacho huko tunakoendelea, sasa hivi siwezi kuanza na maelekezo tena.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, asiwe na wasiwasi, nataka tunyooshe mambo katika jedwali la Serikali la tarehe 28 Januari, ukurasa wa nne (k), ndiyo eneo hilo ambalo limefanyiwa marekebisho na Serikali na kwenye (a) wakaongeza ibara mpya ndogo ya 17.

Sasa katika mpangilio, jedwali la Serikali lilitolewa asubuhi hii, kwenye ibara hiyo ya 38(b) tunapofanya *renumbering*, hatufikii katika idadi ya ibara ndogo, tunaishia katika 15. Mimi ninaamini zipo zaidi ya hapo, tusipofanya hivyo, tutawakanganya sana waandishi wakati tunakamilisha zoezi hili. Nilikuwa nashauri, kwa mpangilio huo, *renumbering* sasa hivi itatupeleka kuanzia ibara ndogo ya 8, 9, 10, 11, 12, 13, 14, 15, 16 na mwisho 17, ndiyo tutakuwa tumekaa vizuri katika eneo hilo. Tusipofanya hivyo, kuna *confusion* kubwa kati ya *schedule of ammandments* hizi mbili.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea na nimekubali kwamba, tutazingatia hiyo. Kwa ruhusa ya Waheshimiwa Wabunge, sisi tutaweza kuirekebisha wakati hawa wataalam watakapokuwa wanatengeneza kamili.

**MWENYEKITI:** Tunaipitisha hapa tunagemea sheria yetu itaonekana kwa mtazamo huo.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sijamalizia katika kifungu kipya cha 17(a), ambacho kinasema: *such person has company registered with the Registrar of Companies,* hii ni lugha inayoeleweka lakini kwa uandishi wa sheria na hiki namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hakitabadilisha maana ila kinaboreshwa tu; kwa nini tusiseme *such person owns shares in a company*, ndiyo

utaratibu huo? Huwezi kusema *has company,* ana kampuni, *owns shares in a company.* Vilevile (b) tuseme; *such company attempt to engage in hunting of animals*, maana *hunting* unaweza kufanya lakini tunalenga katika maeneo ambayo ni mahususi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Chenge, tunakubali hayo masahihisho. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho cha 38 kipya, kifungu kidogo cha 6, umewekwa utaratibu wa namna ya ugawaji wa vitalu vya kuwindia, lakini baada ya Waziri kushauriwa na Kamati ile ya Ushauri, Waziri anachukua mamlaka yake ya kugawa maeneo.

Sasa nilichokuwa nasema, pale ambapo kitalu cha kuwindia kipo kwenye ardhi ya vijiji, mamlaka zinazohusika katika maeneo haya ya vijiji, ziweze kushirikishwa kama *schedule* of *amendment* inavyoonekana. Ninadhani Waziri atakumbuka, kwenye Kamati tulikubali, lakini ninataka iwe *recorded* hasa pale tunapoongeza *where hunting blocks are within any village land, the Minister shall in consultation with relevant Authority and upon advice by the Committee, allocate a hunting block to the applicant.* Nilifikiri kama Waziri atakubaliana na mimi kwenye pendekezo hilo, basi itakuwa imesaidiana sana kuhakikisha kwamba, vijiji na maeneo ambayo *hunting blocks* hizo zipo basi wanaweza kushirikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo marekebisho niliyoyawasilisha.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli kwamba, tukishawapa wanavijiji zile *controlled area*s, zikiwa chini yao, kuna baadhi tulipendekeza kwamba waingie kwenye *WMA.*

Mheshimiwa Mbunge alisema kwamba, kuna baadhi watakuwa wameingia; je, wale ambao hawajaingia? Tukasema kwamba, wale ambao hawajaingia bado watakuwa na Idara ya Wanyamapori katika kipindi hicho cha mpito, watakuwa wanasaidia kukendesha mpaka watakapokuwa kwenye *WMA* watawakabidhi. Sasa Mheshimiwa Mbunge, ndiyo alitaka kuona kama idara itaendelea, basi kwa vyovyote vile wale wanakijiji wa sehemu husika, waweze angalau kuwa *consulted* nao wafahamu nani yuko pale na mambo kama hayo.

Hilo hatuna tatizo nalo na tumelikubali, lakini sasa ikawa kwamba; je, iwekwe wapi? Mimi nikasema katika kanuni tutakazozitengeneza, kwa sababu hicho kitakuwa ni kipindi cha mpito. Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Mbunge, tukubaliane kwamba, kwenye kanuni nitahakikisha hiyo imewekwa. Kwamba, MkurugEnzi wa Wanyamapori, kabla ya kugawa kitalu kwenye sehemu zile, bado wanavijiji hawajatengeneza *WMA*, ahakikishe kwamba, anawa-*consult* kijiji husika ili waelewe na wakubaliane nini kinaendelea kwenye kijiji chao.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, lakini bado nilikuwa nafikiri ipo haja, ardhi hii

ni ya vijiji, hapo kuna mahali *WMA* haijaanzishwa, unataka kumleta mwekezaji wa kumpa *hunting block* katika eneo hilo, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ni haki. Nilikuwa nafikiri hii iendelee kubaki; Muswada huu kwenye Sheria hii itajifia yenyewe huko tunakokwenda, baada ya *WMA* nyingi kuanza ili kutowanyima wananchi haki katika hili.

Inawezekana *regulations* zikaja kutungwa baada ya mwaka, miaka miwili na ikaendelea kupoteza muda na kutowapa wananchi, mamlaka ya kushiriki mchakato mzima wa kugawa vitalu. Ninafikiri kwamba ni haki ili wawekezaji hawa waweze kuwajibika pia na kuwaheshimu wale wanakijiji katika maeneo hayo.

Kwa hiyo, bado nilikuwa namshawishi Waziri, kama tulivyokubaliana kwenye Kamati, waendelee kuya-*accommodate* haya niliyoyapendekeza ili kuweza ku-*harmonize* kwa sababu halina mgogoro huko tunakoenda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nafikiri maelezo aliyoyatoa ni kwamba, kwa sababu hii itazingatiwa katika kipindi cha mpito na sheria itadumu kwa muda mrefu zaidi; sasa kama itawekwa kwenye kanuni, ina maana kwamba, itatumika kipindi cha mpito kuliko kuendelea kuibadilisha tena sheria baada ya kipindi hicho cha mpito. Bahati nzuri, nilikuwepo kwenye majadiliano ya mchana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 44

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu kile kuna masuala ya ku-*set quota* ambayo ni wanyama wangapi waruhusiwe kuwindwa, kwa wakati katika kitalu hicho. Nataka tu Waziri anithibitishie kwamba, ku-*set quota* kwa vyovyote vile lazima kutahusisha kujua namba za wanyama kwenye vitalu vile kwa kuwahesabu na sio kutumia utaratibu wa sasa, ambapo mara nyingi wana *estimate* wanadhani kuna wanyama kadhaa.

Kwa hiyo, kutokana na namba hiyo, unaweza ukawa-*harvest* wanyama kiasi fulani. Mara nyingi *estimation* hizo sio za kweli, zinasababisha kumaliza wanyama kwenye vitalu. Kwa hiyo, *quota* ziwe *set* kutegemeana na *statistics* ambazo zipo *based on counting*. Naomba anithibitishie na Hansard irekodi kama ndivyo watakavyofanya, itakuwa *based on counted animal not estimated animals*.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, kuwa hesabu wanyama ni *exercise* moja ambayo ni ngumu sana na ya gharama sana. Kwa hivi sasa, kufuatana na kazi ambayo tulikuwa tumepewa na Wabunge, mojawapo ilikuwa ni kuwaangalia upya wanyama, kuwahesabu na kuangalia vitalu vikoje. Hiyo kazi inatuchukua miaka miwili hivi sasa na pia ni ya gharama kubwa.

La pili, hao wanyama sio kama sisi binadamu, kila siku jioni unarudi kwenye nyumba yako; hawa wanyama wanasafiri leo wanaweza wakawa Ngorongoro, kesho wakazunguka Manyara, siku nyingine wakaenda kwa Ole-Sendeka Simanjiro, kwa hiyo ni wale wale. Sasa ukikaa kuwahesabu, ujue kwamba hawa kila siku wapo hivi sio rahisi. Tunachofanya kwa sababu baada ya kipindi kadhaa hesabu inafanywa, tunakuwa tunajua kwa kukisia kwamba, sasa hivi wanyama wapo kiasi kadhaa.

Tunavyotoa *quota* pia ile inatusaidia kwa mahesabu ya haraka kujua kwamba, baada ya kutoa *quota* kiasi hiki, wanyama wako wangapi, ingawa sio sahihi mpaka tutakapoweza kuhesabu moja kwa moja na ndiyo kazi ambayo inafanyika kila baada ya vipindi. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 45

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 46
Ibara ya 47

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 48

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye majedwali ya marekebisho ya Serikali yote mawili; ukurasa wa tano lingine ukurasa wa pili, nianze na ukurasa wa tano; imependekezwa kwa usahihi kabisa kwamba, tuongeze ibara ndogo mpya ya tatu na vile vifungu vidogo vilivyopo sasa hivi kwenye Muswada ukurasa wa 37 viwe 4 na 5, hakuna tatizo. Sasa kwenye *schedule of amendment* ya jana, ukurasa wa pili imependekezwa tuwe na kifungu kingine kidogo cha tano, ambacho kinasomeka: "*The preceding provisions of these section …*" Ninadhani isiwe *plural "of these section"* iwe

*singular*.  Kwa maana hiyo sasa, hiki kinachoonekana katika ukurasa wa pili, hakitakuwa cha tano bali cha sita.

La pili, ningelipenda tu nisaidiwe na Serikali; *transition period* ni ya muda gani, maana kwenye *schedule of amendment* hii, inaongelea ni miaka mitatu; *which is which?* Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu la kwanza linahusu *numbering*, kwa hiyo, inaweza kuzingatiwa na sio kubadili tena maana nyingine ya *schedule of amendment*.  Ya pili, Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi wa *transition period*.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 48 kinahusiana na mambo ya *professional hunting*, sijui kama ndivyo?  Ninataka kujua *period* hiyo au mimi ninasoma tofauti.  *Professional hunting transition period* ni kwamba, kwanza, naomba nikiri kwamba, mpaka sasa *professional hunters* wa Kitanzania tulionao hawazidi hata kumi. Kwa hiyo, hata kusema kuanza sasa hivi kuwawekea hiyo *transition period*, kwa sababu tunaingia katika awamu ya kutaka kuhakikisha kwamba, Watanzania wanakuwa *trained*, tuwe na *professional hunters* wengi iwezekanavyo.  Tukisema kwa sasa hivi labda ni hao kumi tu, ambao ndiyo wanaweza wakawa *available* na sijui kama itakuwa ni nyepesi kuwawekea *transition period*.

Kwa hiyo, kwa kitu hicho ndiyo yale mambo ambayo tangu mwanzo tulikuwa tunayaongea kwamba, *professional hunters* ni mpya kwetu na ni kitu ambacho watu wanahitajika wasome, waweze kuelewa na sio mwindaji yeyote yule anaweza akashika bunduki akawa *hunter*.  Ndiyo sababu ninasema, bado tuko nyuma kidogo, kuweza kuwa na *real professional hunters* wa kujitosheleza, mpaka sasa hivi wanapoingia katika mafunzo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56
Ibara ya 57
Ibara ya 58
Ibara ya 59
Ibara ya 60
Ibara ya 61
Ibara ya 62

Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67
Ibara ya 68
Ibara ya 69
Ibara ya 70

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 71

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho kipya cha 71(1), kinampa Waziri mamlaka ya kutoa kifuta machozi, baada ya kuwasiliana na Waziri wa Fedha, kwa wale ambao wameathirika na wanyama hao waharibifu, lakini mtu pamoja na mazao ya mifugo haikuigizwa.

Nimependekeza kwenye *schedule of amendment* kwamba, *livestock* iweze kuingizwa. Hilo ni pendekezo langu la kwanza, kutokana na ukweli kwamba, mifugo ndiyo inayodhurika zaidi na wanyama.

Lingine ambalo nililipendekeza kwenye *paragraph* ya pili, niliomba lifutwe hasa sehemu ile ambayo inaweka wazi kwamba, kwa namna yoyote ile kifuta machozi kisitambulike kama haki ya kufidia. Kwa hiyo, nimeleta marekebisho ili ile *paragraph* ya pili ifutwe, *provided that the amount shall not in whatever circumstances, be considered right or a compensation.* Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri hiyo ingefutwa. Nilipendekeza kwenye Kamati, kama Waziri atakuwa bado anakumbuka, haya mawili yakifanyika, sitakuwa na mgogoro na Muswada wenyewe.

**MWENYEKITI:** Ulipendekeza kwenye Kamati, lakini uli-*move* pia *schedule of amendment.*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, hayo yote nakiri nimeyaona na tumejadiliana. Ninapenda kusema, tumekubali kuongeza *livestock* na sababu tuliyokubali kuongeza ni kwamba, sasa hivi kuna mabadiliko tunayoyafanya; tunao baadhi ya wanavijiji ambao watakuwa wanaishi huko kwa wanyama na mazizi yao yanaweza yakawa huko huko. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile, simba anaweza akaingia akawaathiri, akaua wanyama; kwa hali hiyo, tukakubali kuongeza *livestock* katika sehemu kama hizo.

Vilevile tulizingatia mengi; napenda tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kuna ile mifugo ambayo haimo ndani ya sehemu hizi wapo nje huko, labda watajaribu kutaka kuingia kwenye sehemu kama hizo, wakipatikana na madhara yoyote,

hiyo ndiyo ambayo hatutaweza kulipa na katika vifungu mbalimbali humu tumeonyesha. Kwa hiyo, *livestock* kama ilivyo, tumekubaliana nayo na pia la kufuta hiyo nimekubali kwamba, tuna-*delete proviso* hatuna neno. (*Makofi*)

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza, nampongeza Waziri na timu yake kwa usikivu; kwa sababu *schedule of amendment* nyingi tulizozipeleka, ameweza kuzi-*accommodate* katika Muswada huu.

La pili, leo mchana wakati nachangia kwenye Bunge letu Tukufu na kwenye Kamati, nilijaribu kuweka masahihisho kwamba, hakuna kipengele ambacho nimezungumzia *compensation* ya *human life.* Bahati mbaya, Mheshimiwa Waziri, wakati anajibu hoja za Wabunge mbalimbali, ametaja jina langu miongoni mwa Wabunge ambao wamezungumzia *compensation* ya *human life*. Sasa ili *Hansard* iweze ku-*record* vizuri, Mtutura Abdallah Mtutura, hajazungumzia *compensation* ya *human life;* ni hilo tu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 72

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 73

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 74
Ibara ya 75
Ibara ya 76
Ibara ya 77
Ibara ya 78
Ibara ya 79
Ibara ya 80
Ibara ya 81
Ibara ya 82
Ibara ya 83
Ibara ya 84
Ibara ya 85
Ibara ya 86
Ibara ya 87
Ibara ya 88
Ibara ya 89

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 90

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kipya cha 90, napenda nihakikishiwe na Mheshimiwa Waziri, kama *regulations* atakazozitayarisha ni kwa ajili ya *activities* kama *wildlife ranching, wildlife farming* na kadhalika; kwa sababu ni mambo mapya haya, hivyo *regulations* zitakuwa ni pamoja na *Environmental Impact Assessment.*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia kwamba, *Environmental Impact Assessment* ni muhimu na ni ya lazima kabla mambo haya hayajatekelezeka.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 91
Ibara ya 92
Ibara ya 93
Ibara ya 94
Ibara ya 95
Ibara ya 96
Ibara ya 97
Ibara ya 98
Ibara ya 99
Ibara ya 100
Ibara ya 101
Ibara ya 102
Ibara ya 103
Ibara ya 104
Ibara ya 105
Ibara ya 106
Ibara ya 107
Ibara ya 108
Ibara ya 109
Ibara ya 110
Ibara ya 111
Ibara ya 112
Ibara ya 113
Ibara ya 114
Ibara ya 115

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge*

*Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 116

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 117
Ibara ya 118

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 119

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 120
Ibara ya 121
Ibara ya 122

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1
Jedwali la 2
Jedwali la 3

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 4

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo katika hiyo *schedule* ya nne, ambayo inawataja wanyama hatari. Kwa kuwa kwenye *interpretation* sikuona tafrisi ya mnyama hatari, mimi ninataka nipate ufafanuzi tu; ni vigezo gani vilivyotumika ku-*classify* mnyama hatari na kilichopelekea Mbwamwitu na Nyoka kunusurika katika *schedule* hii na kama kweli wanastahili kuwepo katika *schedule* hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwa kifupi tu; katika tafsiri ambayo tumeorodhesha humu ni kwamba, wale wanyama wakali ambao wanaweza wakamshambulia mtu bila

kuchokozwa. Nyoka hawezi tu akakukimbilia akakugonga labda umkanyage na kama kuna Nyoka ambao wanagonga nadhani ni wachache lakini wengine hawafanyi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimlinde, hoja ina mwenyewe. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba ni wale wanyama ambao wanaweza wakamshambulia mtu bila kuchokozwa. Sasa labda kama kuna Waheshimiwa Wabunge wengine, wanawafahamu wanyama ambao kweli bila kuchokozwa zaidi ya hawa ambao sisi tumewaorodhesha Kisayansi, tunaomba watuletee orodha ya wanyama hao. Wakituletea tutafanya utafiti na mambo mbalimbali, kuweza kuona kama nao wanaweza wakaingizwa kwenye jedwali hilo wataingizwa. Ahsante.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumzia Nyoka na Mbwamwitu; Mbwamwitu naye mpaka achokozwe jamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kidogo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hilo nililosema kwamba, zaidi ya hili jedwali tulilonalo, sisi nimetoa pendekezo kwamba Mheshimiwa mwingine yeyote, kama anawafahamu wanyama wengine wakiwemo Mbwamwitu, Nyoka na kadhalika, ambao kweli bila kuchokozwa wanaweza kumshambulia mtu, walete majina hayo, tupo tayari kwa majadiliano na kufanyia utafiti tuwaingize. *(Makofi)*

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 5
Jedwali la 6

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumepata baadhi ya mapendekezo na mengine tulikuwa hatujaweza kuyatafakari kwa pamoja na kwamba, kifungu hicho tumekipitisha; naomba nipate ufafanuzi katika kifungu kinachozungumzia kwamba badala ya kupewa kitalu mtu ambaye ana-*own* kampuni, badala yake iwe ni anaye-*own shares*.

Ninataka nifahamu *shares* hizo zinaweza zikawa aidha hata mbili, tatu au ni nyingine? Naona inaweza pengine ikaleta utata baadaye. Ninaomba nijiridhishe.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti yuko kwenye Kiti, sasa kwa nini mnamjibu Mbunge na Mwenyekiti yupo?

Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme tu kwanza ilitakiwa Mheshimiwa Engineer utuambie utaratibu wa Kanuni gani ambao ulikiukwa. Vilevile ulitakiwa usimame katika kifungu ambacho una wasiwasi nacho ili uweze kutoa ushauri huo na kuona ni namna gani Serikali na Wizara inaweza ikazingatia. Hata hivyo, haikufungi huko mbele unaweza ukaleta hoja binafsi ya kufanya mabadiliko katika kifungu ambacho unaona kwamba kina matatizo.

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori wa Mwaka 2008**
***(The Wildlife Conservation Bill, 2008)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imekaa na kupitia Muswada wa Sheria ya Wanyamapori wa Mwaka 2008, kifungu kwa kifungu na kuupitisha pamoja na marekebisho yake. Hivyo basi, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali na kuupitia Muswada huu.

Mheshimiwa mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnawahisha shughuli.

Ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa sana ya ukomavu wa kisiasa, iliyojidhihirisha katika kuupitia Muswada huu. Hilo lazima niliseme; na kwa niaba ya Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Wabunge, ninawapongeza Wabunge wote. *(Makofi)*

Ninaomba niipongeze sana Kamati, kwa kukubali kukutana na wadau wote na timu zote ili kuweza kufikia muafaka wa Sheria hii. *(Makofi)*

Ninachukua nafasi ya pekee, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake. Muswada huu umepitishwa kiaina yake, umeweka historia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ninaomba nichukue nafasi hii, kukupongeza sana wewe na Naibu wako, lakini vilevile na Timu yako ya Wataalam, kwa hatua hii ambayo tumeifikia.

Waheshimiwa Wabunge, wengine wanasema na mimi mwenyewe; mtanipongeza mtakaposoma kesho.

Baada ya hayo sasa, tumemaliza hatua za Bunge kwa maana ya kuupitisha Muswada huu ili uwe Sheria na sasa unasubiri kupata idhini ya Mheshimiwa Rais na hatua zile ambazo Mheshimiwa Rais atazimalizia. Basi tuwatakie Wizara na Watendaji wote, utekelezaji wa umakini kabisa katika kuusimamia Muswada huu.

Baada ya kusema hayo, ninaomba nimwite Katibu tuendelee na hoja inayofuata.

**Muswada wa Sheria Kuidhinisha Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009** ***(The Supplementary Appropriation (For Financial year 2008/2009) Bill, 2009)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Mara ya Kwanza)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na hatua inayofuata, ninaomba niseme ukweli kwamba; na mimi nina *interest* na Muswada unaokuja, ninataka kuchangia kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Peramiho. Kwa hiyo, ninaomba nimwite Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, aweze kunisaidia kuendesha shughuli hizi ili na mimi niwawakilishe Wananchi wa Jimbo la Peramiho.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu.

**Muswada wa Sheria Kuidhinisha Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009** ***(The Supplementary Appropriation (For Financial year 2008/2009) Bill, 2009)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Sasa ninaomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Nyongeza kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 *(The supplementary Appropriation for Financial Year 2008/2009 Act,*

*2009),* pamoja na marekebisho yake, wenye lengo la kuwasilisha makadirio ya matumizi ya nyongeza ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2008/2009 ya kiasi cha shilingi bilioini 53, yaliyo nje ya bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2008/2009, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unawasilishwa kwa mujibu wa ibara ya 99, ikisomwa pamoja na ibara ya 136(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ambapo Serikali kabla ya kufanya matumizi ya ziada ya yale yaliyoidhinishwa na Bunge kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, inawajibika kupata idhini ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza matakwa ya Katiba, naomba kuwasilisha Muswada wa Matumizi ya Nyongeza kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 ili kuomba idhini ya matumizi ya nyongeza ya kiasi cha shilingi bilioni 53, zilizotokana na marejesho ya fedha za *EPA.* Aidha, nyongeza hii ya shilingi bilioni 53, itatumika kwa ajili ya ruzuku ya mbolea na mbegu bora kwa wakulima, madawa ya mifugo na mikopo katika Sekta ya Kilimo kupitia *TIB.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada wenyewe, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuujadili kwa kina na kuutolea maoni Muswada huu. Aidha, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba kuwasilisha mgawanyo wa matumizi ya nyongeza ya shilingi bilioni 53 kwa kila kifungu kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 21 – Hazina.

Kiasi cha shilingi bilioni tatu kinaongezwa kwa ajili ya kuiongezea mtaji Benki ya Raslimali Tanzania, yaani *Tanzania Investment Bank*. Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wakulima nchini.

(b) Fungu 43 – Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Kiasi cha shilingi bilioni 40 kinaongezwa katika Mfuko wa Ruzuku ya Mbolea kwa ajili ya kununulia pembejeo za kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha shilingi bilioni 40 kitatumika kwa ajili ya ununuzi wa zana za kilimo, kama vile matrekta madogomadogo, yaani *Power Tillers*, Madawa na Mbegu bora kwa ajili ya mahitaji ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la fedha katika kifungu hiki, limetokana na kupanda kwa bei ya mbolea, baada ya kupitishwa kwa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 na uamuzi wa Serikali kuongeza fedha za kununulia mbegu bora na zana za kilimo. Aidha, Serikali kupitia Kitengo cha Ufuatiliaji wa Matumizi na Ukaguzi wa Miradi *(Expenditure Tracking and Project Inspection),* kitafuatilia kwa karibu matumizi ya fedha hizi kwa kila robo mwaka ili kudhibiti matumizi yake na kuhakikisha kwamba, fedha zinatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

(c) Fungu 99 – Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Kiasi cha shilingi bilioni 10 kinaongezwa kwa ajili ya kununulia madawa ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakuwa ikitenga fedha katika bajeti yake ya kila mwaka, kwa ajili ya kujiandaa kulipa madeni ya *EPA*, endapo wadau halali watajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili:-

Sehemu ya kwanza, kama ilivyorekebishwa ni kifungu cha I – IV; inahusu masuala ya utangulizi kama vile jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Muswada wenyewe, ambapo imebainishwa kwamba, Muswada huu unapaswa kusomwa pamoja na Sheria ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009, ambayo ilipitishwa na Bunge mnamo mwezi Agosti, 2008. Aidha, sehemu hii inabainisha pia Mamlaka ya Hazina, kutumia kiasi cha shilingi bilioni 53 kutoka Mfuko Mkuu Hazina, kwa ajili ya kulipia gharama za Serikali kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu hii, yamefanyika marekebisho kama inavyobainishwa katika jedwali la marekebisho, ambapo kifungu chote cha tano cha Muswada, kimefutwa kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa sheria *(Drafting Principles);* kwa kuwa matakwa ya kifungu hiki tayari yameainishwa katika Sheria ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009, ambayo tayari Bunge lako Tukufu limekwishaipitisha wakati wa kuhitimisha Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya jedwali kama ilivyorekebishwa, inabainisha mgawanyo wa matumizi haya ya nyongeza ya shilingi bilioni 53 kwa Fungu 21 - Hazina; Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Fungu 99 - Wizara ya Maaendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyobainishwa katika Jedwali la Marekebisho, ambapo kiasi cha shilingi bilioni tatu kinachoongezwa kwa ajili ya kuiongezea mtaji Benki ya Raslimali Tanzania, kitakasmiwa katika Fungu 21 - Hazina, badala ya Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Uchumi, kama ilivyobainishwa kwenye Muswada, kwa kuwa bajeti

ya Benki ya Raslimali Tanzania inakasmiwa chini ya Idara ya Msajili wa Hazina ambayo ipo chini ya Fungu 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuupitisha Muswada huu na kuidhinisha matumizi ya nyongeza ya shilingi bilioni 53 kwa mwaka wa fedha 2008/2009, kwa ajili ya maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nachukua nafasi hii kumwita Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, ambayo inashughulikia masuala ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu.

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, nachukua nafasi hii, kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kuhusu Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Nyongeza kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009 *(The Supplementary Appropriation (For Financial Year 2008/2009) Bill, 2009).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha maoni ya Kamati, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini. Uchaguzi huu umetokana na kifo cha Mheshimiwa Richard Nyaulawa, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. Aidha, tunamtakia Mheshimiwa Luckson Mwanjale, mafanikio katika kutekeleza kazi ya kuwawakilisha wananchi wa Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kamati ilikutana Siku ya Ijumaa tarehe 30 Januari, 2009 hapa Dodoma, kuupitia Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Nyongeza kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009. Hoja hii iliwasilishwa mbele ya Kamati na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo. Napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru kwa dhati, Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kushiriki kwao kikamilifu katika kuupitia na kuujadili kwa ufasaha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada huu, napenda kwanza kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati hii ya Fedha na Uchumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Abdallah O. Kigoda ambaye ni Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Anthony M. Diallo Mjumbe, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Felix Christopher Mrema, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Dkt. Omari Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza mtoa hoja kwamba, Muswada huu unawasilishwa kwa mujibu wa ibara ya 99, ikisomwa pamoja na ibara ya 136(3) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ambapo Serikali kabla ya kufanya matumizi ya ziada ya yale yaliyoidhinishwa na Bunge hili Tukufu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, inawajibika kupata idhini ya Bunge.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia utaratibu huu, kwa maana ya kupunguza hoja kati ya Bunge na Serikali, mara Serikali inapoamua kutumia fedha za nyongeza na halafu baadaye kuja kuomba idhini hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba, Mheshimiwa Rais, alipolihutubia Bunge tarehe 21 Agosti, 2008, alieleza na kutoa agizo kwamba, fedha za *EPA* zilizorudishwa Serikalini, ziingizwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya shughuli za maendeleo ya nchi, ikiwemo kuongeza fedha katika Mfuko wa Ruzuku ya Mbolea kwa Wakulima, madawa ya mifugo na mikopo katika Sekta ya Kilimo, kupitia Benki ya Raslimali Tanzania *(Tanzania Investment Bank)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, agizo lile la Mheshimiwa Rais, limezaa Muswada huu wenye lengo la Serikali kuwasilisha makadirio ya matumizi ya nyongeza kwa mwaka wa fedha 2008/2009 ya kiasi cha shilingi bilioni 53, zilizopatikana baada ya fedha za *EPA* kurudishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia Muswada uliopo mbele yetu, Kamati ya Fedha na Uchumi, imetafakari hali ya sasa ya uchumi duniani, iliyokumbwa na mtikisiko mkubwa wa kiuchumi na fedha *(Economic and Global Financial Crisis)*.

Kwa bahati mbaya, nchi yetu haiwezi kujitenga na mazingira ya uchumi wa dunia na hivyo kutufanya na sisi kuchukua tahadhari zote. Nchi nyingi duniani pamoja na nchi tajiri, hivi sasa zina hali mbaya kiuchumi na kwa nchi zinazoendelea, yapo maeneo mawili ambayo yataendelea kutusumbua.

Kwanza; ni mfumko wa bei unaotokana na upungufu wa chakula na pia mfumko wa bei za mafuta ingawa hivi sasa bei hizo zimeanza kupungua. Kwa hiyo basi, katika kipindi hicho cha mpito ni busara kuangalia athari za kiuchumi za muda mfupi, wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia sura ya uchumi nchini kwetu katika mazingira hayo kwa maana ya mfumko wa bei, mwezi Desemba, 2008 ulifikia 13.5% ikilinganishwa na 6.4% Desemba, 2007. Bei ya vyakula peke yake imeongezeka kwa 18.6%, ukiondoa Chakula mfumko wa bei umefikia 6%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wenzetu jirani, kwa mfano, Kenya mfumko wa bei katika kipindi hicho umepanda kutoka 12% hadi 39% hivi sasa. Mfumko huu mkubwa kwa kiwango kikubwa, umechangiwa na bei kubwa za chakula. Hivi sasa Kenya imetangaza baa la njaa, wakati hapa nchini dalili za upungufu wa chakula kutokana na hali mbaya ya hewa tayari zimekwishaanza kujionyesha. Hotuba za mwisho wa mwezi za Mheshimiwa Rais za Desemba, 2007 na Januari 2009, vilevile zimethibitisha wasiwasi kuhusu upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hoja ya msingi hapo juu, Kamati ya Fedha na Uchumi, imeunga mkono pendekezo la Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Nyongeza kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 la kuongeza shilingi bilioni 40 Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; shilingi bilioni 30 kwa ajili ya mbolea; na shilingi 10 kwa ajili ya pembejeo nyingine za kilimo kama mbegu bora, zana za kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali kutumia fedha za *EPA* kugharimia Sekta za Kilimo na Mifugo kwa kutoa mikopo ya kununulia matrekta, majembe ya kukokotwa na ng’ombe na mbegu bora kuwa ni sahihi na izingatie umuhimu wa kupanua wigo wa matumizi ya fedha hizi ili wananchi wengi katika Mikoa mbalimbali waweze kunufaika na fedha hizo.

Pamoja na fedha hizo, Kamati inasisitiza kwamba, Serikali iweke mikakati ya kutafuta fedha nyingine kutoka katika taasisi nyingine ili kutoa mikopo kwa wakulima, wafugaji na wavuvi, kwa ajili ya kuendeleza sekta hizi muhimu. Aidha, Kamati imeunga mkono pendekezo la shilingi bilioni 10 kuongeza kwa ajili ya kununulia madawa ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua hii, kama utekelezaji wake utafanyika vizuri kwa upande wa Serikali, itasaidia Taifa kujiandaa kwa kipindi cha sasa na kile cha muda wa kati. Kamati imeishauri Serikali, fedha hizi zitakazoelekezwa katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, zitolewe haraka ili ziweze kusaidia maeneo yenye uhaba mkubwa wa mbolea za kukuzia mazao ili tupate mazao makubwa katika kipindi kijacho. Nyongeza ya shilingi bilioni 30, itafanya jumla ya shilingi bilioni 61 kuelekezwa kwenye upatikanaji wa mbolea, ambayo bei yake imepanda sana hivi sasa.

Kamati imeishauri Serikali kuhakikisha kuwa, dhamana inayotolewa kwa Sheria ya Mbolea Tanzania, ikamilishwe ili kuwezesha shirika hilo kusafirisha mbolea ya Minjingu katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza gharama ya mbolea ni muhimu kuwa na barabara bora ya kusafirisha mbolea kutoka kiwandani kwenda kwa watumiaji. Kiwanda cha mbolea cha Minjingu Mkoani Manyara, kitasaidia kuondoa tatizo la uhaba wa mbolea hapa nchini kama barabara ya kutoka Minjingu – Babati - Dodoma itaimarishwa na kuwa madhubuti zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kuondoa kutokuelewana kati ya Benki ya NMB na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na hivyo kuwezesha zoezi la ununuzi wa mbolea kwa kutumia vocha, kuendelea vizuri kupitia Wakala waliowekwa. Kamati imeishauri Serikali vilevile kuangalia suala la gharama za usafiri wa mbolea zitakazonunuliwa ili zisiwe ni mzigo kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile hivi sasa zipo tani 150,000 katika Hifadhi ya Chakula ya Taifa, bado maeneo mengine hususan Mikoa ya Kusini, ambayo ina chakula kingi, mara mbili zaidi ya kile tulichonacho kwenye hifadhi. Hata hivyo, katika Mikoa mingine kwa sababu ya hali ya hewa kuwa mbaya, imenyemelewa na upungufu mkubwa wa chakula kama siyo njaa. Kamati inaishauri Serikali, kuharakisha taratibu za kupeleka chakula kwenye maeneo yenye uhaba kutoka kwenye Mikoa yenye ziada. Hatua hii ikichukuliwa na Serikali, pamoja na zile za kuongeza bajeti ya mbolea na madawa, itasaidia kutuhakikishia usalama na utoshelezaji wa chakula nchini katika kipindi hiki, ambacho dunia nzima ina changamoto kubwa ya kuchukua hatua madhubuti za kupambana na athari za mtikisiko wa kiuchumi na fedha duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu wa Fedha, shilingi bilioni tatu zimepangwa kupelekwa Benki ya Rasilimali Tanzania kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wakulima nchini. Fedha hizi si nyingi kwa lengo linalokusudiwa. Hata hivyo, Kamati inaelewa kwamba, tayari imekwishaongeza mtaji wa Benki hii kutoka shilingi bilioni 29 hadi shilingi bilioni 50 katika mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, nyongeza iliyokusudiwa inapandisha mtaji wa Benki hii hadi kufikia shilingi bilioni 53. Kamati imearifiwa na Serikali kuwa, shilingi bilioni 50 ni kwa ajili ya maendeleo. Nia kubwa sasa ni kuanzisha dirisha kwa ajili ya mikopo ya kilimo, dirisha hili litaanza kufunguliwa kwa shilingi bilioni tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kamati ilivyobaini awali kiasi cha shilingi bilioni tatu ni kidogo, lakini kutokana na janga linalonyemelea uchumi wetu na nchi yetu, Kamati imeona ni bora Sekta ya Kilimo na ile ya Mifugo, zipewe kipaumbele hivi sasa ili hapo baadaye tujihami kutokana na athari zozote zitakazotupunguzia au kutuletea uhaba wa chakula nchini.

Kamati inaishauri Serikali kuwa na mikakati kabambe kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya kuiongezea mtaji Benki ya Rasilimali ya Tanzania ili iweze kutoa mikopo kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za kiusalama za kiuchumi *(Economic Intelligence Report),* zinaonyesha kuwa mtisikiko huu wa kiuchumi na fedha duniani, pamoja na jitihada zote zilizochukuliwa na nchi tajiri, uchumi duniani utaendelea kudorora kwa miaka miwili au miwili na nusu hivi. Taarifa hizi kwetu sisi nchi zinazoendelea, zinatusukuma tuweke kipaumbele katika yale maeneo ambayo tuna uwezo wa kukabiliana nayo. Hakika eneo la kilimo na mifugo hasa kwa kuzipatia ziada ya chakula, ndiyo eneo pekee tunalohitaji kuliwekea msisitizo.

Kamati ya Fedha na Uchumi, inaunga mkono pendekezo la Serikali la kuongeza shilingi bilioni 50 moja kwa moja ziende kusaidia kilimo na mifugo na shi-lingi bilioni tatu ziweze kusaidia eneo hilo hilo, ingawa itakuwa ni mkakati wa muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kamati ya Fedha na Uchumi, inampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uamuzi wake na agizo lake la fedha zilizotokana na marejesho ya fedha za *EPA* zielekezwe kuongeza fedha zilizotengwa kwa kilimo na mifugo kwa njia ya ruzuku ya mbolea kwa wakulima, madawa ya mifugo, pembejeo nyingine na kwa ajili ya mikopo katika Sekta ya Kilimo kupitia *TIB.* Uamuzi huu umekuja wakati mzuri na ni matumaini ya Kamati kwamba, Serikali itatekeleza agizo hili kwa uadilifu, tija na ufanisi mkubwa.

Maoni ya Kamati ni kwamba, Serikali iendelee na mikakati ya kukusanya fedha za *EPA* na kuziweka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ili fedha hizo ziweze kutumika kwa manufaa ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati.

Vilevile namshukuru Katibu wa Bunge, kwa kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi ya kuchambua Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Nyongeza kwa mwaka 2008/2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naomba nimshukuru Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, pamoja na Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati; nawashukuru sana. *(Makofi)*

Ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, Nnaibu Mawaziri; Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu wa Hazina Ndugu Kija na Wataalam wote, waliotusaidia katika kuchambua Muswada huu. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika ujEnzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Lawrence Makigi, kwa kazi nzuri ya kuihudumia Kamati hii, ikiwa ni pamoja na kuandaa maoni ya Muswada huu kwa wakati unaotakiwa. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Sasa namwita Waziri Kivuli wa Wizara hii ya Fedha na Uchumi, ambaye ni Kiongozi wa Upinzani, lakini nadhani kwa niaba yake namwona Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, tafadhali.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS (K.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima na nguvu za kuweza kusimama hapa mbele yenu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Nyongeza kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani ya Bajeti ya 2008/2009, tuliishauri Serikali kwamba, pesa za *EPA* shilingi bilioni 131.8 ziingizwe katika bajeti, sisi tuuliita C*ommitment* ya EPA, Serikali ilijibu hivi, nanukuu: "Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote wanaonisikiliza, fedha za *EPA* hazikuwa fedha za Serikali wala za Benki Kuu, hizi fedha zilikuwa za wafanyabiashara, ambao kwa wakati ule waliilipa iliyokuwa *NBC* kwa ajili ya kuagiza bidhaa mbalimbali toka nje."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nukuu hii, Serikali ilikataa kuziingiza pesa katika Bajeti yake. Tunashukuru kwamba, yale tuliyoyasema wakati ule sasa yameonekana yanawezekana. Matumainio yetu ni kuwa na ushauri mwingine tulioutoa pia utazingatiwa ili kuwapunguzia mzigo wa maisha Watanzania, wakati rasilimali zipo lakini zimekosa usimamizi thabiti. Kama unatakiwa uthibitisho wa hayo, tupo tayari kuutoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi ya Upinzani, inasikitika kwa kuwa majibu yaliotolewa na Serikali sio tu yalipingana na ushauri wetu, bali hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, jambo ambalo linaidhalilisha sana Serikali. Ushauri wetu kwa siku za mbele, Serikali iongeze umakini katika kutoa majibu na hasa pale ambapo ushauri wa Kambi ya Upinzani na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwani yeye katika taarifa yake alizionyesha fedha za *EPA* kuwa ni fedha za Serikali zilizotakiwa zirudishwe na Serikali ikazikana au taasisi zinazoheshimika maoni yao kwa kiasi fulani yanaoana, maana leo Watanzania watajiuliza hivi ni nani mkweli ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unaonyesha kuwa, shilingi bilioni 40 zinaongezwa katika Mfuko wa Ruzuku ya Mbolea kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo, ili kuweza kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula. Kambi ya Upinzani inauliza; hivi hii mbolea ya ruzuku inamnufaisha nani kati ya mkulima au mfanyabiashara? Kutokana na taarifa halisi kutoka kwa wakulima wa mikoa mbalimbali, inaonyesha mbolea hii ya ruzuku haina faida kwa wakulima na badala yake kwa kiasi kikubwa inawanufaisha wafanyabiashara. Hii ni kumwongezea mlipa kodi wa Tanzania mzigo. Tunaishauri Serikali, isikie kilio cha wakulima ambacho kimewasilishwa vyema na Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni, juu ya matatizo ya mbolea ya ruzuku; kwanza, kuwa kidogo haitoshi, lakini pili, haifiki kwa wakati na hivyo wafanyabiashara ndiyo wanaofaidi kuliko wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kauli aliyoitoa Mheshimiwa Rais hapa Bungeni kwamba, fedha hii itakwenda kwenye kilimo kupitia *TIB* ni vyema Serikali ikaeleza wazi, kiasi gani kinaenda *TIB* na kwamba, hizo nyingine zimekwisha kutumika au bado zilikuwa zinangoja idhini ya Bunge au vipi? Kwa kuwa tunaamini Serikali haiwezi kutumia bila ya idhini ya Bunge; ni vyema basi ikatoa mchanganuo wa matumizi kamili ya fedha hizi, hasa kwa kuzingatia kuwa fedha hizi kwa mujibu wa kauli ya Serikali, huenda wenyewe wakaja kuzidai; hivyo, zinahitaji kutumika katika kuzalisha ili ziweze kulipwa zikihitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikwishatoa tathmini yake ya upembuzi yakinifu, juu ya azma yake ya kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa ndio ghala kuu la chakula hapa nchini. Kambi ya Upinzani inaona kuwa, badala ya Serikali kuendelea kuwanufaisha wafanyabiashara ni bora basi ichukue uamuzi wa kuwekeza fedha hizo kwa Mkoa wa Morogoro. Tunaamini mafanikio yake yatajionyesha kwa kipindi cha muda mfupi na nchi itaondokana na tatizo la njaa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria hii unapendekeza mgao wa shilingi bilioni tatu kwenda kuongeza mtaji kwenye Benki ya Raslimali. Kambi ya Upinzani toka mwanzo ilipendekeza kuwa, Benki hii ya Raslimali, japokuwa imepewa majukumu makubwa ya kutoa mikopo kwa wakulima, bado ilikuwa ni changa kwa dhana kuwa, mtandao wake bado ulikuwa ni mdogo mno na mtaji wake pia ulikuwa ni mdogo; na hivyo kutumiwa kama ndiyo Benki ya Taifa, kutoa mikopo ya kilimo ni kiini macho na hadaa kwa wakulima! Ni vyema Serikali ikaeleza ni namna gani Benki hii itawafikia wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, kabla haijaunga mkono hoja hii; ni vyema tukafahamishwa hizi fedha ziko wapi kabla hazijatumika, kwa sababu Gavana anashindwa kujua ni akaunti ipi yenye fedha hizo; je, ni mamlaka gani inayoweza kulielimisha Bunge fedha hizo zipo katika mfuko gani hata Serikali sasa iwe na mamlaka ya kuzitumia?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Waheshimiwa Wabunge, sasa nachukua nafasi hii, kumwita mchangiaji wetu wa mwanzo, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbele, naomba niseme kwamba, naiunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeza pia Mheshimiwa Rais, katika hotuba zake za hivi karibuni ameonyesha nia njema kabisa ya kuangalia na kuzingatia umuhimu wa kukuza kilimo kama uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania. Kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Peramiho, naomba nimpongeze na mimi niseme tu ninamuunga mkono kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu nianze kwa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge Enzi za Mwalimu mwaka 1972. Enzi za mwalimu, Azimio la Iringa kupitia Halmashauri Kuu ya TANU liliweka msisitizo wa Siasa ni Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku Azimio hilo linapitishwa ili lizingatiwe, malengo makubwa yalikuwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze na hayo halafu nirudi katika hoja yenyewe.

Moja, Enzi hizo za Mwalimu katika Azimio la Iringa "Siasa ni Kilimo" ilikuwa ni kuhakikisha nchi inawapatia wakulima na wafanyakazi chakula cha kutosha. Mwaka 1972, Azimio hilo liliazimia Serikali ijitosheleze kwa chakula ndani na iuze nje ya nchi. Vilevile Serikali iuze chakula nje ili iongeze akiba ya fedha za kigeni na kuweza kukuza uchumi wa nchi, lakini kilimo kiongeze uzalishaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda. Enzi hizo za Mwalimu tulikuwa na viwanda vingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulitafakari Azimio, yalionekana matatizo ya kimsingi, ninaomba niyataje: La kwanza, ilionekana kabisa kwamba, hakuna utaalam wa kutosha kuweza kuinua kilimo. Pili, kanuni za kilimo bora za kukifanya kilimo kiwe chenye tija hazipo na hazifuatwi kikamilifu. Matumizi ya mbolea yalikuwa ni kwa kiwango kidogo sana miaka hiyo ya 1972. Vilevile zana bora za kilimo kwa ajili ya kuwawezesha wakulima kulima kilimo cha kuweza kuyafikia malengo hayo zilikuwa bado ni duni, kwa maana ya majembe ya mkono kama ilivyo mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi yaliyofikiwa kwenye Azimio hilo ili kuweka mkakati, ilikuwa ni uboreshaji wa mbegu bora, kuhakikisha wakulima wanatumia kanuni bora za kilimo, matumizi ya mbolea yawafikie walengwa, yaani wakulima mpaka wale wa Jimbo la Peramiho, zana bora za kilimo yakiwemo matrekta na majembe ya

kukokotwa kwa ng'ombe, yaende kule kwa wakulima wazalishaji, ambako ndiko kwenye uti wa mgongo wa Taifa. Vilevile nchi ihakikishe inatengeneza soko la ndani na la nje la wakulima wetu, kwa mazao yote ya chakula na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hizo zilikuwa ni Enzi za Mwalimu mwaka 1972. Habari ya Enzi za Mwalimu bado tunazizungumza mpaka leo na sasa hivi ni miaka 48 toka tumepata uhuru. Ndiyo maana mimi leo kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Rais, kwa maazimio yake makubwa na ya kimsingi ya kuamua sasa ni lazima Sekta ya Kilimo ifanyiwe mabadiliko. *(Makofi)*

Pili, ninampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuona umuhimu wa kuliomba Bunge, fedha hizi sasa ziende kwenye Sekta ya Kilimo na Mifugo ili kuleta mabadiliko kwa kuzingatia Enzi za Mwalimu kama nilivyosema hapo mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa wakulima na wafugaji, wanapata shida kubwa sana ingawa ndiyo wanaotegemewa kujenga uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli Bunge litaazimia kupitisha Azimio hili la kuongeza fedha ya bajeti kwenda kwenye kilimo, ninaiomba sana Serikali fedha hizo kweli zikafanye kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwa nchi yenye heshima kama Tanzania, asilimia kubwa ya wakulima wake, waendelee kupinda migongo kwa kutumia majembe ya mkono miaka yote kwenye uzalishaji wao. Kwa maana hiyo, lengo hili sasa la kufanya mabadiliko kutoka jembe la mkono kwenda kwenye matrekta, liwe ni lengo mahususi linaloweza kupimika na kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Serikali hii tulifanya maamuzi ya kujenga shule za sekondari na zimejengwa; zilijengwa namna gani? Njia zile tulizotumia kujenga shule za sekondari hebu tuzitumie njia hizo hizo kuhakikisha wakulima wetu sasa wanaondokana na jembe la mkono na kuingia kwenye uzalishaji wa mazao kwa kutumia matrekta na majembe ya kukokotwa na ng'ombe, inawezekana. Ninaamini kabisa kila mtu akitimiza wajibu wake inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hapa Enzi za mwalimu tatizo la mbolea lilikuwepo, lakini tunaendelea na tatizo hilo mpaka leo. Muswada huu unakusudia kuongeza nguvu katika suala nzima la mbolea ili kusaidia kuzalisha mazao kwa ziada, kujitosheleza kwa chakula kama Enzi zile za mwalimu, na kuweza kuwa na akiba ya chakula ya ndani na kuuza nje kwa maana ya kuongeza uchumi na pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kwamba Serikali imefanya kazi kubwa sana katika suala nzima la ruzuku. Lakini Serikali inaelewa yanayoendelea huko vijijini kuhusiana na ruzuku kwa sasa? Pamoja na nia njema ya Serikali bado wakulima kwa mbolea hii ya ruzuku wanaipata kwa mikingamo mikubwa, na pamoja na kwamba haitoshelezi lakini bado kuna mikingamo mikubwa sana. Ninashukuru sana nimeongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi akaniambia kwamba sasa hivi fedha zimepelekwa

kwenye benki ya NMB. Nilikuwa nazungumza na wakulima wa Jimboni kwangu Peramiho, Mawakala wote wanasimama kusambaza mbolea kwa wakulima kwa sababu walikuwa hawajapata fedha kutoka Benki NMB, na hivyo zoezi nzima la kusambaza mbolea lilisimama kwa namna fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua tuliyofikia, Mikoa inayopata mvua ambazo ni za kuweza kuzalisha chakula, ilibakia minne tu ya *Big Four* mpaka hivi sasa, lakini haina mbolea. Kweli yale malengo toka Enzi za Mwalimu yatatekelezeka kama hatutakuwa na nia ya kufanya hayo mabadiliko kabisa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme, kwa kweli tuamue kwa dhati. Mkoa wa Ruvuma tunalo Agizo la Mlale; Agizo hili linaeleza kalenda ya kilimo ya mwaka mzima. Ukituambia kilimo katika Mkoa wa Ruvuma; kuna tarehe ya kutayarisha shamba, kuna tarehe ya kupanda, kuna tarehe ya kulima, mpaka tarehe ya kuvuna kama Enzi za Mwalimu katika Azimio la Iringa la Siasa ni Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninaendelea kusema kwamba, inasikitisha pamoja na fedha hizi kama tunazipitisha, lakini kama zitawafikia wakulima misimu hiyo yote ya kilimo imekwishapita. Kwa hiyo, tutaendelea kubaki pale pale badala ya kupiga hatua kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitoe angalizo, nilichokigundua baada ya Serikali kuamua kutoa ruzuku kwenye pembejeo, yapo makampuni binafsi yaliamua kushusha bei ya mbolea chini ya bei ile iliyopangwa ya ruzuku na wakati huo wakulima tayari wamekwishaji-*commit* kununua mbolea kwa bei ya ruzuku iliyopangwa na Serikali; kumetokea mtafaruku mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hayo yote ni mambo ya kuchukua tahadhari ili kuweza kuinua kilimo katika nchi yetu ya Tanzania na kukifanya kilimo hicho kiwe chenye tija. Ninaipongeza Serikali kwa kuamua kuipa *TIB* fedha ya kutosha ili iweze kutoa mikopo kwa wakulima. Niseme hii fedha tuliyoi-*allocate* safari hii, itaanza tu siyo ndogo, lakini haiwezi kutosheleza kuanzisha Benki ya Wakulima wala kuwasaidia wafugaji. Kwa hiyo, nitoe changamoto kwa Serikali yetu, nia njema ya Serikali tumeiona, lakini wakulima wanahitaji mahali pa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Benki hiyo ya *TIB,* tunavyo Vyama vya Akiba na Mikopo vipo hoi bin taabani na vilikuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa wakulima kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, azma ya Serikali, ninaomba iendane na kuviimarisha Vyama vya Akiba na Mikopo, ndiyo mahali pekee ambapo wakulima wanaweza wakaanza kwa hatua ya kwanza kukimbilia kupata mikopo midogo midogo na wale wakulima wakubwa wakakimbilia kupata mikopo mikubwa kutoka kwenye Benki ili upate mkubwa lazima uanze na mdogo. Kwa hiyo, tuwaimarishe wakulima wadogo kwa namna yao na wakulima wakubwa nao waimarishwe kwa namna yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Jimbo la Peramiho, wanaiunga sana Serikali hii, lakini kwa kweli kilio chao kikubwa ni suala zima la kuboresha kilimo kupitia mambo makubwa matatu ama manne:-

La kwanza, kuwabadilishia kilimo hiki kutoka jembe la mkono kuingia katika kutumia jembe la kukokotwa na ng'ombe ama matrekta.

La pili, kuwasaidia kupata pembejeo kwa wakati kwa maana ya mbegu bora na mbolea.

La tatu, kuhakikisha wataalam wa ugani wanapatikana kwa muda wote.

La nne, Serikali izingatie kuhakikisha soko la ndani na soko la nje linapatikana bila kuwa na tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakishafanya hivyo kuanzia Jimbo la Peramiho na Majimbo mengine yote, lakini hasa ile Mikoa inayotegemewa kuzalisha chakula itafanya kazi yake na huu mfumko wa bei na hasa kwenye chakula ndani ya nchi, utaweza kuwa umedhibitiwa kwa namna fulani.

Uchumi unatetereka katika Ulimwengu na sisi tujipange kwa kuzingatia hali halisi ya Ulimwengu jinsi ilivyo, tusipokwenda na wakati, wakati utakuwa ukuta na utatuumiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais, naipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi na ninaiunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu mdogo katika hoja hii muhimu sana. Mimi kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, ninaamini kabisa kwamba, ametuwakilisha kikamilifu, bali nilikuwa nataka nitoe nyongeza tu katika sehemu chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Kikao hiki, ningependa nimpongeze ndugu yetu Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, kwa kuchaguliwa kwake na kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa kule Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, amekwishampongeza Mheshimiwa Rais, kwa Agizo na wenzangu walionitangulia wameyasema hayo, sina haya ya kuyarudia kwa sababu Mwenyekiti ametuzungumzia sisi sote Wajumbe wa Kamati yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake; kwanza, kwa kusikia kilio cha wakulima juu ya tatizo la mbolea na pembejeo. Pili, kwa kutekeleza hilo Agizo la Mheshimiwa Rais. Tatu, kwa kuona umuhimu wa

kupeleka fedha kwenye kilimo na uwekezaji wa Benki ya *TIB.* Mwisho, nampongeza kwa kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba, matumizi ya fedha hizi yatasimamiwa kwa karibu zaidi na *Expenditure Tracking Unit.* Nafikiri ule uwoga wa kusema fedha hizi zitatumika vibaya, utakuwa haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kwa kutokurudia tu nizungumzie sehemu kubwa moja, nayo ni mgao. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Waziri, alituridhisha kwenye Kamati, juu ya mgao ule wa shilingi bilioni 40 kwa ajili ya kwenda kwenye kilimo. Kati ya hizo; shilingi bilioni bilioni 30 zitakuwa kwa ajili ya mbolea na shilingi bilioni 10 kwa ajili ya pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri angalizo langu ni kwamba, mbolea zaidi itakwenda kwenye mazao ya chakula. Kwa kuwa sasa hivi msimu wa vyakula vingi unakaribia ukingoni, ningependa kuishauri Serikali pawe na *flexibility* katika kuzitumia fedha hizi kwa maana moja tu kwamba, inawezekana ikanunuliwa mbolea, lakini *logistics* za usafirishaji zikachelewesha na kule zitakapofika pengine kukawa hakuna *capacity* ya *utilization,* maana yake ni kwamba, tutakuwa tumenunua mbolea tu, lakini pengine itabidi ikae mpaka kungojea awamu zijazo za msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi, ningependa kuishauri Serikali pawe na *flexibility* kwa maana moja; pamoja na kuthamini tatizo la njaa kwa ajili ya chakula, lakini kuna hii *global financial crisis* na sisi tunataka tujihami nayo. Kwa hiyo, ikiwezekana waangalie hasa *hii Expenditure Tracking Unit,* ifuatilie kwa karibu kuona kwamba, kama sehemu ambazo mbolea itapelekwa itakuwa imechelewa haitatumika, basi pawe na uwezekano wa kuweza kununua pembejeo zaidi ili ziweze kuzalisha na kuweza kupata fedha zitakazoweza kusaidia katika matumizi yetu. Sisi wa Mikoa wa Pwani, Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Tanga na kule Tunduru ni wakulima wa korosho. Wakulima wetu sasa hivi wana tatizo kubwa sana la pembejeo za korosho. Sasa kama kutakuwana na *flexibility,* maana yake ni kwamba, Sekta hiyo basi iongezewe pembejeo wakati Serikali ikiangalia maeneo mengine ili korosho ziweze kuzalishwa.

Bahati nzuri, kwa korosho bado tupo katika msimu mpaka mwezi Mei mwaka huu, ndiyo itakuwa labda tunahitaji pembejeo ziwe zimekwishafika kwa kuweza kupulizia mikorosho. Kwa hiyo basi, Serikali inatakiwa ifanye busara sana kama kutakuwa na *flexibility* hiyo. Vilevile ningependekeza kwamba, pamoja na kuwa *TIB* imeongezewa hizo shilingi bilioni tatu, pamoja na zile shilingi bilioni 50 kuwa na shilingi bilioni 53, lakini Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati alituambia kwamba, kiwango ambacho kilitakiwa hasa kitolewe kilikuwa shilingi bilioni 20.

Kwa hiyo, hapa pana pengo la shilingi bilioni 17, pengine itakuwa si busara kutaka kubadilisha mgao huu hivi sasa, lakini ningependa Mheshimiwa Waziri alihakikishie Bunge hili, tumebakiza miezi 3 au 4 tutaingia katika bajeti, basi ili *TIB* iweze kuwa na mtaji wa kuridhisha hususan kwa maana ya kukopesha wakulima ambao ndio walio wengi katika nchi hii, basi lile pengo lizibwe wakati wa bajeti ijayo. Tukifanya hivyo, nadhani tutakuwa tumeweza kunufaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, mengi yamesemwa na Mwenyekiti na nilikuwa sina haja ya kurudiarudia. Nia yangu kubwa ni kufafanua katika eneo hili na ninaamini Serikali imenisikia na wakulima wa kule Kisarawe Mkoa wa Pwani na mikoa yote wanakolima korosho, watategemea kupata jibu la hizi pembejeo ambazo ninazizungumzia hapa. Nakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia huu Muswada mdogo wa fedha za ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi naomba nimpongeze Waziri, Manaibu wake, pamoja na Wataalam wetu wa fedha, kwa kutuletea hili mapema ili tuweze kuidhinisha na fedha zitumike kwa wakati bila migogoro yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuwa akichangia Mheshimiwa Jenista Mhagama, ameeleza vizuri sana jinsi ya Enzi za Mwalimu zilivyokuwa zikitumia alipokuwepo na leo; tofauti ya miaka 48 toka tumepata uhuru, uhai wangu mimi hapa nilipo, yapo mabadiliko na mengi yamefanyika lakini pia yapo mengine ambayo sisemi kwamba yalikuwa yakisuasua, lakini labda kutokana na matatizo ya kifedha, ndiyo yalikuwa yanashindwa kukamilika kuweza kufanikisha hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi shilingi milioni 40 leo zimetoka kwa ajili ya kuimarisha kilimo na wala hakuna Mtanzania ambaye ataleta neno la pembeni kwamba kwa nini zote wapeleke kwenye kilimo, kwa sababu hakuna mtu asiyeamini katika nchi kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa maisha yetu au wa nchi yetu. Nasema naipongeza sana Serikali kwa kulifikiria hilo, hasa Waziri wa Kilimo kwa kuziomba hizi fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zimetolewa kwa *TIB*, fedha zimetolewa kwa Wizara ya Mifugo. Sasa bahati mbaya katika mifugo, tulipokuwa tukikutana na wataalam mbalimbali, ipo dhana na hisia au mapenzi ya mtu kwa fani yake, hata kule vijijini maafisa wetu ugani wanaposimamia Halmashauri kama afisa yule ugani anatokea kwenye kilimo, hata sekta ya mifugo inapata tabu kidogo, inakuwa inalegalega, kwa sababu ana-*base* sana katika ile taaluma aliyokuwepo.

Hivyo hivyo tena afisa ugani anapotokea kwenye Mifugo, basi na Kilimo nacho kinakuwa kama wanakwisha kulingana na taaluma zao. Ndiyo maana tunaiomba sasa hivi Serikali, kama fedha hizi zitaweza kusaidia kufungua vyuo vya ugani katika sekta zote za mifugo, kilimo, uvuvi na kadhalika, basi waweze kuongeza ili kila Halmashauri iweze kuwa na maafisa ugani; ikiwa wa mifugo, ikiwa wa kilimo, ili shughuli zote ziweze kwenda na fedha hizi zitumike vile tulivyokuwa tumeziomba na kuziidhinisha hapa ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mhagama, alipokuwa akitoa maelezo, alipata wasiwasi shughuli zitakavyokwenda na matumizi haya yatakavyofika kule vijijini. Mimi nafikiri sisi tutakuwa imara, lakini katika Wizara ya Mifugo kwa kutumia mfano ule wa maafisa ugani, bado tumemsahau mvuvi. Tunasema nini juu ya uvuvi?

Tunafahamu tuna Miradi ya MASEMU imesaidia na sasa hivi imekwenda Ukanda mzima wa Pwani, lakini tuna wavuvi wa Maziwani kwa maana Victoria, Tanganyika na Nyasa; tuna mabwawa, tuna mito, hawa wote wanahitaji kusaidiwa kwa maana ya pembejeo. Leo fedha zote hizi ukizipeleka kwenye madawa ya mifugo na ukaacha kuangalia za wavuvi na ikiwa sisi Serikali kazi yetu kutoa amri ya kuchoma moto nyavu, kamata funga, piga, sasa imeshatoka amri ya miezi sita ya operesheni.

Mimi naiunga mkono Serikali na narudia tena kwamba, sitakubali bahari yetu ya Mafia iathiriwe na watu wanaotoka nje ya Mafia kwa sababu ninaamini kwao wameshavuruga sasa wanakuja kwetu. Lazima tushirikiane na Serikali, lakini tatizo sasa wavuvi popote pale walipo *pressure* inapanda, *pressure* inashuka. Wanapoona tu lile suala la *patrol*, kuhimiza usimamizi bora na uvuvi endelelvu, linakuwa shida na yote haya yanatokana na nyavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba katika fedha hizi, kama kuna uwezekano wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, basi uvuvi nao ukumbukwe tuweze kusaidiwa katika kuangalia au kubadilisha nyavu; tatizo ni nyavu. Nyavu ziingie kwenye pembejeo, kama ilivyokuwa matrekta, majembe, mbolea na kadhalika. Hili naomba sana Serikali mkae mlifikirie, watu wa baharini ambao tunategemea kuvua sasa tunaiogopa bahari. Tunahitaji kulima tupate mahindi, mpunga, mtama na kadhalika; sasa kitoweo kiwe ng'ombe tu, inabidi kuwe na ng'ombe na samaki, watu wanahitaji *protein.* Tutakapowabana zaidi au kutokuwasaidia na iwe sisi kazi yetu kukamata na kuchoma moto, hatuwatendei haki. Kwa hiyo, ninachoomba Serikali kupitia fedha hizi za *EPA*, kama fungu hili halitatosha limeshapangiwa, sina matatizo nalo na wala sina hiyana kwa kupelekwa sehemu yoyote, kwa sababu atakayefaidika ni Mtanzania na mimi kama kiongozi wao, nawajibika kwa watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoiomba Serikali, kama ipo ziada ya hizi fedha; najua zipo zitakuja na Mheshimiwa Rais ameshasema kwamba, hizi zitakuja kwa manufaa ya Watanzania, basi litoke fungu maalum kwa ajili ya wavuvi katika kubadilisha zile zana tunazozisema haribifu. Wataalam wetu wanatuchanganya, matokeo yake sasa uharibifu unakuja, tunaharibu bahari na ni kweli tutakosa samaki na tutaendelea kuwa maskini. Tukizitumia fedha hizi kwa kuwaambia lete nyavu yako mbaya chukua hii nzuri, mimi nafikiri kutakuwa hakuna tatizo lolote. Wananchi wote wa Tanzania watafaidika na fedha hizi na nchi itapata kipato kizuri. Halmashauri zetu zitakuwa na fedha na Taifa litapata mchango kutoka sekta huru, kile kiasi tulichokuwa nacho kitazidi maradufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ya kusema, wakati umekwisha, naomba kwa heshima zote kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia noja. Naomba *pressure* za wavuvi zishuke na wao waweze kusaidiwa mashine za boti, nyavu, maboya, mishipi na nyuzi zile ambazo tunazitumia katika kushonea nyavu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naendelea kusema ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shah. Muda tuliobakia nao ni kama dakika tano ambazo Mheshimiwa Rished Abdallah amesema yeye zitamtosha. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Rished uchangie hizo dakika tano.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *economic crisis* ya dunia imetokana na *energy* (mafuta) na mafuta yamezaa matatizo mengi. Sasa hivi mafuta yameshuka, baada ya kushuka na hali ya hewa pia imesababisha *global warming*, ambayo inasababisha matatizo ya njaa. Chanzo kikubwa cha kuanguka kwa uchumi duniani, kimeanza na mafuta. Sasa mimi nataka kuishauri Serikali mambo yafuatayo:- Fedha za *EPA* hizi zipo, nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa uamuzi huu ambao ameufanya na sisi tunaukubali leo kupitisha hizi fedha, kwa ajili ya maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nasema kwa muda tuliokuwa nao na kwa fedha za *EPA* zilizobaki, badala ya sisi kununua mbolea kutoka nje, tazama gharama zake zinavyokuwa bilioni 30 na nyingine ni ruzuku ambazo hazirudi. Fedha hizi zilizokuwepo, kwa nini tusijenge Kiwanda cha Mbolea pamoja na kwamba azma ya Serikali ni kujenga Kiwanda cha Mbolea. Moja ya *raw material* ya kutengeneza hii mbolea sasa hivi tulinayo ni gesi. Kwa nini gesi sasa isitumike vizuri katika kutengeneza mbolea yetu?

Tulishazungumza wakati wa bajeti kwamba, gesi hii sasa itumike kupunguza matatizo ya *energy,* ambayo ni mafuta kwa ajili ya kuendeshea mitambo mbalimbali, magari na kadhalika ili tupunguze hii *inflation* ambayo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ameizungumzia.

Sisi tuko 13.5% kwenye chakula, Kenya wako 39%, sasa tusipoweka mikakati ya haraka kwa kutumia fedha hizi za *EPA* ambazo zimebakia naiomba Serikali, kwa haraka kabisa ifikirie utaratibu mzima wa kujenga kiwanda tuondokane kabisa na kununua mbolea, kwa sababu kila kukicha mbolea kuiagiza kutoka nje itazidi kupanda bei. Sasa jaribuni kuifikiria hiyo, gesi tunayo na fedha ipo; sasa mikakati hata kama ni kuingia *joint venture* tuingie, lakini kiwanda cha mbolea kiwepo kwa sababu tuna gesi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia hayo mawili tuondokane na matatizo ya *crisis* iliyopo duniani, ili nchi yetu tusije tukaingia katika mkumbo *inflation* ikawa ni kali zaidi na *resources* tulizokuwa nazo sasa hivi tuzitumie vizuri, hatimaye tuondokane na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rished. Waheshimiwa Wabunge, orodha tuliyonayo ni kubwa, watu walioomba ni wengi, lakini kwa leo na muda tulionao

hautoshi kumpa mchangiaji mwingine. Kabla sijaahirisha Kikao cha Bunge, kuna tangazo limeletwa na Katibu wa Chama cha Mapinduzi; anawataka Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi ya Wabunge wa CCM, wahudhurie kikao muhimu mara baada ya kuahirishwa Kikao cha Bunge leo katika ukumbi wao wa kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho tarehe 4 Februari, 2009 Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 4 Februari, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*